Jumatano Novemba 16, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581131
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ
nipasheTZ
nipasheTZ
0745 700710
LIKE & FOLLOW US



Ukurasa 19

**EDIMUND SENGONDO MVUNGI 1952- 2013 Jina kubwa linalodumu linaloendelea kuishi mioyoni mwa tasnia, sekta nyingi**

Ukurasa 16

DRC yatupa karata ya mwisho kwa mzozo wa Kivu Kaskazini

**siasa**

JUMATANO NOVEMBA 16, 2022 Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

**KUMPINGA RAIS MITANDAONI Vyama vyasisitiza uteuzi anaofanya Rais Mwinyi usisababishe taharuki**

CHADEMA MGOMO RUZUKU

**Wadai bado hawatambui uchaguzi 2020,Msajili vyama asita kuwagusa**

•Yasema viti maalumu haviongezi ruzuku

mbalimbali.

Hata hivyo, kwa upande wa ushindi matokeo ya uchaguzi huo yaliwapa mbunge mmoja Aida Khenani kutoka Nkasi Kaskazini.

Katibu Mkuu huyo anasema kiasi cha fedha za ruzuku ambacho chama hicho kinatakiwa kupokea ni Sh. milioni 109, kinachotokana na idadi ya kura za wabunge kuanzia asilimia tano na kuendelea, ambazo CHADEMA ilipata.

"Lakini kuna mbinu chafu ambazo zimekuwa zikienezwa kwamba fedha hizo ni za viti maalum 19, sio kweli, viti hivyo havichangii lolote katika ruzuku ya chama chochote cha siasa," anasema Mnyika.

Mwanasiasa huyo anadai mbinu hizo zinafanyika kwa ajili ya kutaka kuuminisha umma wa Watanzania kuwa viti hivyo ndivyo vinavyoleta ruzuku kwenye

UKURASA 13

SUPA JACKPOT
TZS.1,051,207,683
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



## CCM sasa yaonya rushwa uchaguzi wa mikoa, jumuiya

UKURASA 3

RIPOTI MAALUM:

# Ukame washusha thamani ya mifugo

• **Ng'ombe** auzwa hadi 150,000/- majani yawa lulu kwa wamiliki mashamba... *Endelea ukurasa 4*



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Elkaria, Kata ya Sepeko, wilayani Monduli wakiwa kwenye foleni ya kuchota maji nje ya nyumba ya mmoja wa mwananchi ambaye hununua bidhaa hiyo, jijini Arusha na kuwauzia wanakijiji kwa 1,000/- dumu moja la lita 20. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Dada, kaka wafungwa jela kumshambulia mama mzazi

UKURASA 2

## Kocha Simba mbaroni madai ya kukamatwa na dawa za kulevya

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA, NAMUNGO SOKA KUTEMBEA LEO** UK.32

**KABWELA** UK.7



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Uledi Abbas Mussa, akizungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa maadhimisho ya wiki ya shukrani kwa mlipakodi. Wengine ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Deudatus Balile (kushoto) na (kulia) ni Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kocha Simba mbaroni madai kukutwa na dawa za kulevya

**Na Waandishi Wetu**

KOCHA wa Makipa wa Timu ya Soka ya Simba, Muharami Sultan (40), mkazi wa Kigamboni mkoani Dar es Salaam, na wenzake wanane, wanashikiliwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), kwa madai ya kukutwa na kilo 34.89 za dawa za kulevya aina ya heroine.

Pia watuhumiwa wengine wawili wanadaiwa kukutwa na biskuti 50 zilizotengenezwa kwa kutumia dawa za kulevya aina ya bangi kama moja ya malighafi.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema watuhumiwa hao walikamatwa mwanzoni mwa mwezi uliopita kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama baada ya kufanyika operesheni maeneo mbalimbali.

Kuhusu tukio la heroine, Kamishna Jenerali Kusaya alisema wanamshikilia Sultan ambaye pia mchezaji wa zamani wa timu ya Simba pamoja na mtoto wa dada yake, Maulid Mzungu (40) maarufu Mbonde, mkulima na mkazi wa Kamegele Kisemvule.



Aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni mfanyabiashara na mmiliki wa Kituo cha Cambiasso Sports Academy kilichoko Tuangoma, Kigamboni, Kambi Seif (40) maarufu kama Alhaji Kambi, mkazi wa Oysterbay.

Pia alisema Seif ni mmiliki wa magari ya kusafirisha abiria kutoka Dar es Salaam kwenda mkoa wa Pwani na Fundi Seremala, Said Matwiko (41), mkazi wa Mahole A, Kivule.

Kamishna Jenerali aliwataja wengine ni mfanyabiashara John John (40) maarufu kama Chipanda, mkazi wa Magore, Kitunda, Rajabu Dhahabu (32) mkazi wa Tabata Segerea, Hussein Pazi (41) mkazi wa Kibugumo, Kigamboni na Ramadhani Chalamila (27) mkazi wa Mzinga, Kongowe.

Alisema upelelezi na kuwasaka watu wengine wanaotuhumiwa kujihusisha na biashara hiyo unaendelea na kwamba wakati wowote watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Alisema wanawashikilia watuhumiwa wengine wawili kwa kudaiwa kukutwa na biskuti 50 zilizotengenezwa na dawa za kulevya aina ya bangi.

Aliwataja kuwa ni Abnasir Kombo mkazi wa Kaloleni, Arusha aliyedaiwa kukutwa na biskuti 50 na mtengenezaji wake, Hassan Ismail (25) pia mkazi wa Arusha.

"Serikali haijalala bado tunaendelea na msako nchi nzima kwa hiyo wakae wakijua magereza yako wazi na wanaotarajia kutajirika na Dawa za Kulevya wasijisumbue tutawadaka," alionya.

**SIMBA YAMKANA**

Wakati hayo yakiendelea, uongozi wa Klabu ya Simba, katika taarifa yake iliyoitoa jana muda mfupi baada ya taarifa hiyo kutolewa, ilisema Muharami, maarufu kama Shilton, hakuwa mwajiriwa wa klabu hiyo.

"Simba ilimwomba na kukubaliana na ndugu Muharami kuwanoa makipa wetu kwa muda wa mwezi mmoja, wakati huo klabu ikiendelea kutafuta kocha wa magolikipa.

"Kwa mantiki hiyo, klabu haihusiki na tuhuma zinazomkabili kocha huyu, uongozi wa Simba unaomba mashabiki wa klabu hii, kuwa wavumilivu kwani hakuna athari yoyote kwa klabu kutokana na kadhia iliyomkumba kocha huyo," ilisema taarifa hiyo.

# Dada na kaka wahukumiwa kifungo kwa kumshambulia mama yao mzazi

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Ilala imewahukumu kifungo cha miaka minne jela Zulfikar Safraz na dada yake, Nurin Safraz, kwa kumpiga na kumshambulia kwa matusi mazito mama yao mzazi, Maria Vazi.

Wanandugu hao walitiwa hatiani jana mbele ya Hakimu Mkazi Rehema Liana baada ya kukubaliana na hoja za rufani zilizowasilishwa na mama yao akipinga uamuzi wa Mahakama ya Mwanzo Kariakoo uliowaachia huru.

Liana, akisoma hukumu hiyo, alisema mrufani hakukubaliana na uamuzi wa kuachiwa huru washtakiwa na katika kesi hiyo ya jinai ya Septemba mwaka huu upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi watatu.

Akisoma ushahidi alisema siku ya tukio maeneo ya Ilala, Mtaa wa Tanga na Utete, Zulfikar alikuta watoto wakicheza nje ya nyumba yao, aliwafukuza huku akiwatukana ndipo mama yake alipomkataza kufanya hivyo.

Alisema mshtakiwa alipokatazwa aliamua kuanza kumtukana mama yake matusi mazito, alimsukuma na kumpiga.

Hakimu Liana alisema mashahidi watatu wote walishuhudia tukio hilo la kaka na dada kumshambulia mama yao, kupigwa na kutukanwa, kulikomfanya mama huyo kuhama nyumbani kwake.

"Mahakama ya Mwanzo ilikubaliana na ushahidi wa mashahidi, ilikubali kwamba washtakiwa walimtukana mama yao, walimpiga lakini mahakama hiyo iliwaachia huru washtakiwa kwa sababu hakukuwa na PF 3," alisema Liana.

Alisema kutokana na uamuzi huo, aliukatia rufani akiwa na hoja kwamba mahakama ilighafilika kuwaachia huru bila kuzingatia ushahidi wa upande wa Jamhuri na ushahidi wa kuona wa mashahidi watatu.

Hakimu Liana alisema mrufani alishambuliwa na watoto wake na hakuna ubishi na iko wazi katika hukumu ya Mahakama ya Mwanzo.

"Kigezo cha kutokuwepo kwa PF 3 ni hoja ambayo hakuna upande wowote uliozungumzia. Hoja iliibuliwa na Hakimu mwenyewe akajibu," alisema Hakimu Liana.

Alisema baada ya kusikiliza rufani hiyo anakubaliana na hoja za mrufani na kuwatia hatiani washtakiwa wote wawili kwa mashtaka yanayowakabili.

Walipoulizwa kama wana makosa ya zamani ili mahakama ijue na kutoa adhabu, kaka na dada waliibuka na kuzungumza tuhuma mbalimbali dhidi ya mama yao.

Kaka: Mama huyu ameshanifunga mara tano, kila kesi mwaka mmoja mmoja na kuna kesi nyingine nilifungwa 10.

Kaka: Siku moja tumetoka disko usiku tunagonga akasema tunampigia kelele, tukalala nje, akaita polisi wakatukamata nikafungwa. Nilikuwa na mdogo wangu jela, mama anachukua kodi zetu, alibadilisha majina kwenye nyumba anadai tumekufa.

Aliendelea kudai kwamba: "Katika kesi nyingine nilifungwa miezi sita Wazo, nilipasua mawe, nilipomaliza kifungo nilirudi kama filimbi nimekonda. Kesi nyingine nasafiri akanichongea nasafirisha dawa za kulevya.

"nikakamatwa Uwanja Ndege nikafungwa miaka kumi, hajaridhika sababu sijafa, mama anarudi nyumbani saa nne usiku mpaka saa tano usiku. Yuko baba wa kambo anakula hela zetu."

Dada; Mheshimiwa huyu mama anajifanya mnyonge hapa, hatujamkosea, yeye kila siku matusi nyumbani hakuna amani. Sasa hivi tunaamani sababu nyumbani yupo mdogo wake lakini asingekuwepo matusi na ugomvi vingekuwepo. Akirudi saa tano usiku ananikuta nimeshalala, sasa hivi tuna amani.

Mama: Niliwazaa kwa mapenzi, nikawasomesha hadi kufika hapa ni nguvu zangu lakini naishi kama mfungwa nyumbani kwangu, napigwa na kuvuliwa nguo.

Hakimu Liana alisema mahakama imezingatia hoja zilizowasilishwa na washtakiwa, itatoa adhabu ili iwe fundisho kwa watoto wengine.

"Kutokana na mashtaka yenu, mahakama inawapa adhabu. Mshtakiwa wa kwanza Zulfikar utakwenda jela miaka minne na mshtakiwa wa pili Nurin utakwenda jela miaka mine, mnayo haki ya kukata rufani, "alisema Hakimu Liana.

# Waziri aipa DART maagizo 18 katika kuboresha utendaji

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ameipa maagizo 18 Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) kuboresha usafiri huo.

Alitoa maagizo hayo jana Dar es Salaam, wakati akizundua Bodi ya Ushauri ya Wakala itakayoongozwa na Katibu Mkuu mstaafu, Dk. Florence Turuka.

Kairuki alisema pamoja na kulalamikia changamoto ya mapato, DART inapaswa kuangalia upya idara yao ya fedha ili kuiboresha na kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya fedha.

Aliwataka kuwa wabunifu wa vyanzo vya mapato, akitoa mfano wa matangazo yanayowekwa kwenye mabasi yao yakiwamo yale ya kidijitali ambayo yanaweza kuwaingizia mapato mengi.

"Agizo lingine ni stahiki za wafanyakazi 163 mlio nao na hili nimekuwa nikilisisitiza kila ninakokwenda maana hawa wasipoangaliwa vizuri, si rahisi kutimiza wajibu wao. Kwa hiyo muwe mnaangalia hoja zao mara kwa mara, mtoe motisha na kulipa madai yao kwa wakati," alisema.

Aidha, alisema bodi hiyo inapaswa kuangalia namna ya kuanzisha usafiri wa namna hiyo kwenye majiji mengine nchini suala ambalo alisema liliwahi pia kusisitizwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwenye moja ya mikutano.

"Hili liwekeeni kipaumbele tuone tunaendaje nje ya Dar es Salaam. Angalieni kwa makini tuanzie wapi na tumalizie wapi na pia muanze kutafuta fedha za kujenga miradi hiyo. Wa mikoani nao ni Watanzania na wangependa kupata huduma ya usafiri huu," alisema.

Pia aliitaka DART kuangalia hoja zote za ukaguzi zilizoainishwa na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na hoja mbalimbali zilizokuwa zikitolewa na wabunge kwa nyakati mbalimbali tangu wakala kuanza ili kama wakiulizwa maswali hayo leo wawe na majibu yake.

Alisema hatarajii kuona hoja zile zile zinajirudia rudia wakati wa ukaguzi wa CAG kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 na aliwataka kuwatumia wakaguzi wao wa ndani na wahasibu kuhakikisha wanapata hati safi.

Aliipongeza DART kwa kuanzisha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwa kutumia wataalamu wa ndani huku akiagiza kadi za kielektroniki zikamilike mapema kuondokana na tiketi za makaratasi.

"Mmeniambia kadi zitakamilika Februari, mwakani, lakini hakikisheni zinakuwa na viwango na ambazo haziwezi kughushiwa maana unaweza ukawa na kadi ambayo baada ya mwezi imeshaanza kufutika," alisema.

Kairuki aliitaka bodi hiyo pia kutathmini miaka 15 tangu kuanzishwa kwa wakala kama kuna mafanikio yamefikiwa na changamoto zilizoko ili watafute namna ya kuzitatua na kusonga mbele.

Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Edwin Mhede, alisema wateja wa mabasi hayo wataanza kutumia kadi janja kupanda mabasi hayo mwakani na hawatalazimika kukata tiketi kama ilivyo sasa.

Alisema kadi janja zitasaidia pia kuondoa foleni zinazoonekana kwenye mabasi ya mwendokasi hivyo kupunguza muda wa abiria kusubiri basi na wameweka mifumo ya TEHAMA kurahisisha utendaji wa kazi mbalimbali za wakala.

Dk. Mhede alisema tangu wameanza kutoa huduma hizo za usafiri wamefanikiwa kupunguza muda wa kusubiri usafiri huo na kwamba kabla ya utekelezaji wa DRT 1, wasafiri kutoka Kimara kwenda Posta walikuwa wanatumia saa tatu kufika katikati ya mji.

"Sasa ninapozungumza mambo yamebadilika kwani ni wastani wa dakika 40 kufika mjini lakini bado tunasema haitoshi tunapoendelea kudhibiti changamoto mbalimbali tutaendelea kupunguza huo muda," alisema.

# CCM yaonya rushwa uchaguzi wa mikoa

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) katika mikoa kimetangaza ratiba ya kuanza uchaguzi wa ngazi mbalimbali na jumuiya huku kikionya wagombea waliopitishwa kugombea nafasi hizo kutojihusisha na vitendo vya rushwa.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kuhusiana na uchaguzi huo, makatibu wa mikoa walionya wagombea wao huku kikisisitiza wagombea wafuate maadili na si vinginevyo.

Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma, Pili Augustino, wakati akitangaza ratiba ya uchaguzi huo, aliwaonya wagombea watakaojihusisha na vitendo vya rushwa. Alisema uchaguzi utakaoanza ni wa jumuiya ngazi ya mkoa kwa leo kufanyika wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) na kesho Umoja wa Wanawake wa Tanzania na Ijumaa ni Jumuiya ya Wazazi.

"Wagombea wasitumie fedha wala kufanya kampeni zinazovunja kanuni. unapokwenda kuzunguka kuomba kura, unaleta ushawishi kwa wajumbe. Yeyote atakayekamatwa atachukuliwa hatua," alisisitiza.

Alitaja walioteuliwa kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa UWT ni Neema Majule, Kaundime Kasase, Elizabeth Lameck na Zabibu Maftaha.

Katibu huyo alitaja walioteuliwa kuwania nafasi ya Baraza Kuu la UVCCM ni Manishozi Mazanda, Linus Marko, Barikieli Selemani.

"Jumuiya ya Wazazi walioteuliwa nafasi ya Mwenyekiti ni Dk. Damas Mukasa, Samwel Malecela, Peter Makasi, kwa upande wa Baraza Kuu la Jumuiya hii ni Siwajibu Clavery, Jafari Mwanyemba, Ally Mohamed, Vivian Komu, Tumsifu Mwasamale," alisema.

Naye Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Adamu Ngalawa, aliwataka wagombea kutojihusisha na vitendo vya rushwa katika uchaguzi huo ambao mkoani humo unatarajia kufanyika Novemba 21, mwaka huu.

"Wagombea wote wajihadhari na kutoa rushwa katika kipindi hiki chote cha mchakato wa uchaguzi wafuate maadili ya uchaguzi na si vinginevyo," alisema Ngalawa.

Aliwataja waliopitishwa kugombea nafasi ya uenyekiti wa CCM mkoa wa Dar es Salaam kuwa ni Kate Kamba ambaye anatetea nafasi yake, aliyekuwa Mbunge wa Temeke, Abbas Mtevu, Baraka Konisaga, Jamal Rwambow.

Ngalawa alisema wanaogombea ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) kupitia mkoa ni Edmund Lyatuu, Dk. Walter Nnko, Juma Simba na Prof. Mary Kitula.

Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Shaibu Akwilombe, aliwataja wagombea kwa nafasi ya Mwenyekiti kuwa ni Mchungaji Jacob Mwakasole ambaye anatetea kiti hicho akipambana na Dk. Stephen Mwakajumilo, Devotha Sanga na Said Salimin.

Nafasi ya Mjumbe wa NEC, wanaogombea ni Agnes Mgoma, Ndele Mwaselela, Christopher Uhagile na Saul Mwaisenye huku Jumuiya za Chama wanaowania nafasi ya uenyekiti wa Vijana mkoa ni Agrey Mwaijande, Yasin Ngonyani na Baraka Chalamila.

Nafasi ya Mjumbe wa Baraza Kuu Taifa-Vijana kupitia mkoa ni Gabriel Kilembe, Moses Kasumo, Timida Fyandomo na Stephen Halinga huku nafasi ya Uenyekiti wa Wazazi Mkoa ikiwaniwa na Frank Maemba, James Mwampondele, Moses Mwidete na Fatuma Kasenga.

Kutoka mkoani Mwanza, aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Anthony Diallo, amekatwa huku nafasi hiyo ikiwaniwa na Dk. Sillivanus Nyanda, Reuben Chijabu na Nyiriza Makongoro Nyiriza.

***• Imeandaliwa na Agusta Ngoji (DOM), Grace Mwakalinga (MBEYA), Beatrice Shayo (DAR) na Vitus Audax (MWANZA).***


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
15.10.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Kampuni ya **FM CARGO LTD** inatarajia kusafirisha mizigo mipana (kuanzia tarehe 17/11/2022) kutoka **Dar es Salaam kwenda Kigoma** kwa kutumia magari yafuatayo,
   **T927BCR / T205AQM,**
   **T378DHX / T687DKZ,**
   **T109DYK / T741DYS,**
   **T579DPF / T791DEA,**
   **T231DTW / T265CBX**
2. Gari hizo zina vipimo kama ifuatavyo
   **Urefu... mita 20m**
   **Upana...mita 3.99m**
   **Kimo......mita 5m**
3. Njia itakayotumika: **Dar es salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida na Tabora.** Gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117149702



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
16.11.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe **17-11-2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji,** gari hizo zina namba za usajili:
   **T 624 DFA / T 137 CHN T 118 EAG / T 269 DUH T 204 DYG**
   **T 499 DXZ T 859 DXS / T 139 CHN T 649 BZU / T 146 CHN**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 24.00**
   **Upana - mita 5.45**
   **Kimo - mita 5.20**
3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji** kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117149902



WAPAMBANAJI
**KATEMANA AUCTION MART & GEN. SUPPLIES**
(Auctioneers. Brokers. Debt Collectors. Estate Agents & Commission Agents)

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KWA WADAIWA WA BENKI YA VISION FUND (VFT – MFB) TAWI LA NJOMBE,IRINGA NA SINGIDA**

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu Benki ya **Vision Fund Tanzania (VFT – MFB)** tutauza kwa njia ya munada wa hadhara mali zilizo orodheshwa hapa chini ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo minada itafanyikia mahali zilipo mali hizo siku na saa kama zinavyoonyesha katika jeduwali lifuatalo:-


| No. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA NA MAHALI ILIPO | DHAMANA IPO KWA JINA LA | NYARAKA ILIYOWEKWA NI | TAWI | SIKU NA TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MAKWAYA FREDRICK MHAKILICHA | NYUMBA-SIGRID KIVAVI-MAKAMBAKO | MAKWAYA FREDRICK MHAKILICHA | LESENI YA MAKAZI | NJOMBE | Jumamosi Tar.26/11/2022 Saa 4.00 Asubuhi |
| 2. | GEOPHREY NICOLAUS MPETE | SHAMBA-NGALANGA | GEOPHREY NICOLAUS MPETE | HATI YA URITHI | NJOMBE | Jumamosi Tar.26/11/2022 Saa.10.00 Jioni |
| 3. | GODLOVE BRAYTON MBENI | SHAMBA-SAKALENGA | GODLOVE BRYTON MBENI | HATI YA URITHI | NJOMBE | Jumapili Tar.27/11/2022 Saa.4.00 Asubuhi |
| 4. | BURA GODLOVE MBENI | SHAMBA- SAKALENGA | BURA GODLOVE MBENI | HATI YA URIYHI | NJOMBE | Jiumapili Tar.27/11/2022 Saa.6.00 Mchana |
| 5. | JAMES LAMSON NDONDOLE | SHAMBA-SAKALENGA | JAMES LAMSON NDONDOLE | HATI YA URITHI | NJOMBE | Jumapili Tar. 27/11/2022 Saa.8.00 Mchana |
| 6. | LISTON GEORGE SANGA | NYUMBA-KIMBENGWA | LISTON GEORGE SANGA | BARUA YA MAUZIANO | IRINGA | Jumamosi Tar.03/12/2022 Saa 4.00 Asubuhi |
| 7. | ALEX JOHN KIBANGALI | NYUMBA-MTWIVILA SEKONDARI | ALEX JOHN KIBANGALI | BARUA YA MAUZIANO | IRINGA | Jumamosi Tar.03/12/2022 Saa.6.00 Mchana |
| 8. | KEFFA ABRAHAM CHENGULA | NYUMBA-ILALA IRINGA MJINI | KEFFA A.CHENGULA | HATI MILIKI | IRINGA | Jumamosi Tar.03/12/2022 Saa.8.00 Mchana |
| 9. | ELIZEKIEL CHESCO LUVINGO | NYUMBA-NDIWILI KILOLO | ELIZEKIEL C.LUVINGO | HATI YA KIMILA | IRINGA | Ijumaa Tar.02/12/2022 Saa.4.00 Asubuhi |
| 10. | RENATUS MSIMBILA | NYUMBA-NDIWILI KILOLO | RENATUS MSIMBILA | HATI YA KIMILA | IRINGA | Ijumaa Tar.02/12/2022 Saa.6.00 Mchana |
| 11. | JULIANA JACOB | NYUMBA-UNYANKAE | JULIANA JACOB | BARUA YA MAUZIANO | SINGIDA | Jumamosi Tar.10/12/2022 Saa.4.00 Asubuhi |
| 12. | STELLA MICHAEL MBUTU | NYUMBA-KIMPUNGUA | ALLY MOHAMED NKENDWA | OFFER LETTER | SINGIDA | Jmamosi Tar.10/12/2022 Saa.6.00 Mchana |

**MASHARTI YAMNADA**

i. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa katika mnada,salio litalipwa ndani ya siku 14 toka tarehe ya mnada huo
ii. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa muda huo atakuwa amepoteza haki yake ,mnada utarudiwa 25% haitarejeshwa.
iii. Wateja wataruhusiwa kukagua mali husika kabla ya mnada.
iv. Mali itauzwa kama ilivyo.
v. Gharama za usajili/ ubadilishwaji umiliki ni jukumu la mnunuzi.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**
**MKURUGENZI MTENDAJI :**
**KATEMANA AUCTION MART & GS MOBILE :0763 452 525 / 0784 988 615**
**AU FIKA TAWI HUSIKA.**

117149302



Mfugaji Mollel Losullu akisaka malisho ya mifugo yake wilayani Handeni, Tanga. **PICHA: JENIFER GILLA**

# Ukame ulivyoshusha thamani ya mifugo

- Majani yawa lulu kwa wamiliki wa mashamba
- Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo watikiswa

**Na Jenifer Gilla, aliyekuwa**

HANDENI

NI majira ya alfajiri, anaonekana Joshua Godliver (45) akiwa njiani na mifugo yake kwa safari kuelekea kijiji jirani cha Kingona kusaka malisho ya mifugo yake.

Mkazi huyo wa Kijiji cha Sindeni, Kata ya Sindeni, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, anabainisha ni kawaida kwa wafugaji kuamka alfajiri ili kuiwahisha mifugo yao kijijini Kingona kuliko na uhakika wa malisho kwa sasa kutokana na ukame uliokikumba kijiji chao (Sindeni).

Godliver mwenye ng'ombe takribani 100 na mbuzi 70 anaeleza kuwa kabla ya kuchukua uamuzi wa kuihamishia Kingona mifugo yao, walikuwa wanatembea umbali mrefu uliochukua wakati mwingine saa mbili safarini kuyafikia maeneo yenye malisho, hali iliyozorotesha afya za mifugo yao.

"Kutokana na kutembea mwendo mrefu, sisi wenyewe tulikuwa tunachoka na kuumwa kwa sababu jua linatupiga siku nzima, lakini pia mifugo ilikuwa inakonda kwa sababu ya kushinda juani siku nzima, sasa hivi tunashukuru afya za mifugo zimeanza kuimarika," anasema.

Ni shida inayopatiwa ufafanuzi zaidi na Ofisa Mifugo wa Kata ya Sindeni, Dotto Deus, anayekiri iko kwa wafugaji wengi, akibainisha mwaka huu wametoa vibali zaidi ya 100 vya kuhamisha mifugo na wanaendelea kupokea maombi.

"Tumetoa vibali vingi, lakini wafugaji waliohamisha mifugo ni zaidi kwa sababu wengine wanaungana wawili hadi wanne na kuomba kibali kimoja. Wale wenye mifugo zaidi ya 50 wote wamehamisha mifugo kutokana na ukame," anasema Deus.

Mfugaji Zubeda Ndimwe anasema baada ya kuhamishia mifugo yake katika Kijiji cha Mswaha kilichoko Kata ya Mswaha, anaona afya zao zikiimarika tofauti na walipokuwa kijijini Sindeni.

"Ilibidi nifanye uamuzi mgumu, kwa sababu ilifika mahali ng'ombe niliyekuwa ninamuuza Sh. 300,000 ninamuuza bei ya hasara ya Sh. 150,000 kwa sababu walikuwa wamekonda sana kulinganisha na ng'ombe wanaotoka yanakopatikana malisho mazuri," anasimulia.

> **Kuhusu maji, kule kuna afadhali kidogo kwa kuwa kuna Ruvu (Mto Pangani) ingawa changamoto iliyoko ni umbali kwani inatulazimu kutembea saa mbili na nusu kufika eneo hilo, hivyo tunalazimika kwenda kila baada ya siku moja ili kuipumzisha mifugo.**

Zubeda anasema kijijini kwao Sindeni kuna maeneo yenye majani yanayofaa kwa malisho ya mifugo, lakini wamiliki wake wanataka walipwe fedha kwanza ndipo mifugo iruhusiwe kuingia, jambo ambalo kwake aliona si sahihi kuyageuza majani biashara ya kujinufaisha kiuchumi.

"Kuhusu maji, kule kuna afadhali kidogo kwa kuwa kuna Ruvu (Mto Pangani) ingawa changamoto iliyoko ni umbali kwani inatulazimu kutembea saa mbili na nusu kufika eneo hilo, hivyo tunalazimika kwenda kila baada ya siku moja ili kuipumzisha mifugo," anasema.

Mollel Lolusu anakumbuka hasara aliyoipata kutokana na ukame, akibainisha kuwa kabla ya kuhamishia mifugo yake katika Kijiji cha Mswaha, alipoteza ng'ombe watano waliokufa kutokana na kukosa malisho na maji.

**RANCHI ZA TAIFA**

Kukabiliana na ukame, mfugaji Mwanahawa Omari anaiomba serikali itenge na kuwapatia maeneo ndani ya ranchi ya taifa iliyoko Kijiji cha Nzeli ili wapate malisho ya mifugo yao kwa kuwa wamekuwa wakikamatwa wanapokutwa kwenye maeneo hayo.

"Sisi hatutaki kupewa bure, watupe vitalu vya kulipia, mradi mifugo yetu ipate sehemu ya kula kwa sababu hata huko tulikohamishia mifugo, pia tunalipia na ni mbali, inatulazimu kuamka usiku kwenda kulisha mifugo," anawasilisha kero zao.

Ofisa Mifugo wa Kata ya Sindeni, Dotto Deus, anasema wanawapatia elimu ya ufugaji wa kuku, kwa kuwa hawana mahitaji makubwa kulinganisha na mifugo waliyoizoea, ili wawe na njia zingine za kujipatia kipato.

"Kwa kuwa mifugo waliyonayo sasa utunzaji wake unahitaji uwe na fedha nyingi, tunawafundisha kufuga kuku ili wanapowauza wapate fedha ya kununua majani ya kulisha mifugo yao, pia kupata fedha ya haraka ya kuhudumia familia kwa kuwa hawa wanakua ndani ya muda mfupi," anafafanua.

**MIKAKATI SERIKALINI**

Ofisa Mifugo Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Sekiara Kiariro anakiri eneo lake la kazi kukumbwa na tatizo hilo, akisema serikali inafanya jitihada za kuwasaidia wananchi kupunguza makali ikiwamo kuwajengea mabwawa ya kuhifadhi maji ya mvua kwa ajili ya kunywesha mifugo.

"Mpango wa halmashauri ni kuwa fedha ikipatikana, itajenga mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya mifugo, lakini kwa sasa hatujapata, wakati wowote tukipata tunaanza utekelezaji," anaahidi.

Kiariro pia anawashauri wakulima wapunguze mifugo walionayo kwa kuiuza na kuwekeza kwenye shughuli nyingine ili wawe na mifugo michache wanayoimudu kuipa huduma zote stahiki kulingana na hali ya ukame iliyoko japo mwitikio wao katika hilo ni mdogo.

Kuhusu pendekezo la mfugaji Mwanahawa serikali kuruhusu mifugo yao kupata malisho kwenye ranchi za taifa, Ofisa Mifugo Kiariro anakiri kupokea maombi hayo lakini wameshindwa kuchukua uamuzi huo kwa kuwa maeneo hayo hayamilikiwi na halmashauri, bali Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na kuwashauri waende kuomba kibali kwa mamkala hiyo.

"Kwa sababu suala la maji na chakula ni mtambuka, kwetu sisi kwa sababu tunategemea mvua kwa ajili ya majani kukua na kunywesha mifugo, hata hayo mabwawa tutakayojenga pia tutategemea mvua ili kuyajaza," anasema.

Mikakati hiyo imekuja baada ya Tanzania kupitia makubaliano ya Paris kuandaa mpango kabambe wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi wa 2030, ikiahidi kufanya mambo mbalimbali kusaidia wafugaji kukabiliana na athari hizo.

Tanzania pia imeahidi kuimarisha miundombinu na huduma za mifugo inayostahimili mabadiliko ya tabianchi, kuboresha njia zinazofikiwa na wafugaji dhidi ya majanga yanayohusiana na athari hizo, ikiwamo bima ya mifugo, kuimarisha tija ya mifugo kupitia afua zinazozingatia hali ya hewa na kuimarisha utafiti na maendeleo ya mifugo.

**HALI YA MIFUGO**

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), mwaka 2021, Sekta ya Mifugo ilikua kwa asilimia tano kutoka mwaka 2020, huku mchango wake katika Pato la Taifa ukiwa wa asilimia saba.

NBS ilibainisha Tanzania mwaka huo ilikuwa na ng'ombe milioni 35.3, mbuzi milioni 25.6, kondoo milioni 8.8, kuku milioni 92.8 na nguruwe milioni 3.4.

Kwa mujibu wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea kukumbwa na athari za mabadiliko ya tabianchi zikiwa na majanga kama vile mafuriko na ukame, yanayoathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za kiuchumi na kurudisha nyuma juhudi za kupunguza umaskini.

Ni athari zinazoathiri utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999-2025 yenye dhima kuu ya kupunguza walau nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya waishi katika uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.

## HABARI KITAIFA



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), Dk. Siston Masanja, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya wakala huo katika mwaka wa fedha 2022/2023. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tanzania yapongezwa kupunguza kasi ya maambukizi ya VVU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA imetajwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Ukimwi (UNAIDS) kufanikiwa kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU).

Kwa mujibu wa takwimu mpya, maambukizi yamepungua kutoka watu 110,000 hadi 54,000 kila mwaka huku zikibainisha kuwa theluthi ya maambukizi hayo mapya, yanatokea kwa vijana.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, aliyasema hayo jana kwa waandishi wa habari jijini hapa ikiwa ni kuelekea maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani Desemba Mosi. Maadhimisho hayo kwa mwaka huu, yatafanyika mkoani Lindi.

"Nchi yetu imepiga hatua za kutosha na zinatia moyo kwenye mapambano ya VVU. Mtendaji Mkuu wa UNAIDS kwenye kongamano la kisayansi lililofanyika Canada mwaka huu, alizungumza moja ya nchi zilizofanya vizuri ni Tanzania katika kupunguza maambukizi mapya," alisema.

Alisema miaka 12 iliyopita, mambukizi hayo yalikuwa watu 110,000 kila mwaka na kufikia mwaka 2021 ni watu 54,000 huku akisema vijana wenye umri wa miaka 15-24 maambukizi mapya yanatokea kwa asilimia 30 ambayo ni takribani theluthi.

"Ni pungufu karibu ya nusu ya maambukizi mapya, lakini vifo vimepungua kwa asilimia 50 kutoka 64,000 mwaka 2010 hadi 29,000 mwaka 2021. Haya ndiyo mafanikio tunayojivunia kama nchi. Pamoja na mafanikio haya, tunahitaji kuongeza nguvu kufikia malengo ya 0-0-0 mwaka 2030," alisema.

Dk. Maboko alisema katika malengo ya kufikia sifuri tatu mwaka 2030, ya 90-90-90 ambayo kwa sasa ni 95-95-95, yaani ya kwanza ni kuhakikisha watu wanaokadiriwa kuwa na VVU wanajua hali zao, ya pili ni wanaojua hali zao wameanza dawa za kufubaza VVU, na ya tatu ni asilimia 95 wawe wamefubaza VVU.

"Makadirio yaliyofanyika mwaka 2016/17 asilimia 61 tu katika ile 95 ya kwanza walikuwa wanajua hali zao lakini hadi kufikia mwaka 2021 tunazungumzia asilimia 89.7. Lakini 95 ya pili ya kuanza dawa kumekuwa na ongezeko pia. Mwaka 2016/17 ilikuwa asilimia 95 lakini mwaka 2021 ni asilimia 99, lile ongezeko kwenye kufubaza VVU mwaka 2016/17 ilikuwa asilimia 87 sasa 2021 asilimia 96," alisema.

Kuhusu maadhimisho ya Siku ya Ukimwi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, George Simbachawene, alisema kutakuwa na maonyesho ya wiki nzima ya wadau wanaoshughulika na mapambano ya Ukimwi mkoani Lindi.

Alisema kutakuwa na kijiji cha vijana kutokana na nguvu inahitajika kwenye kuimarisha usawa na ni eneo ambalo linakabiliwa na maambukizi mapya, hivyo aliagiza mikoa yote nchini kuandaa na kuadhimisha siku hiyo.

Mkurugenzi Mkazi wa UNAIDS Tanzania, Martin Odiit, alipongeza Tanzania kwa kuendelea kupiga hatua kwenye mapambano dhidi ya VVU na kwamba kaulimbiu ya mwaka huu inatoa wito wa kuchukua hatua.

"Ni wajibu wa kila mmoja kuhakikisha anashughulikia ukosefu wa usawa na kusaidia kumaliza Ukimwi na itawezekana kwa kuongeza upatikanaji na ubora wa huduma," alisema.

# ACT-Wazalendo yapingwa uteuzi Mkurugenzi NEC

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAULI ya Chama cha ACT- Wazalendo kupinga uteuzi wa Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Thabit Idarous Faina, imeua mjadala visiwani hapo na kusababisha baadhi ya vyama vya siasa Zanzibar kulaani huku vikieleza kuwa ACT inaingilia uamuzi wa Rais Hussein Ali Mwinyi.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia Makini, Ameir Hassan Ameir, alisema viongozi wa ACT-Wazalendo wanatumia uteuzi huo kuwarudisha nyuma Wazanzibar kulumbana.

"Kwa mujibu wa taratibu na sheria za Zanzibar Rais Dk. Mwinyi anaendesha vizuri Serikali ya Umoja wa Kitaifa na ndiyo maana tupo na uhuru kwa kufanya mambo yetu," alisema.

Alisema kitendo cha chama hicho kushinikiza kutengua uteuzi wake ambao ametoa hivi karibuni inaonesha wazi ubinafsi wa chama hicho.

"Rais Dk. Mwinyi ana uwezo wa kumteua mtu yeyote ambaye anamuona anafaa kushirikiana naye katika kuwaletea maendeleo Wazanzibar na hiyo ndiyo dhana ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa," alisema.

Alisema kitendo kinachofanywa na ACT-Wazalendo ni kumvunjia heshima Rais Mwinyi na kwamba kinachotakiwa ni chama hicho kurejea kwenye mstari.

Katika maelezo yake Katibu Mkuu huyo aliwataka Wazanzibar kutokubali kuyumbishwa, kurudishwa nyuma na kuingizwa kwenye mifarakano isiyokuwa na ulazima.

"Sasa hivi Zanzibar tunataka kujenga nchi yetu na mheshimiwa Rais ameshasema kuwa tunatarajia kujenga barabara za juu hivyo tumuache afanye kazi zake tusimwingilie," alisema.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Jumuiya ya Wanawake UDP, Naima Salum Hamad, alisema kuwa vyama vya siasa ambavyo vimedhamiria kuichafua serikali ya umoja wa kitaifa vinakumbushwa kutosahau vipindi vilivyopita kilichobaki ni kuipeleka Zanzibar mbele.

"Tunaoathirika zaidi ni kinamama na watoto, watu wenye ulemavu na wazee na tukirudi nyuma tutaiweka wapi Zanzibar yetu na kwa sasa ipo vizuri ikilinganishwa na zamani tulikuwa hatuzikani, hatusalimiani," alisema.

Katibu Mkuu wa Chama cha UPDP, Hamad Mohamed Ibrahim, alisema ACT-Wazalendo inapaswa kutambua kuwa sio Wazanzibar wote wapo kwenye siasa na kwamba dhamira yao hiyo itawatesa watu hao. Alisema vyama hivyo havitakubali kutokea kwa hali hiyo, wanaungana na Rais Mwinyi kuwaletea maendeleo Wazanzibar ambaye alitoa ahadi wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2020.

"Inasikitisha kuona Rais anafanya uteuzi ambapo wenzetu hawajaridhishwa wao wanakataa kitendo hicho ni cha kukebei na kuingilia mamlaka na maamuzi ya Rais," alisema.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Magonjwa yasiyoambukiza yanaweza kudhibitiwa

**JAMII** inaweza kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza ambayo kwa sasa yanaelezwa kuwapata Watanzania wengi kutokana na kutotilia maanani ulaji ulio sahihi na kufanya mazoezi.

Magonjwa yasiyo ya kuambukiza ni yale ambayo hayasambazwi kwa mtu mwingine kwa kuwa hakuna vimelea mwilini vinavyohusiana na magonjwa hayo. Magonjwa hayo ni moyo, shinikizo la damu, figo, saratani, kifua sugu, kisukari, magonjwa ya akili, magonjwa ya kinywa na meno na mengine ya kurithi kama vile ugonjwa wa selimundu.

Tanzania, katika mpango wa upimaji wa afya kwa magonjwa yasiyoambukiza jijini Dar es Salaam, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umebaini kuwa idadi kubwa ya wanaume wanapatwa na magonjwa hayo kuliko wanawake.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mfuko wa Bima ya Afya, athari ya magonjwa yasiyoambukiza ni mara nne zaidi ya watu waliopo mijini kuliko vijijini, huku asilimia 12.8 ya wanaougua wakiwa wako mijini na asilimia 3.1 wako vijijini kutokana na mfumo wa maisha.

Magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanaelezwa kusababishwa na ulaji usiofaa na mtindo usio bora wa maisha kwa kutumia vyakula vyenye chumvi nyingi, mafuta mengi au vinywaji vyenye sukari nyingi ikiwa ni miongoni mwa viashiria hatarishi vya kupata magonjwa yasiyoambukiza.

Kulingana na utafiti mbalimbali uliofanywa, unaonesha kuwa kuna ongezeko kubwa la watu wenye uzito uliozidi pamoja unene uliokithiri na kuwaweka watu kwenye hatari ya kupata tatizo la magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama kisukari, saratani pamoja na magonjwa ya moyo na shinikizo la damu.

Mtindo usio bora wa maisha ni kutofanya mazoezi, matumizi ya sigara na tumbaku pamoja na unywaji wa pombe ambavyo husababisha mtu kupata magonjwa hayo.

Magonjwa hayo yana athari kubwa katika maendeleo ya taifa, lakini yanawezekana kudhibitiwa endapo elimu kwa jamii itatolewa kwa kuandika taarifa sahihi ili watu waweze kufuata taratibu za ulaji unaofaa na mtindo bora wa maisha.

Kwa mujibu wa Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa la Usalama, John Ashe, mwelekeo wa kufa kwa magonjwa hayo ni asilimia 10 kwenye nchi zilizoendelea na asilimia 60 kwenye nchi zinazoendelea. Tofauti hiyo kubwa inakumbusha kwamba suluhu la jumla linaomba ushirikiano wa wadau wote kupambana na magonjwa hayo ili watu wasiendelee kuathiriwa.

Ili kudhibiti magonjwa hayo yasishambulie zaidi, watu wanashauriwa kula mlo ulio bora na kuzingatia mazoezi.

Inashauriwa watu wapunguze vyakula vyenye mafuta mengi, chumvi na sukari nyingi na kupunguza kula vyakula vyenye wanga ambavyo husababisha uzito kuongezeka.


Ufanyaji mazoezi unashauriwa ufanyike kila siku kwa muda usiopungua nusu saa ili mishipa ya damu iweze kufanyakazi yake vizuri na viungo vya mwili viweze kujiendesha vizuri.

Watu wajiepushe kupenda kukaa sehemu moja muda mrefu na badala yake watembee ili kunyoosha viungo viweze kufanyakazi vizuri.

Pia inashauriwa muda wa jioni watu wale vyakula laini badala ya vizito na chakula kiliwe mapema muda wa saa 12 jioni hadi saa moja usiku ili kiweze kusagika vizuri tumboni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com






Na Golden Kisapile TUDARCo

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera waliojitosa kuokoa maisha Bukoba

**HONGERA** Watanzania kwa kuthubutu kuwaokoa wenzetu katika mazingira hatarishi bila kujali kama kuna kuumia hata kufa.

Wakati yanapotokea majanga hasa ajali, moto kulipuka, majengo na miundombinu kubomoka hata mafuriko, inaweza kuwa vigumu kujitosa kusaidia waathirika. Lakini, ukweli unabaki kuwa kuwasaidia walio katika hatari ndiyo njia ya kuokoa maisha na kupunguza madhara yanayoweza kuwafika binadamu.

Wataalamu wa majanga na kukabiliana na kiwewe, shoki na mfadhaiko (trauma) wanasema msaada wa haraka ndiyo wa muhimu kuliko chochote na unatakiwa kupatikana ndani ya dakika 60 au saa moja baada ya ajali.

Nikumbushe kuwa mnamo Novemba 6, mwaka huu ilitokea ajali ya ndege katika Ziwa Victoria na kusababisha abiria wa ndege 19 kupoteza maisha na wengine 24 wakiokolewa na wavuvi wasamaria wema akiwamo Jackson Majaliwa, aliyefanyakazi ya ziada kuwasaidia.

Ni pongezi kwa kila mmoja aliyekuwapo wakati ajali inatokea na kutoa msaada huo bila kujali kuwa ilikuwa ni ndani ya maji. Zipo ajali za moto, za barabarani, mafuriko na hata kuangukiwa na majengo ambazo zilitokea na baadhi kusababisha maafa kwenye jamii.

Lakini wapo Watanzania waliopambana kuwaokoa na kuwasaidia wengine kwenye ajali mbalimbali bila kujali hatima zao. Ni wazi kuwa kuwanusuru na kuwaokoa waathirika kunapunguza vifo vya wazee, wagonjwa, watoto, vijana na kunusuru nguvu kazi inayohitajika mno katika jamii tunayoishi.

Kunusuru watu kunapunguza idadi ya walemavu na wategemezi katika jamii wakiwamo ombaomba ambao wanakosa walezi au wahitaji.

Tukumbuke kuwa kuwa waathirika wa ajali kuanzia za barabarani na nyinginezo wasiposaidiwa na kuokolewa kwa haraka pamoja kupoteza maisha wengine hupoteza viungo kama vile mikono, miguu na kuwa walemavu wa kudumu na hupelekea kuwa tegemezi kwa ndugu, jamaa na marafiki.

> **Kwa hiyo kuwaokoa wengine wakati wa ajali ni jambo jema na la muhimu ili waweze kufanya shughuli zao za kila siku husu-san zile za kiuchumi, maen-deleo ya jamii na taifa.**

Ni kuwa endapo msaada utatokea wahusika kama kwenye ajali za moto, au za barabarani watanusurika na idadi ya walemavu katika jamii wanaotokana na ajali inapungua pia. Ajali ni mwiba inakwamisha watu kufikia malengo yao ya kimaisha kwa ujumla, mfano kama baba au mama akipata ajali atakaye athirika ni watoto na wategemezi wao.

Inaweza kukwamisha masomo ina maana atakatisha masomo, ataacha shule, ataondoka bweni au mengine mengi yanayokwamisha. Ni wazi kuwa kama aliyeumia au kupoteza viungo kwenye ajali anafanya biashara atasitisha kufanya ndoto yake na hatimaye kupelekea kutofikia malengo fulani, kwa hiyo endapo angeokolewa inakuwa na tija pamoja na hao wanaowategemea.

Ni wazi kuwa mfululizo wa ajali una athari kichumi ambao unashuka, kama mtu amepatwa na ajali na asipookolewa kwa wakati kama atanusurika itapelekea awe mlemavu na kushindwa kufanya shughuli zake za kila siku kama vile uzalishaji yote hayo huweka uchumi pabaya.

Matokeo yake ni kukosa pato lake la kila siku na hushindwa kuchangia tozo na kodi katika mfuko wa serikali, hatimaye uchumi wa taifa huweza kushuka kutokana na ajali za mara kwa mara.

Kwa hiyo kuwaokoa wengine wakati wa ajali ni jambo jema na la muhimu ili waweze kufanya shughuli zao za kila siku hususan zile za kiuchumi, maendeleo ya jamii na taifa.

Kuokoa ni suala jingine, lakini zipo zinazozuilika, ningetoa rai watu wote kuwa wakati mwingine ni kujitahidi kujaribu kila linalowezekana kuzuia ajali zisitokee.

Kama taifa si kila mmoja anaweza kukimbilia kuokoa kuna kamati zinazohusika na maafa ni vyema serikali izioongezee nguvu ya kuokoa watu wakati ajali zinapotokea.

Isifike wakati watu wakaumia lakini wakakosa msaada na kuumia hata kupoteza maisha. Uwezesha uangalie miundombinu, nguvu kazi na maslahi kwa wahusika.

# Biteko aagiza tathmini maeneo yenye makaa mawe

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WAZIRI wa Madini, Dk. Dotto Biteko, ametoa miezi mitatu kwa Tume ya Madini kutafuta maeneo yenye makaa ya mawe yanayokaliwa na watu bila kuendelezwa ili wapewe walio tayari kuendeleza nchi ipate mapato na kukuza ajira.

Akifungua mkutano wa wadau wa makaa ya mawe wa mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe na Ruvuma mjini hapa, alisema ni muhimu baada ya tathmini hiyo kama watakuwa wameshindwa kuendeleza wapewe wanaoweza.

Alisema pamoja na mambo mengine mkutano huo utajadili changamoto za uchimbaji na biashara ya malighafi hiyo.

Dk. Biteko alisema hivi karibuni malighafi hiyo itahitajika duniani kwa kuwa ni chanzo kikubwa cha nishati hasa wakati huu wa vita vya Urusi na Ukraine, kuwezesha nchi kupata fedha nyingine.

Alitaja viwango vya makaa hayo na thamani yake kwenye mabano kwa kila mkoa kuwa ni Ruvuma tani 1.5, yenye thamani ya Sh. bilioni 485.5, Songwe tani 16,328,000 (Sh. bilioni 1.12) na Njombe tani 2762 (Sh. milioni 238).

Aidha, alisema kwa mwaka huu mkoa huo umezalisha makaa ya mawe yenye uzito wa tani 764,816.5 yenye thamani ya Sh. bilioni 287.6, Songwe 4587.9 yenye thamani ya Sh. milioni 331.4, Njombe tani za makaa ya mawe 41,000 yenye thamani ya Sh. milioni 47.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, alisema kumekuwa na changamoto za maabara ambazo zinapima makaa ya mawe zikichelewesha na kutoa majibu tofauti ya madini hayo kwa kuwa zipo mbali na maeneo ya uchimbaji.

Naye, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati, Dastan Kipangula, alipongeza ubunifu wa wizara kushuka chini na kufanya mikutano ya kutatua changamoto za wachimbaji wa sekta ndogo ya makaa ya mawe kwa kuwa itasaidia kuleta ufanisi.




Meneja wa Biashara wa Benki ya NMB Kanda ya Zanzibar, Naima Shaame (kushoto), akizungumza katika warsha maalum ya benki hiyo na makandarasi, jijini Zanzibar jana. Wengine ni Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed (wa pili kulia), Waziri wa Ardhi, Rahma Kassim Ali (kulia) na Mkuu wa Idara ya Miamala wa benki hiyo, Linda Teggisa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto ataka mjadala kitaifa bima ya afya

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDURU

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ametaka kuitishwa kwa mjadala wa kitaifa na wananchi washirikishwe kujadili mfumo bora wa kugharamia afya za Watanzania.

Alisema changamoto ya afya hususan gharama za matibabu zimekuwa zikiwasumbua wananchi wengi kutokana na hali mbaya ya uchumi na kwamba ni jambo la msingi wakawa sehemu ya kuamua mfumo bora watakaouridhia badala ya kufanyiwa uamuzi usiowashirikisha.

Alitoa kauli hiyo jana katika Kijiji cha Ligunga, wilayani hapa, akiwa katika ziara ya ujenzi wa chama hicho inayohusisha mikoa mitatu ya kusini ambayo ni Lindi, Mtwara na mkoa wa kichama wa Selous.

"Tunaendelea kutoa rai ya kuitishwa mkutano wa kitaifa wa kujadili mfumo bora wa kugharamia afya za Watanzania. Wananchi washiriki kikamilifu kwenye kuamua juu ya afya zao," alisema.

Alisema hali za uchumi wa wananchi wengi ni mbaya, wengi ni maskini na wengine hawana kipato cha uhakika kinachoweza kuwahakikishia wanapokuwa na magonjwa kumudu gharama hizo.

Alisema kwa sasa wananchi wengi wanatumia Mfumo wa Afya ya Jamii (CHF), ambao alisema haukidhi matarajio ya wananchi kwa kuwa hawapati matibabu pindi wanapoyahitaji, huku ikiwa na changamoto ya ukomo wa matumizi yake kupitia mfumo wa rufaa.

"Serikali ilitumia nafasi hiyo ya matatizo ya Watanzania kupata huduma bora za afya, kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote, waliyoipeleka bungeni, sisi tuliipinga kwa sababu ulikuwa hauendi kuondoa matatizo ya msingi kwenye upatikanaji wa huduma bora ya afya kwa usawa na kwa uhakika wa leo na kesho," alisema.

Alisema muswada huo ungeenda kuwatumbukiza zaidi kwenye lindi la umaskini Watanzania kwa kuwa ulikuwa na mapendekezo ya gharama za juu kwa kaya moja kugharamia Sh. 340,000, kila mwaka.

Zitto, alifafanua katika uchambuzi wa ACT, waliieleza serikali tatizo la afya ya Watanzania halitokani na kukosa matibabu pekee bali ni mazingira hatarishi ya kazi, watu kukosa vipato vya kueleweka, masikini kuendelea kuwa maskini zaidi, wazee kutopatiwa mahitaji yao ya msingi, umaskini wa chakula na kipato.

**ATAKA HATUA KUKABILI TEMBO**


Akizungumzia kadhia ya tembo kuvamia makazi ya wananchi, aliitaka serikali, kuchukua hatua za kukabiliana na matukio ya tembo kuvamia vijiji hali inayotishia usalama wa watu na uhakika wa chakula nchini.

**RUWASA**

Kuhusu kero ya maji Tunduru, alisema kwa sasa kuna hali ya kusuasua kwa mradi huo hasa katika Kijiji cha cha Namwinyu ambao unahudumia vijiji viwili vya Namwinyu na Namakungwa ambao vina jumla ya vitongoji 25 na kueleza hali hiyo imechangiwa na Mamlaka ya Maji Ruvuma (RUWASA) kufanya kazi kwa kusuasua.

Alisema ni wakati sasa Waziri wa Maji, Juma Aweso kuongeza nguvu ya kufuatilia kwa umakini na kushughulika na waliozembea utekelezaji wa majukumu yao na kuwafanya wananchi wataabike.

## KABWELA



# Waziri akemea waajiri kuficha barua uhamisho wa watumishi

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amekemea tabia ya baadhi ya waajiri katika taasisi za umma kuficha barua za uhamisho wa watumishi wa umma.

Amesema anashangazwa na tabia hiyo wanayofanyiwa watumishi ambao Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ameridhia na kutoa kibali cha uhamisho ili wakautumikie umma katika maeneo mengine ambayo mamlaka imeona kuna uhitaji.

Akizungumza jana na watumishi wa Halmashauri ya Manispaa Kigoma Ujiji na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Ndejembi alisema waajiri na maofisa utumishi wanapaswa kutenda haki kwa watumishi wa umma ambao wanastahili kuhama baada ya kupatiwa kibali cha uhamisho na mwenye mamlaka ambaye ni Katibu Mkuu-Utumishi badala ya kufichiwa barua zao.

"Waajiri na maofisa utumishi tendeni haki kwa watumishi wa umma ambao wanastahili kuhama baada ya uhamisho wao kuridhiwa na mamlaka. Tusifiche barua zao kwani kitendo hicho kinakwenda kinyume cha mamlaka na ni kinyume cha sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utumishi wa umma," alisisitiza.

Ndejembi aliongeza kuwa wako watumishi wa umma ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu katika kituo kimoja cha kazi, hivyo mamlaka kupitia Katibu Mkuu- Utumishi ikaamua kumpeleka mtumishi huyo katika eneo lingine la kazi ili abadili mazingira ya kazi ambayo yatamwongezea ufanisi kiutendaji. Pamoja na uamuzi huo, alisema baadhi ya waajiri hukwamisha uhamisho huo wakati mamlaka iliridhia baada ya kufanya uchambuzi yakinifu.

Aidha, Ndejembi aliwataka waajiri katika taasisi za umma kutopitisha barua za kuomba uhamisho za watumishi ambao ni wa ajira mpya kwa kuwa ajira zao hazina muda mrefu na baadhi yao wanakuwa hawajathibitishwa kazini, hivyo kutotimiza kigezo cha kutumikia miaka mitatu tangu waajiriwe.

Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Ester Mahawe, alimshukuru Ndejembi kwa kuhimiza uwajibikaji, kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kiutumishi ikiwa ni pamoja na kutatua kero na changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili watumishi walio katika wilaya yake.

Mahawe aliwahimiza watumishi wa umma walio katika eneo lake la utawala, kufanya kazi kwa bidii na weledi kama alivyoelekeza Ndejembi ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono kwa vitendo Kaulimbiu ya Kazi Iendelee ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Naye mtumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, ambaye ni Ofisa Utumishi, Stanford Bidebuye, alimshukuru Ndejembi kwa kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kiutumishi, ikiwa ni pamoja na kutatua kero na changamoto zilizokuwa zikiwakabili watumishi wa Halmashauri hiyo kwa muda mrefu.

Bidebuye alisema kupitia elimu ya masuala ya kiutumishi waliyoipata kutoka kwa Naibu Waziri, anaamini mkoa wa Kigoma utafunguka katika kila sekta na kupata maendeleo chini ya uongozi makini wa Rais Samia.

Naibu Waziri Ndejembi ameanza ziara ya kikazi mkoani Kigoma yenye lengo kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma na kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kuzinusuru Kaya Maskini nchini unaoratibiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).




Mwendesha guta akisafirisha tangi kubwa la kuhifadhia maji, huku likiwa limemziba asiweze kuona nyuma eneo la Mabibo Mwisho, Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## TADB yaahidi kusaidia mikopo wenye ulemavu

**Na Frank Monyo**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imewaambia Kituo cha Wakulima Wafugaji Viziwi Tanzania (KIWAWAVITA) kuwa itaendelea kuwasaidia wakulima walio katika makundi maalum nchini.

Pia benki hiyo imezitaka taasisi zingine za fedha kulisaidia kundi hilo ambalo mara nyingi huachwa nyuma.

Hayo yamesemwa jana na Ofisa Mwandamizi wa Maendeleo ya Biashara wa TADB, Grayson Ferdinand, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya siku tatu kwa kituo cha KIWAWAVITA.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na TADB yamefanyika mkoani Morogoro na yana lengo la kuwajengea uwezo kwa nadharia na vitendo kundi hilo kuinuka kiuchumi na kuongeza uzalishaji katika shughuli zao za kilimo.

Grayson alisema TADB imeona umuhimu wa Watanzania walio katika makundi maalum ambao ni wakulima, kujengewa uelewa wa kujua jinsi ya kupata mikopo ya kilimo pamoja na kufanya kilimo chenye tija.

Akifungua mafunzo hayo, Ofisa Tawala Ofisi ya Wilaya ya Morogoro, Hilary Sagara, aliitaka jamii kutambua na kuthamini kundi maalumu la viziwi katika kuwashirikisha katika uchumi jumuishi ili kuwasaidia kuondokana na utegemezi kwa kuwa wana nguvu na uwezo wa kufanya kazi kama watu wengine wanapowekewa mazingira rafiki.

Kwa mujibu wa Sagara, kundi hilo limekuwa likipitia changamoto ya kutosikia na jamii imekuwa ikiwasahau katika kuwashirikisha, hivyo TADB imeonyesha mfano kwa kampuni na taasisi mbalimbali kuiga kuwasaidia.

"Serikali imejipanga vizuri, hivyo kila halmashauri nchini imepewa asilimia mbili ya fedha kwa ajili ya kukopesha makundi maalumu wakiwamo wenye ulemavu wak utosikia (viziwi) bila riba yoyote, hivyo wajiunge katika makundi ili wapatiwe fedha hizo," alisema Sagara.

# Afungwa jela miaka 6 kumuua mke kwa koleo

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu mkazi wa Lwamgasa, Paschael Kanani (55) kutumikia kifungo cha miaka sita jela baada ya kupatikana na kosa la kumuua mke wake.

Mshtakiwa huyo amehukumiwa kifungo hicho baada ya kumuua Helena Thomas kwa kumpiga koleo kichwani na kufariki dunia. Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji wa Mahakama hiyo, Kassim Robert, baada ya mshtakiwa kukiri kosa lake la kumuua mke wake bila kukusudia.

Jaji Robert alisema kwa kuwa mshtakiwa amekiri kosa lake mwenyewe pasipo kulazimisha na amekiri kwa hiari yake, basi Wakili wa Serikali, Winfrida Ernest, amsomee mshtakiwa maelezo ya awali.

Akimsomea mshtakiwa maelezo ya awali, Ernest alidai kuwa Novemba 23, 2021 Hellena alimpelekea mshtakiwa chakula akiwa kwenye kazi yake ya ulinzi wa mitumbwi katika Ziwa Victoria, wilayani Chato na baada ya kumpa mume wake chakula, alikaa pembeni.

Ernest alidai kuwa baada ya mshtakiwa kupewa chakula, alimuuliza mke wake ambaye kwa sasa ni marehemu kuwa mbona hakuna maji ya kunawa na maji ya kunywa na mke wake hakujibu neno lolote bali aliondoka na kurudi nyumbani kwake eneo la Lwamgasa, wilayani Geita.

Aliendelea kudai kuwa mshtakiwa baada ya kumaliza kazi yake ya ulinzi, alirudi nyumbani na kukuta mke wake hayupo na yeye akaondoka na ilipofika majira ya usiku, mshtakiwa alirudi nyumbani na kukuta tena mke wake hayupo na baada ya muda mfupi mke wake alirudi hapo nyumbani.

Baada ya hapo, alidai kuwa mshtakiwa alimuuliza mke wake ulikuwa wapi na hakujibu chochote, ndipo wakaanza kuzozana na mshtakiwa kuchukua koleo na kumpiga nayo kichwani na kufariki dunia papo hapo.

Wakili alidai kuwa baada ya watoto wawili wa marehemu kuona mama yao ameanguka chini walikimbia hadi kwa mjumbe kutoa taarifa na waliporudi wakiwa na mjumbe, walikuta mama yao mzazi ameshafariki dunia.

Alidai kuwa mshtakiwa alikamatwa na kupelekwa kituo cha polisi Geita huku mwili wa marehemu ukipelekwa kwenye chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Geita na uchunguzi wa daktari ulibaini kuwa chanzo cha kifo cha Helena lilikuwa jeraha kubwa kichwani ambalo lilisababisha damu kuvilia ndani na kufanya damu kuchanganyikana na ubongo.

Baada ya Wakili wa Ernest kumaliza kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali, Jaji Robert alisema: "Mshtakiwa umekiri kosa lako la kumuua mke wako bila kukusudia, hivyo mahakama hii inakutia hatiani kwa kosa uliloshtakiwa nalo."

Kabla ya hukumu kutolewa, Jaji Robert alimtaka mshtakiwa huyo ajitetee ili mahakama impunguzie adhabu. Wakili wa Kujitegemea Ernest Makene, aliyekuwa akimtetea mshtakiwa, aliiomba mteja wake apewe adhabu ndogo kwa sababu ana umri mkubwa wa miaka 55 pia ana watoto watano wanaomtegemea.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili Ernest uliomba mahakama impe mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na kwa wanaume wengine wenye tabia za kuwaua wake zao.

Jaji Robert alitupilia mbali utetezi huo na kusema: "Mshtakiwa kitendo hiki ulichokifanya cha kumuua mke wako ni cha kikatili sana kwa sababu umejichukulia sheria mikononi bila kutoa taarifa kwenye vyombo husika ukaamua kuua bila kukusudia. Sasa utakwenda gerezani kutumikia kifungo cha miaka sita jela ili iwe fundisho kwako na kwa watu wengine wenye tabia za kikatili kama zako.

HABARI KITAIFA

# Uagizaji mafuta pamoja waleta tija kwa taifa

Na Mwandishi Wetu

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imesema uagizaji pamoja wa mafuta unaosimamiwa na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) una tija kwa taifa kutokana na kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa hiyo muhimu hasa disel na petroli.

Wajumbe wa kamati hiyo walisema hayo juzi baada ya kukagua miundombinu ya kushusha na kupima mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam na hifadhi kubwa ya mafuta ya kampuni ya TIPER ambayo serikali ni mbia kwa umiliki wa asilimia 50.

**Lengo la ziara lilikuwa kuona uwezo wa miundombinu hiyo katika kushusha na kuhifadhi mafuta.**

Ziara hiyo iliongozwa na Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato na Naibu Katibu Mkuu, Kheri Mahimbali, ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema kuwa lengo la ziara lilikuwa kuona uwezo wa miundombinu hiyo katika kushusha na kuhifadhi mafuta.

Hasunga alisema baada ya ukaguzi huo, kamati imejihakikishia kwamba miundombinu iliyoko ya ushushaji na uhifadhi mafuta ina uwezo wa kukidhi mahitaji ya nchi, hivyo kamati imefurahishwa na uwepo wa miundombinu hiyo.

Kamati hiyo ilitoa wito kwa TIPER kujenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta katika maeneo mengine ya nchi ili kuongeza uwezo wa kampuni na nchi katika kuhifadhi mafuta na kuleta urahisi katika usafirishaji wa mafuta ndani na nje ya nchi.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PBPA, Erasto Mulokozi, alieleza kamati hiyo kuwa tangu kuanzishwa kwa wakala huo, mwaka 2015, kumekuwa na mafanikio mbalimbali ikiwamo uhakika wa upatikanaji wa mafuta yanayotosheleza mahitaji na yenye viwango vya ubora unaohitajika.

Manufaa mengine, kwa mujibu wa Mulokozi, ni serikali kupanga ukusanyaji wa mapato kwa kuzingatia takwimu sahihi, kupanga bei elekezi ya mafuta na kupata unafuu wa gharama za uagizaji wa mafuta nchini kutokana na uagizaji wa pamoja kwa wastani wa zaidi ya Dola za Marekani milioni 200, sawa na Sh. bilioni 462 kuokolewa kwa mwaka.

Pia alisema kutokana na mfumo huo kuleta ufanisi, nchi za jirani pia zinatumia mfumo huo kuagiza mafuta kupitia Tanzania, hivyo kuipatia serikali mapato kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya bandari.

Aliongeza kuwa mfumo huo umesaidia kupunguza upotevu wa mafuta wakati wa kupakua kutoka melini ambapo wastani wa tani 1,100 (lita 1,300,000) huokolewa kila mwezi sawa na Sh. bilioni 4.3.




Maandamano ya kuadhimisha Siku ya Ugonjwa wa Kisukari Duniani yaliyofanyika kitaifa wilayani Misungwi, mkoani Mwanza juzi na kushirikisha wadau mbalimbali wanaopambania magonjwa yasiyoambukiza wakiwamo Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TNCDA) na Chama cha Kisukari Tanzania (TDA). PICHA: MPIGAPICHA WETU

## Shule iliyojengwa kwa ufadhili TEA kuanza mwaka 2023

Na Mwandishi Wetu

SHULE ya Msingi Msangalale ya mchepuo wa Kiingereza inayojengwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) inatarajia kuanza rasmi Januari, 2023.

Akitoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Bodi ya TEA, Prof. Maurice Mbago, aliyetembelea mradi huo unaojengwa katika Kata ya Makulu jijini Dodoma, Mkuu wa Divisheni ya Elimu Awali na Elimu Msingi wa Jiji la Dodoma, Prisca Myalla, alisema shule itaanza na wanafunzi 320.

Baada ya kuanza, Myalla alisema shule hiyo itaendelea kuongeza wanafunzi hadi watakapofikia 640 idadi ambayo ni uwezo wake halisi.

Myalla aliongeza kuwa mradi huo utasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule zenye upungufu wa vyumba vya madarasa na kusogeza karibu na jamii huduma ya elimu.

Sambamba na hayo, ofisa huyo alisema shule hiyo itasaidia na kupandisha ufaulu wa kitaaluma katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Msanifu Majengo na Msimamizi wa Mradi huo, Emmanuel Mateo, alisema kwa sasa ujenzi huo unaohusisha jengo la utawala, vyumba vinane vya madarasa na matundu 32 ya vyoo umefikia asilimia 80 na kwamba umepangwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Mfuko wa Elimu wa Taifa umetoa ufadhili wa Sh. milioni 750 kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo itakayotoa elimu kwa lugha ya Kiingereza katika mwaka wa fedha wa 2021/ 2022 kwa lengo la kusaidia jitihada za serikali za kutoa elimu bora.

## Magonjwa yasiyoambukiza mzigo kwa serikali

Na Romana Mallya

SERIKALI imesema Watanzania wanahitaji elimu zaidi ili kuepuka magonjwa yasiyoambukiza ukiwamo ugonjwa wa kisukari ambao umekuwa ukiongezeka nchini.

Takwimu zinaonyesha miaka ya 1990 kulikuwa na asilimia moja tu ya ugonjwa wa kisukari nchini lakini kwa sasa imeongezeka hadi kufikia asilimia tisa.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Misungwi, Petro Sabato, aliyasema hayo juzi katika maadhimisho ya Siku ya Kisukari Duniani ambayo kitaifa ilifanyika wilayani humo mkoani Mwanza.

"Elimu inahitajika zaidi ili kuwakinga wananchi na magonjwa yasiyoambukiza hasa ugonjwa wa kisukari kwa kuwa umekuwa ukigharimu maisha ya watu ikiwamo baadhi yao kukatwa viungo," alisema.

Kutokana na hali hiyo, kiongozi huyo alitoa rai kwa wananchi kufanya juhudi katika kukabiliana na maradhi yao, wafanye mazoezi mara kwa mara na kupima afya angalau mara moja kwa mwaka ili wale watakaobainika waanze matibabu mapema.

Kaimu Meneja Mpango wa Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza, Valeria Milinga, alisema vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukiza huchangiwa kwa asilimia 33 na kisukari kwa asilimia 9.10.

"Katika kuongeza uhamasishaji na uelewa kwa wananchi kuhusu magonjwa haya hasa kisukari, tumefanya maonyesho ya wiki ya magonjwa yasiyoambukiza yaliyoanza tarehe Novemba 5, mwaka huu hadi 12," alisema.

Milinga alisema kupitia maonyesho hayo jumla ya wananchi 3,000 walijitokeza kupima kisukari na waliogundulika kuwa nao ni 34.

Pia alisema mbali ya kupima, walitoa huduma ya dawa, mafunzo kwa watoa huduma za afya katika vituo 300 kwenye mikoa tisa.

Mwenyekiti wa Chama cha Kisukari Tanzania, Prof. Andrew Swai, alisema miaka ya 1990 kulikuwa na asilimia moja tu ya ugonjwa wa kisukari nchini lakini kwa sasa imeongezeka hadi kufikia asilimia tisa.

"Kutokana na ongezeko la ugonjwa wa kisukari nchini, imekuwa tatizo ambapo inagharimu asilimia 20 ya bajeti ya serikali kwa kuwahudumia wagonjwa hao," alisema.

Maadhimisho hayo yaliandaliwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau wa Chama cha Kisukari Tanzania (TDA), Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TNCDA) na viongozi wa Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya.

# Chalamila ataja mikakati kuipaisha Kagera kiuchumi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, ametaka vipaumbele vyenye tija vinavyoweza kupandisha uchumi na kunufaisha wananchi wa mkoa ili kufikia kiwango cha juu cha maendeleo ya kiuchumi.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa juzi, Chalamila alisema mkoa huo umebarikiwa kuwa na rasilimali ambazo kama wananchi wake wakitumia vizuri zitaleta tija.

Chalamila alisema mkoa una watu takribani milioni 2.9 wanaojishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali, huku kahawa ikitegemewa kuwa zao la kibiashara.

**Shughuli kubwa ya wananchi wa mkoa huu ni kilimo hasa kilimo cha kahawa, ndizi na mazao mengine.**

"Shughuli kubwa ya wananchi wa mkoa huu ni kilimo hasa kilimo cha kahawa, ndizi na mazao mengine. Mazao haya yakiboreshwa kwa namna mbalimbali, wananchi watapata tija," alisema Chalamila.

Pia alisema kwa zao la kahawa, shughuli iliyopo ni kuhamasisha zaidi wawekezaji ili kupandisha thamani na kujipatia masoko ya ndani na nje.

Aliongeza kuwa zao la ndizi ambalo mkulima wa kawaida anapata faida kidogo litaanza kufanyika kitaalamu, ili kumwondoa kwenye hali ya chini kwa kumpatia masoko yenye tija na faida kubwa.

"Ndizi zitaanza kulimwa kitaalamu kumwondoa mkulima wa kawaida wa zao hilo na kuzifikisha katika nchi kubwa zenye uhitaji wa zao hilo ikiwa ni pamoja na kusafirisha Ulaya, Jamaica na Brazil," alibainisha Chalamila.

Aidha, alisema katika sekta za mifugo na uvuvi, watapitia upya ranchi na kuweka ufugaji mkubwa wenye tija na uwekezaji wa kweli ili kuboresha upatikanaji wa nyama kwa wingi pamoja na mazingira ikiwa ziko nchi nyingi zenye uhitaji mkubwa wa nyama.




Meneja wa Bidhaa za Intaneti wa Tigo, Imelda Edward (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Biashara Samsung Tanzania, Mgope Kiwanga wakionyesha simu janja ya Samsung A04, baada ya kuizindua Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## 'Ufugaji nyuki ni mbadala wa mkaa'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MHIFADHI masuala ya nyuki Wilaya ya Kibaha, Fatuma Masoud, amesema kuna njia mbadala ya biashara ya mkaa kwa wananchi kufanya ufugaji wa nyuki ambao unakwenda sambamba na utunzaji wa mazingira.

Masoud alisema hayo jana alipokuwa akizungumza ofisini kwake huku akisema ufugaji bora wa nyuki ambao ulirasimishwa mwaka 2005 ni njia bora ya kutunza mazingira na kuingiza kipato.

Mhifadhi huyo alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi, wananchi sasa wanatakiwa kubadilika kutoka kwenye kutegemea biashara ya mkaa na kuanza kufuga nyuki itakayowasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira.

"Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Kibaha tunatoa elimu ya ufugaji nyuki popote na pia tunasaidia upatikanaji wa mizinga. Tunategemea kila mmoja kupitia ufugaji nyuki, atatunza mazingira na tutapunguza hali ya ukame kwenye nchi yetu," alisema.

Masoud alisema kuna vikundi takribani vitano katika wilaya ambavyo vinajishughulisha na ufugaji wa nyuki na wananchi wanaendelea kuelimishwa namna ya kuwa na ufugaji nyuki ili waondokane na imani ya kuwa mkaa pekee ndio unaweza kuwaingizia kipato kikubwa na kuendesha maisha yao.

Pia aliwashauri wanawake kujitokeza kufanya shughuli ya ufugaji nyuki eneo ambalo watanufaika na elimu lakini kupitia njia hiyo itawasaidia kuwahamasisha wanawake kuachana na biashara ya mkaa ambayo inasababisha athari za mazingira.

Masoud pia aliwasisitiza wananchi kutumia gesi badala ya mkaa ili kupunguza uharibifu wa mazingira na ukataji miti unaofanyika katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kibaha ukiwamo msitu wa Hifadhi Ruvu Kusini.

**Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Kibaha tunatoa elimu ya ufugaji nyuki popote na pia tunasaidia upatikanaji wa mizinga.**

# Sigini awataka Polisi kutunza vitendea kazi

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sigini, amelitaka Jeshi la Polisi nchini kutunza vitendea kazi yakiwamo magari ili kusaidia katika kutunza usalama na kutenga bajeti ya kuyafanyia matengenezo kila baada ya kutembea kilomita 1,000.

Aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa hafla ya kupokea magari 150 kutoka Kampuni ya Ashok Leyland yenye makao makuu nchini India, ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa mkataba wa masharti nafuu wenye thamani ya dola milioni 29.7 ambao uliingiwa mwaka 2013 kati ya Tanzania na India.

Sigini alisema kumekuwa na malalamiko ya upungufu wa vitendea kazi kutoka maeneo mbalimbali katika Jeshi la Polisi na kwamba mkataba huo utakapokamilika, watakuwa na magari 881 na kwamba kwa sasa tayari wameshapokea zaidi ya magari 600.

"Mahitaji ya vitendea kazi ni makubwa kwa nchini, hivyo kukamilika kwa mkataba huu kutasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza upungufu wa vitendea kazi hasa magari kwenye vituo vyetu vya polisi katika mikoa na wilaya," alisema.

"Baada ya kupokea magari haya Jeshi la Polisi litaingia kwenye utaratibu wa kufundisha madereva. Tusingependa wakosee tangu wanapoanza lakini tutayaingiza kwenye mgawo ili kujua yatapelekwa maeneo gani. Pia magari haya yatumike kwa utunzaji ili yaendelee kusaidia katika utekelezaji wa majukumu ya jeshi letu," alisisitiza.

Sigini alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha na kuweka msukumo zaidi ili magari hayo kupatikana pamoja na kuwezesha vyombo vyao kutimiza majukumu yake vizuri.

Naye Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Srikanta Pradhan, alisema ushirikiano kati ya nchi hizo mbili umezidi kuimarika kwa kuwa wamekuwa wakishirikiana kuleta maendeleo katika nyanja mbalimbali zikiwamo usafirishaji, elimu na afya.

"Kumekuwa na wanafunzi pamoja polisi ambao wameenda India kwa ajili ya kuongeza elimu na maarifa yatakayowasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao. Yote yanayofanyika ni kuhakikisha ushirikiano wetu unazidi kuimarika kwa manufaa ya pande zote," alisema Pradhan.

HABARI KASKAZINI

# Mgogoro viongozi wakwamisha hatimiliki

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

**Kwa zaidi ya miaka 15 sasa, tunamiliki eneo la ardhi ambalo tulipewa kihalali na viongozi wa serikali ya kijiji waliotangulia.**

MGOGORO unaotokana na viongozi kutuhumiana kujinufaisha kisiasa, unadaiwa kukwamisha mchakato wa kutafuta hati ya umiliki wa ardhi inayotumiwa na Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Nuru Maendeleo SACCOS, ambacho kinahudumia wakulima wa vijiji vitatu vya Kata ya Kahe, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Akizungumzia jana madhara yatokanayo na mgogoro huo, Mwenyekiti wa Nuru ya Maendeleo SACCOS, Madina Mshana, alisema maslahi ya kisiasa kutangulizwa mbele, badala ya kuhudumia wananchi kumechangia kuathiri shughuli za kiuchumi za wanachama wake zaidi ya 1,000 waliosajiliwa.

Alisema kwa muda mrefu wamefuatilia upatikanaji wa hati hiyo na kuelekezwa walipie Sh.100,000 lakini Mwenyekiti wa Kijiji hicho, amekataa kutia saini hati hiyo, jambo ambalo limewalazimu kuomba serikali kuingilia kati ili kupata ufumbuzi wake.

"Kwa zaidi ya miaka 15 sasa, tunamiliki eneo la ardhi ambalo tulipewa kihalali na viongozi wa serikali ya kijiji waliotangulia. Kwa miaka kadhaa, tumekuwa tukihangaika kuomba uongozi mpya uliopo madarakani kutia saini hati ya kumiliki ardhi ya kijiji, bila mafanikio.

"Eneo hilo tayari limeendelezwa, lakini kwa sababu ya maslahi binafsi ya kisiasa, uongozi wa sasa hautaki kutambua kilichofanywa huko nyuma na serikali zilizopita. Hawajui kwamba wanachofanya ili kujinufaisha binafsi, wanaumiza wananchi walio wengi. Tunaomba serikali pamoja na Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro, waingilie kati ili jambo hili lifike mwisho na wananchi waendelee kujikwamua kiuchumi kupitia rasilimali yao.

Kutokana na mgogoro huo kuathiri chama hicho, Mkazi wa Kijiji cha Mawala, David Laizer, alielekeza kilio chao kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, akiomba kuingilia kati mgogoro huo ili kuwezesha wananchi kupata hati, baada ya kufuata taratibu zote za kisheria.

Alipoulizwa kuhusu tuhuma hizo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Oria Kahe, Raymond Mrisha, alisema siyo kweli kwamba anakwamisha suala hilo, isipokuwa watu wanajenga taharuki na kutaka kuonekana wanafanya kazi tofauti na wengine.

Diwani wa Kahe, Aloyce Momburi, akizungumzia mgogoro huo, alikiri kuwa eneo hilo ni mali halali ya chama hicho na kwamba hajajua sababu za Mwenyekiti wa Kijiji cha Oria Kahe, kushindwa kuridhia wanachama hao kupata hati miliki ya eneo hilo.

"Eneo hilo miaka ya nyuma, lilitengwa kwa ajili ya maendeleo ya kijiji na kuna taasisi nyingine za serikali zipo katika eneo hilo kama vile Polisi, Ofisi za Kijiji na Shule, lakini tatizo kubwa limekuwa kwa Nuru ya Maendeleo SACCOS ambayo ni miongoni mwa taasisi zilizopo katika eneo hilo.

"Hata hivyo, tayari tumeshaunda kamati maalum itakayokwenda wilayani na mkoani kushughulikia tatizo hili pamoja na kukutana na mwenyekiti huyo ili kujua tatizo linalokwamisha chama chetu kupata hati na hatimaye kumaliza mgogoro huu," alisema.

## Barabara kufungua fursa za kiuchumi

**Na Oscar Assenga,** MUHEZA

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Geofrey Kasekenya, amesema ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Muheza/Amani katika Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, utafungua fursa nyingi za kiuchumi kwa kuongeza kipato cha wakazi wa wilaya hiyo, ambao ni wazalishaji wakubwa wa mboga, viungo na matunda nchini.

Aidha, alisema kufunguka kwa barabara hiyo, kutaifanya Muheza ikae kwenye ramani ya wazalishaji wakubwa wa sekta ya kilimo, ambao mazao yao yatakuwa yamepitia mchakato wote wa mnyororo wa thamani wa mazao ya chakula na biashara.

Naibu Waziri Kasekenya aliyasema hayo jana alipofanya ziara ya kushtukiza ya kukagua mradi huo wa ujenzi wa barabara ya Muheza hadi Amani, yenye urefu wa zaidi ya kilomita 40.

"Pamoja na umuhimu wa barabara hii kiuchumi. Utekelezaji wake huu ni ahadi ya viongozi wa kitaifa na kimsingi kufika kwake hadi katika kiwango hiki ni kutokana na msukumo wa Mbunge wenu, Hamisi Mwijuma (Mwana FA).

Alisema nia ya serikali ni kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, kwa kutumia fedha zilizotengwa kutokana na bajeti ya ndani, kunalenga kufungua fursa za kiuchumi, kwa kuyafikia masoko makubwa ya kilimo ndani ya mkoa na nje ya Tanzania.

Kwa sasa, alisema Mkoa wa Tanga, una jumla ya kilomita 327 za barabara kuu na 171 za barabara za vijijini zilizojengwa kwa kiwango cha lami, hivyo kujengwa kwa barabara hiyo ni ukombozi mkubwa kwa wananchi hasa wanaoishi Tarafa ya Amani, ambayo jiografia yake ni ya milima.

Barabara hiyo ambayo ilikuwa haipitiki kwa urahisi, tayari serikali ilishajenga kwa zege mwaka 2011, maeneo yenye kona kali na hatarishi ili kupunguza adha ya magari kukwama na kusaidia wananchi wa tarafa hiyo ambao ni wakulima wa viungo vya chai, chakula na wauzaji wakubwa wa vipepeo nje kufika sokoni.



Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mwalimu Nazama Tarimo, akizungumza kwenye mkutano mkuu wa chama hicho katika Mji Mdogo wa Mirerani juzi, ulioendesha harambee ya kuchangisha fedha za ujenzi wa jengo la CWT, Sh. milioni 26 zilipatikana. **PICHA: GIFT THADEY**

## Wachangishana ujenzi zahanati kukwepa gharama

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

GHARAMA kubwa za kukodi usafiri wa pikipiki ili kufuata huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Siha au Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto, imewasukuma wananchi wa Kijiji cha Moyo Njamu, kuanza kufunga mkanda na kuchangishana kila kaya Sh. 2,000 ili kujenga zahanati yao.

Wakazi hao wakiwamo wajawazito, wanalazimika kila siku kutumia kati ya Sh. 3,000 hadi 5,000 kukodi usafiri wa bodaboda kutoka kijijini hapo hadi Kibong'oto au kwenda Sanya Juu iliko hospitali ya wilaya, ambako hupata huduma za tiba na uchunguzi wa magonjwa mbalimbali.

Akizungumza jana wakati akiwasilisha azimio hilo kwa wananchi wake, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Julius Massawe, alisema nia ya kujenga zahanati hiyo ni kuwapunguzia wananchi mzigo wa gharama za kufuata huduma za afya nje ya kijiji hicho.

"Tangu tumezaliwa tumekuwa tukishuhudia wazazi wetu jinsi wanavyopata shida wakati wakitafuta huduma ya afya, tumeshuhudia vifo vya watoto wachanga pamoja na kinamama wanaotaka kujifungua kutokana na kutokuwa na huduma ya afya karibu, tukaamua kuwa ni lazima tufanye jambo," alisema Massawe.

Sera ya Afya ya Mwaka 2007, inaelekeza pamoja na mambo mengine mpango mahususi wa taifa kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi, ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi.

Diwani wa Livishi (CCM), Lucas Nkini, alisema wananchi wa eneo hilo kwa zaidi ya miaka 10 sasa, wamekuwa na shauku ya kuwa na zahanati katika kijiji hicho, kwa kuwa wanaona wao wako kama wanaishi kisiwani.

"Ndiyo maana sasa wameanza michango, japokuwa hali ya kiuchumi sio nzuri. Lakini kutokana na uhitaji wa kusogeza huduma ya afya karibu, kila kaya imepangiwa kuchangia ujenzi huo kwa shilingi 20,000. Makisio yetu yanaonyesha kwamba gharama za ujenzi wake unaweza kuwa zaidi ya shilingi milioni 150 hadi kukamilika kwake.

"Hamasa imekuwa kubwa na kwa siku ya leo, nimepiga simu mimi mwenyewe kwa baadhi ya wananchi wachache na nimepata mifuko 51 ya saruji. Tunategemea wiki hii, tunaanza ujenzi wa msingi, tunawaomba wazaliwa wa kijiji hiki wanaoishi nje ya mkoa, kuwaunga mkono wananchi wenzao ili waweze kutimiza dhamira yao," alisema.

Akitoa ufafanuzi kuhusu usogezaji wa huduma za afya, Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Siha, Dk. Peter Mahuu, alisema kwa muongozo wa serikali kwa kila kijiji hivi sasa ni kuwa na zahanati yake na ngazi ya kata kuwa na kituo cha afya.

Baada ya wasilisho hilo, Neema Mmari, Mkazi wa Mowo Njamu, alieleza kufurahishwa kwao na namna jambo hilo lilivyopatiwa ufumbuzi, kwa kuwa ni kero iliyokuwa ikiwatesa wananchi tangu Tanzania ilipopata Uhuru wake mwaka 1961.

# Ugumu maisha Kwasuva wakwamisha ujenzi vyoo

**Na Mary Mosha,** ROMBO

UGUMU wa maisha unaotokana na umaskini uliokithiri kwa wakazi wa Kitongoji cha Kwasuva, Rombo mkoani Kilimanjaro, unadaiwa kusababisha wananchi wake wasitamani kujenga vyoo bora, wala kutumia maji tiririka kunawa mikono na sabuni.

Inaelezwa kuwa licha ya serikali kupiga kelele na kutoa elimu, bado wananchi hao hawafikirii kwamba hali hiyo inaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa ya kipindupindu na kuhara ambayo yanatishia mustakabali wa ustawi wa afya zao.

Kwa mujibu wa Ofisa Afya wa Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mcharo, kutokana na hali hiyo tayari ofisi yake kwa kushirikiana na wataalamu wa afya ngazi ya wilaya na kata, wameanza kuwaelimisha wananchi kupitia mikutano na mikusanyiko mbalimbali ili kuona umuhimu wa kuwa na vyoo bora na kutumia maji tiririka wanapotoka chooni.

"Ni kweli jambo hilo nalifahamu na tunalishughulikia ingawa kwa mkoa wa Kilimanjaro, asilimia 99.9 ya kaya zina vyoo na kati ya asilimia 90 ndio wenye vyoo bora.

"Sasa hili la kukosekana maji, tumewaelimisha wananchi waanze kuweka maji kwa vigeleni vidogo au vinyunyizi mrashi vinavyotoa maji kwenye matundu yaliyotobolewa kuruhusu maji kupita taratibu watu wanaponawa mikono," alisema.

Maudhui yanayotokana na taarifa za kitafiti za Wizara ya Afya, yanaonyesha kuwa Watanzania wengi hutumia vyoo visivyokuwa bora na hawaoshi mikono kwa majisafi na sabuni. Pia inaelezwa zaidi ya nusu yao hutumia vyoo vilivyo chini ya kiwango na moja ya kumi, sawa na asilimia 6.5 hawatumii vyoo kabisa.

Alipotafutwa kuzungumzia tatizo hilo, Diwani wa Kisale Msaranga, Mathias Assey, alisema: "Idadi kubwa ya wananchi wa eneo hilo hawana vyoo bora, kwa sababu ya kukosa fedha za ujenzi wa vyoo.

"Pia suala la ugumu wa maisha kutokana na umaskini wa wakazi wa eneo hili, ndio kiini halisi cha kuwafanya wasitamani kuwa na vyoo. Tayari nimeanza kuyaita na kufanya mashauriano na mashirika yasiyo ya kiserikali yatusaidie kuandika andiko la miradi kwa ajili ya kuwasaidia wananchi hao wawe na vyoo."

Mmoja wa wakazi wa Kwasuva, Frida Martin, alieleza Nipashe kuwa wanalazimika kujenga vyoo vya kiwango duni shambani na wengine kujisaidia porini au shambani kwa sababu wao ni masikini na wana hali ngumu kwa sasa kutokana na kukosa mazao kwa misimu minne mfululizo, ambayo huuza na kuwapatia kipato.

"Mimi nimejenga choo hiki cha makuti ili niweze kujisitiri mimi na familia yangu. Ni kweli vyoo havina ubora, ila tunamshukuru Mungu tuna uwezo wa kujistiri. Hatujawahi kupewa elimu yoyote juu ya ujengaji wa vyoo bora, kwa hiyo hatujui chochote," alisema.

**Mimi nimejenga choo hiki cha makuti ili niweze kujisitiri mimi na familia yangu. Ni kweli vyoo havina ubora, ila tunamshukuru Mungu tuna uwezo wa kujistiri.**




Meneja Masoko na Mawasiliano wa Kampuni ya GF Trucks & Equipment's Ltd, Smart Deius (wa pili kushoto), akikabidhi sehemu ya msaada wa vyakula na vifaa kwa Ofisa Mfawidhi Daraja la Kwanza na Kiongozi wa Geti la Mweka, Denis Simion, kwa ajili ya askari wanaoendelea na kazi ya uzimaji moto katika Mlima Kilimanjaro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Shule kongwe iko hatarini kuanguka

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SHULE ya Msingi Matemboni iliyoko Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, ambayo ilijengwa baada ya Uhuru, iko hatarini kuanguka kutokana na miundombinu yake kuwa chakavu.

Kutokana na tishio hilo, uongozi wa shule hiyo umelazimika kusitisha matumizi ya vyumba vinne vya madarasa, ikihofia yanaweza kusababisha maafa kwa wanafunzi wanaoyatumia, kwa ajili ya kusomea na kujifunzia masomo mbalimbali.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule hiyo, Joyce Mushi, alisema wamefikia uamuzi huo wa kusitisha matumizi ya madarasa hayo, kwa kuwa yamepasuka nyufa kubwa na yameegama.

"Ni hatari na kwa kweli kwa sasa wanafunzi zaidi ya 300, wanasoma na kujifunzia katika mazingira hatarishi. Tatizo ni kubwa na siyo madarasa peke yake, pia hatuna vyoo kwa sababu ni chakavu. Hali kama hii imekuwa ikisababisha walimu na wanafunzi kuishi kwa hofu shuleni hapa.

Akizungumzia tatizo hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kikarara, Auniel Efremu, alisema ili kukabiliana na hali hiyo, hatua walizochukua ni kuomba serikali kupitia Halmashauri ya Moshi, kutafuta fedha za dharura ili kuikarabati shule hiyo, kwa kuwa mazingira yake kwa sasa ni hatarishi kwa walimu na wanafunzi.

"Ibara ya 8 (1) b ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inaelekeza kuwa wananchi wote ushiriki shughuli za maendeleo ya serikali yao. Kwa mantiki hiyo, kwa kuwa hivi sasa tumebaki na tatizo hili la kukosekana choo cha walimu.

# RC atangazia kiama wahujumu maendeleo

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, amesema hatabaki salama mtu yeyote ambaye atajitokeza kumkwamisha katika utekelezaji wa majukumu yake akiwa Msaidizi wa Rais Samia Suluhu Hassan, hasa linapokuwa suala lenye maslahi mapana ya umma wa Watanzania.

Amejiapiza kusimamia kile anachokiamini, wakati alipokwenda kukagua mradi wa ujenzi wa barabara ya Afrika Mashariki, iliyoanza kujengwa kuanzia Wilaya ya Pangani kupitia Handeni na kwenda hadi Dar es Salaam, ikiwa na urefu wa kilomita 93.5.

Akizungumza jana baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, mkuu huyo wa mkoa, alisema kwa kuwa serikali imewekeza zaidi ya Sh. bilioni 95 kujenga barabara hiyo, hivyo hatavumilia kumwona mtu yeyote anajaribu kukwamisha mradi huo au mkandarasi kusuasua kwa sababu za kisiasa.

Ujenzi wa barabara hiyo mpaka sasa umefikia asilimia 10.5 na unatarajia kukamilika ifikapo mwaka 2025.

"Nitoe onyo na angalizo kwa Watanzania wenzangu wote wanaotanguliza maslahi yao mbele kuliko wenzao, wewe unayeweza kupiga pesa kwenye mradi huu au mingine inayotekelezwa na serikali katika mkoa huu nilioko mimi Mgumba, hutakuwa salama. Lile suala ambalo lilitokea hapa Pangani na kule Kibirashi, wakati ule la kukwamisha mradi huu, iwe mwanzo na mwisho," alionya.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi huo, Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Tanga, Eliazary Rwekiza, alisema katika ujenzi wa barabara hiyo kulijitokeza mgogoro baada ya mwananchi mmoja kuzuia eneo la kuchimba kokoto akidai ni eneo lake na ana kibali cha uchimbaji, akitaka alipwe fidia ya Sh. bilioni 1.7 ndipo aruhusu uchimbaji huo wa malighafi ya ujenzi.

"Tatizo lililopo hivi sasa ni kwenye hili jiwe tulilopo. Baada ya kupimwa uimara wake, tumegundua kwamba kuna mtu mwingine ana kibali cha uchimbaji wake. Kwa hiyo mkandarasi huyu tuliye naye hawezi kulichukua mpaka wafikie mwafaka na huyo mtu mwingine," alisema.

Mbunge wa Handeni Vijijini (CCM), John Sallu, akizungumza katika eneo hilo, aliziomba mamlaka husika kuingilia kati suala hilo, kwa kuwa linachelewesha mradi ambao unakwenda kuleta mabadiliko makubwa kwa wakazi wa Handeni.

"Jamani zabuni imetangazwa mwezi wa nne na mwezi wa tano, kuna mtu aliona fursa na alikwenda kuchukua kibali cha kuzuia hili jiwe la kuvunja kokoto kwa ajili ya kuwekewa lami, sasa imesababisha mkandarasi anachelewa kuanza kazi.

"Watu wa madini, wachukue hatua stahiki ili huu ujenzi ukamilike na juhudi za Rais wetu Samia Suluhu Hassan, zisirudi nyuma," alisema.

Ukurasa 19



**EDIMUND SENGONDO MVUNGI 1952- 2013**
**Jina kubwa linalodumu linaloendelea kuishi mioyoni mwa tasnia, sekta nyingi**

Ukurasa 16



DRC yatupa karata ya mwisho kwa mzozo wa Kivu Kaskazini

Ukurasa 15



**KUMPINGA RAIS MITANDAONI**
**Vyama vyasisitiza uteuzi anaofanya Rais Mwinyi usisababishe taharuki**

siasa
JUMATANO NOVEMBA 16, 2022
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

CHADEMA MGOMO RUZUKU

# Wadai bado hawatambui uchaguzi 2020,Msajili vyama asita kuwagusa

•Yasema viti maalumu haviongezi ruzuku



Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika. **PICHA: MAKTABA**

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya kuwepo madai kuwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kinapata ruzuku kutokana na viti maalum, ambao hata hivyo , wanazozaniwa, Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, amesema viti maalumu havina mchango kwenye kuongeza ruzuku ya vyama.

Mnyika anasema hayo, katika mazungumzo yake na gazeti ufafanuzi wa madai hayo na kuongeza kuwa CHADEMA haipokei ruzuku hiyo na haijafikiria kwa sababu haiutambui uchaguzi mkuu wa 2020.

Anasema CHADEMA, inaendelea na msimamo wake wa kutokutambua uchaguzi mkuu wa ba ulikuwa batili.

Katibu Mkuu wa chama hicho, anasema msimamo huo ndiyo umekifanya chama kisipokee ruzuku ya Shilingi milioni 109 ambazo kinatakiwa kupata kutokana na kura walizopata wagombea ubunge wa majimbo mbalimbali.

Hata hivyo, kwa upande wa ushindi matokeo ya uchaguzi huo yaliwapa mbunge mmoja Aida Khenani kutoka Nkasi Kaskazini.

Katibu Mkuu huyo anasema kiasi cha fedha za ruzuku ambacho chama hicho kinatakiwa kupokea ni Sh. milioni 109, kinachotokana na idadi ya kura za wabunge kuanzia asilimia tano na kuendelea, ambazo CHADEMA ilipata.

"Lakini kuna mbinu chafu ambazo zimekuwa zikienezwa kwamba fedha hizo ni za viti maalum 19, sio kweli, viti hivyo havichangii lolote katika ruzuku ya chama chochote cha siasa," anasema Mnyika.

Mwanasiasa huyo anadai mbinu hizo zinafanyika kwa ajili ya kutaka kuuminisha umma wa Watanzania kuwa viti hivyo ndivyo vinavyoleta ruzuku kwenye chama cha siasa, na kwamba hakuna ukweli wowote.

"Chama chetu kilitakiwa kupokea kiasi hicho, lakini hatujawahi kupokea, ila wapo baadhi ya watu wanapotosha kuwa fedha hizo zinatokana na viti maalum 19 vya wabunge ambao si wanachama wetu," anasema.

Anasema siyo wabunge wa viti maalumu na kwamba kama wangeutambua uchaguzi huo, wangekuwa wanapokea kiasi hicho cha ruzuku kila mwezi. Lakini msimamo wa chama chao ni kwamba hawaukubali.

WANASTAHILI

INAENDELEA UK. 20

# Anwani za makazi zilivyo fursa kutambua na kuenzi wanasiasa




Moja ya vibao vya utambulisho wa barabara na anuani za makazi vilivyosambaa karibu Tanzania nzima. **PICHA: BLOG**

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

MITAA na barabara vijijini na mijini pengine vyote vimepewa majina mapya kuanzia ya watu, vitu,wanyama hata mengine kutoka mataifa ya kigeni.

Ni kazi ya kukamilisha program ya anuani za makazi na misimbo ya posti kodi, inayotoa uwanja wa kutumia majina ya kila aina kuanzia watu binafsi, viongozi , viongozi mashuhuri, makabila, miti, bidhaa hata madini kama tanzanite, dhahabu na ya viumbe hai kutambulisha makazi.

Kuupa mtaa wako jina au majina unayoyapenda ni jambo jema lakini ni pia kutumia majina ya viongozi waliowekeza muda na maisha yao kulitumikia taifa na Watanzania tangu uhuru hata sasa, wakiwamo waliofariki na wanaoishi.

Jina kama Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango, Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa, mawaziri wakuu wastaafu Mizengo Pinda, Edward Lowassa, Frederick Sumaye, Cleopa Msuya, John Malecela , Salim Ahmed Salim, Joseph Warioba na Rashid Kawawa, yanastahili kupewa nafasi kwenye zoezi hili la anuani za makazi.

Kadhalika Visiwani, majina ya viongozi Sheikh Abeid Aman Karume, Thabiti Kombo, Hussein Ali, Mwinyi, Dk. Salim Amour, aidha, Makamu wa Rais

Dk. Omari Ali Juma nao wana nafasi majina yao kutumiwa kutambulisha mitaa na barabara.

Viongozi wa Zanzibar, akiwamo Aboud Jumbe, Idrisa Abdul Wakil, Salmin Amour, Amani Abeid Karume na Ali Mohammed Shein, Mawaziri Kiongozi Maalim Seif Sharif Hamad, Vuai Nahodha , Zena Ahmed, wasisahaulike pia

**PAKUWATUMIA**

Majina ya viongozi hawa yanapendeza kutumiwa kwenye barabara au mitaa ya kuingia kwenye ofisi za makao makuu ya wilaya na mikoa au bomani, hospitali hata taasisi za umma kama vyuo na magereza.

Watu hawa hawana budi kutumika kutambulisha mitaa zama hizi za miradi ya kuyapa majina, anuani na postikodi makazi ya Watanzania.

Kuna maana gani barabara kuelekea makao makuu ya mkoa mfano Kilimanjaro kuitwa Mtaa wa Bomani ? Ni dhahiri itapendeza kuanzia sasa ikipewa jina jipya la Barabara ya Cleopa David Msuya.

Ni habari njema iwapo barabara na mitaa inayokwenda na kutambulisha ofisi za makao makuu ya wilaya, halmashauri, ofisi za mikoa na majiji itatumia majina kama haya Barabara ya Frederick Sumaye ofisi ya DC Ileje.

Barabara ya John Samuel Malecela, Ofisi ya Halmashuri ya Wilaya ya Kilwa, Barabara ya Mizengo Pinda Ofisi ya Manispaa ya Kinondoni.

Mtaa wa Edward Lowassa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mtaa wa Kassimu Majaliwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mwanga Kigoma.

Barabara ya Dk.Salim Ahmed Salim Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Barabara ya Joseph Sinde Warioba, Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Mvomero.

Katika kuweka majina ya mitaa na barabara mwaka huu majina ya viongozi hawa yangestahili kutumiwa si mkoa au wilaya moja bali kwa Tanzania nzima ikiwa ni njia mojawapo ya kuwaenzi na kuwafanya viongozi wa taifa hili, waendelee kuishi na kutajwa na umma walioutumikia.

Mathalani, jijini Dar es Salaam tutasikia majina ya Barabara ya Goba , Mbezi, Kawe, Mbagala, Kizuiani , Segerea na Tandale utambulisho kama huo na mengineyo unafahamika ndiyo majina ya sehemu zenyewe hayahitajiki tena kutajwa.

Utambulisho wake ni mkubwa hata kwenye ruti za daladala yanafahamika, kinachohitajika badala ya kuendeleza utamaduni huo ni kuanza sasa kuwaenzi viongozi kwa kutumia majina yao kwenye maeneo hayo.

YA WANYAMA?

Ukiangalia majina ya mitaa na barabara kwenye sehemu nyingine ni ya wanyama, twiga, tembo, nyati na swala. Inapendeza kutumia majina ya viongozi kama Barabara ya Makamu Dk. Phillip Mpango, Othman Masoud Othman, Dk Mohamed Gharib Bilal, Dk. Omar Ali Juma na Dk. Ali Mohamed Shein.

Baada ya majina ya makamu kutumika ipasavyo wapo viongozi wa Zanzibar, mfano Barabara ya Abdul Jumbe, Mtaa wa Idrisa Abdulwakil, Mtaa wa Salmin Amour .

Yatumike pia majina ya Mawaziri Kiongozi mfano Mtaa wa Shamsi Vuai Nahodha, Barabara ya Seif Shariff Hamad na Mtaa wa Zena Ahmed Said

**WANAWAKE MASHUJAA**

Wapo wanawake mashujaa wapigania uhuru na watetezi wa haki za Watanzania na Wazanzibari kama Bibi Titi Mohamed na Biubwa Amour Zahor wa Zanzibar aliyeshiriki kufanikisha mapinduzi mwaka 1964.

Wengine ni mama Karume mke wa Rais wa kwanza wa Zanzibar Mama Fatuma Karume, Mama Maria Nyerere, majina yao nayo yana nafasi katika anuani za makazi .

Unahitajika utambulisho wa viongozi wakuu wanaofanya mambo makubwa mfano Dk. Asha-Rose Migiro mwanamke wa kwanza kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa duniani, kadhalika vyama vya siasa kama Labour, CHADEMA, CCM, ACT Wazalendo, CUF navyo vitumie majina ya viongozi.

Wakati mwingine si lazima kwenye mitaa na bababara zinazokwenda nyumbani kwao au kwenye ofisi za chama, yatumike popote pale ili kuendeleza kazi zao za kukuza demokrasia.

**MAJAJI WAKUU**

Wakati mwingine kuna haja ya kuachana na majina yasiyogusa wengi na kutumia yale yenye utambulisho na heshima kutokana na majukumu ya kikazi baadhi ya watu waliyoyatimiza.

Mathalani, Mtaa wa Bwawani, si jina lenye kukumbusha kazi au dhamana ni vyema anuani za makazi zikawaangalia hata majaji wakuu badala ya kutumia majina kama mtaa wa kisiwani au ziwani.Barabara zipewe majina ya majaji kama Jaji Othuman Chande, Mtaa wa Jaji Ibrahimu Juma, Barabara Jaji Augustino Ramadhan , Jaji Francis Nyalali, halikadhalika nao siyo maeneo wanayoishi bali popote Tanzania.

**TAASISI ZA UMMA**

Ni nani ambaye hatafurahi kusoma utambulisho kama Chuo Kikuu cha Samia Suluhu Hassan Dodoma. Ni Rais wa kwanza mwanamama na ambaye kazi ya kuiendeleza Tanzania anaifanya kwa bidii zote.

Lakini majina kama DIT yanaweza kubadilishwa na kuitwa Dk. Salim Ahmed Salim Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, kadhalika Chuo Kikuu cha Usafirishaji cha Salmin Amour, Taasisi ya Uhasibu ya Rashid Mfaume Kawawa Dar es Salaam wakati chuo cha IFM kikapewa jina la Chuo cha Usimamizi wa Fedha cha Aboud Jumbe.

Kutoka majina kama Hopitali ya Taifa Muhimbili yanaweza pia kubadilishwa yakasomeka Hospitali ya Taifa ya Ali Hassan Mwinyi Muhimbili, wakati Uwanja wa Kilimanjaro ukapata jina jipya ukiitwa Benjamin William Mkapa International Airport Kilimanjaro.

Majina kama Chuo Kikuu cha Ustawi wa Jamii, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ualimu Chang'ombe DUCE, Chuo Kikuu cha IDM Mzumbe yote yanaweza kubadilishwa na kupewa utambulisho wa viongozi wakuu waliotumia nguvu, akili, muda na maisha yao kulitumikia taifa.

Tanzania kuna barabara kama za viongozi wa nchi nyingine kama Nnamdi Azikiwe, husomwa Nandi Azikiwe wa Nigeria, Kwame Nkurummah wa Ghana, Indira Gandhi wa India, Samora Machel wa Msumbiji, Albert Luthuli wa Afrika Kusini , inakuwaje kuwasahau watoto wa nyumbani kama mawaziri wakuu kama Malecela, Msuya, Lowassa na Pinda?

Si hao tu hata na makamu Dk. Gharib Bilal na Omari Ali Juma? Vipi viongozi wa Zanzibar walioshirikiana na Bara kujenga taifa imara lenye amani la Tanzania, wanasahaulika? Programu ya anuani za makazi na posti kodi iwape nafasi na kuwaenzi.

KUMPINGA RAIS MITANDAONI

# Vyama vyasisitiza uteuzi anaofanya Rais Mwinyi usisababishe taharuki

• Wahusika washauriwa kufuata utaratibu waonywa si vinginevyo

**Mwandishi Maalum, ZANZIBAR**

NI ukweli usiopingika kuwa, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Hussein Ali Mwinyi, anatekeleza kwa vitendo Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) pamoja na matakwa na mapendekezo ya vyama vya upinzani.

Ni katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, hivi karibuni Rais Mwinyi alifanya uteuzi kwa ngazi ya Makatibu Wakuu na Wakurugenzi Wakuu kitendo kilichoibua sintofahamu iliyosababisha taharuki kwa wananchi kuhusu teuzi hizo.

Hata hivyo, chama kimoja cha upinzani kupitia taarifa yake iliyotolewa kwa umma kupitia mitandano ya kijamii kimeonyesha kutoridhika na kupinga uteuzi wa Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Thabit Idarous Faina.

Kwa Mujibu wa Katiba ya Zanzibar Ibara ya 52, Rais ni kiongozi mkuu wa nchi ambaye katika utendaji wake wa kazi anaweza kushauriwa, lakini haamrishwi na hata anapopewa ushauri halazimiki kufuata ushauri huo.

Kitendo cha chama hicho kujitokeza kupinga au kukosoa uteuzi wa Rais kimeelezwa kuwa kinaweza kusababisha taharuki na sintofahamu kwa wananchi.

Wanasiasa na wadau mbalimbali wa demokrasia nchini wametoa maoni yao na kueleza umuhimu wa vyama kuzingatia taratibu kisheria badala ya kupinga wazi wazi uteuzi unaofanywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.







Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, Makamu wa Pili wa Rais , Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Othman Masoud Othman. **PICHA: IKULU ZANZIBAR.**

**DEMOKRASIA MAKINI**

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia Makini, Ameir Hassan Ameir, anasema hakuna chama chenye mamlaka ya kupinga uteuzi unaofanywa na Rais kwa mujibu wa sheria na kanuni za vyama vya siasa pamoja na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Anakumbusha kuwa chama chochote cha siasa kinapaswa kupeleka mapendekezo yake katika kamati iliyoundwa na Rais kushughulikia masuala ya kisiasa katika visiwa vya Zanzibar na haipaswi kujitokeza na kupinga wazi wazi uteuzi unaofanywa na Rais.

"Kwa mujibu wa kanuni na sheria za nchi, Rais ndiye kiongozi mkuu wa nchi, hivyo ukiwa na jambo lolote katika kumshauri unapaswa kufuata kanuni na taratibu kinyume chake ni kumvunjia heshima na kukiuka taratibu za nchi," alieleza.

"Tabia zetu ni kuheshimu viongozi na watu wazima na kama unamshauri ni kupia taratibu za kiheshima sio kutoa amri mitandaoni. Inasikitisha sana kuona chama ambacho kina kiongozi mkubwa katika serikali kinatoa taarifa kwenye mitandao kwa kutoa maagizo kwa kiongozi mkuu wa nchi badala ya kumtumia yeye kwa kupeleka ushauri au maoni kwa utaratibu unaokubalika," anafafanua.

Ameir anampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Mwinyi kwa jitihada mbalimbali anazofanya kuleta maendeleo ya Wazanzibari bila kuangalia itikadi za vyama.

"Mimi nachukua fursa hii kumpongeza Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ili kuhakikisha Wazanzibari wanapata maendeleo, wito wangu kwake aendelee kutekeleza dhamira yake njema kwa wananchi wote bila kuhofu." anaeleza.

> "Mimi nachukua fursa hii kumpongeza Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ili kuhakikisha Wazanzibari wanapata maendeleo, wito wangu kwake aendelee kutekeleza dhamira yake njema kwa wananchi wote bila kuhofu." anaeleza.

**CHAMA UPDP**

Katibu Mkuu wa Chama cha UPDP, Hamad Mohammed Ibrahim, anapozungumzia suala hilo anasema, hatua yoyote ya chama chochote cha siasa kusambaza taarifa kwenye mitandao ya kijamii badala ya kutafuta ushauri au kupeleka maoni kwa Rais kwa kitendo chochote ambacho kinaona hakiko sawa ni kuleta mtafaruku katika nchi na kuchafua jina la Mkurugenzi wa Uchaguzi.

Ibrahimu anasema itakuwa busara kama chama hicho kitajitokeza hadharani kuomba radhi kwa kitendo cha kwenda kinyume na maadili na kujaribu kusababisha taharuki kwa wananchi ambao wanapokea majukumu ya Rais ukiwamo uteuzi wa viongozi anaoufanya.

"Sisi vyama vya siasa tunapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha tunaunganisha jamii na sio kuleta mtafuruku kwa jamii, wanapashwa kujitokeza hadharani kuomba radhi kinyume na hivyo chama hicho kitaonyesha kwa jamii namna kilivyokosa mwelekeo wa kuwa chama cha kisiasa," anasema Katibu Mkuu wa Chama cha UPDP.

Ibrahimu anakumbusha kuwa chama chochote cha kisiasa hakipaswi kuwazungumzia Wazanzibari wote kwa sababu wana uhuru wa kutoa maoni yao badala ya kusemewa, kuhusu uteuzi wa Thabit Idarous Faina.

"Mnasema Wazanzibari hawamtaki Faina, ni wangapi? Mmewauliza saa ngapi, lini hata ingekuwa mnazungumzia hao wanachama wenu tu je? Mmewauliza saa ngapi, au imekaa timu ya watu wachache wanaandaa uchochezi katika chama chenu na kulivaa koti la Wazanzibari, kitendo hicho ni ishara ya uchochezi," anaeleza.

# Uchaguzi Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, mwenyekiti wa sasa atabiri mchuano mkali

## • Aufananisha na vita ya Daudi Vs Goliati



Mmoja wa makada wa CCM waliopitishwa kuwania uenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi, Bakari Nampenya.

**Na Sabato Kasika**

UCHAGUZI wa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM Taifa, unatarajia kufanyika Novemba 25 mwaka huu, kwa kuwapambanisha makada nane waliopendekezwa kuwania nafasi hiyo.

Makada wanaotarajiwa kuchuana ni mwenyekiti wa sasa Dk. Edmond Mndolwa, Bakari Nampenya, Fadhil Maganya, Said Mohamed, Mwanamwanga Mwaduga, Ally Othman, Ali Masudi na Hassan Zahara.

Hao wamependekezwa na chama kutoka katika makada 122 waliokuwa wamejitokeza kuomba nafasi hiyo, na sasa watachukuana ili kupata mmoja atayeongoza jumuiya hiyo kwa kipindi kingine cha miaka minne.

Ikiwa imebakia wiki moja na siku chache kabla ya uchaguzi huo, mwenyekiti wa sasa wa jumuiya hiyo, Dk. Mndolwa anatabiri kuwapo kwa mchuano mkali kutoka kwa makada hao nane.

Anasema vita ni vita na kwamba kila kada ana mbinu zake ambazo amejipanga kuzitumia kwa ajili ya kushinda nafasi hiyo, na kuongeza kuwa hajabweteka kutetea wadhifa huo wa kuongoza wazazi anaoushikilia.

"Ukweli ni kwamba vita ni vita tu ndio maana ilitokea hata Daud alilishinda jitu kubwa Goliati, hivyo nami siwezi kuwaona wapinzani wangu kama wa kawaida bali vita ni vita,"anasema Dk. Mndolwa.

Anaongeza kuwa pamoja na vita hiyo, mwisho wake ni kupata mwenyekiti wa jumuiya ya wazazi taifa atakayechaguliwa miongoni mwa wagombea hao nane ambao anasema wanasubiri uchaguzi huo kwa hamu kubwa.

USHINDI WA 2017

Desemba mwaka 2017, Dk. Mndolwa aliibuka kidedea kwa kuchaguliwa kuwa mwenyekiti mpya wa jumuiya hiyo katika uchaguzi ulioelezwa kuwa wenye ushindani mkubwa uliofanyika jijini Dodoma.

Mwenyekiti Mndolwa alishinda nafasi hiyo iliyokuwa ikiwaniwa na baadhi ya makada akiwamo aliyekuwa mwenyekiti wa wakati huo Alhaji Abdallah Bulembo, ambaye alijiondoa dakika za mwisho kabla ya uchaguzi.

Wengine waliokuwa wamejitosa katika kinyang'anyiro hicho ni John Machemba, Said Bwanamdogo (marehemu), Salim Chikago, Jasson Rweikiza, Alfred Mwambeleko na Alphonce Siwale.

Dk. Mndolwa anasema wakati huo hakukuwa na makada wengi waliojitokeza kama mwaka huu, na kwamba hali hiyo inaashiria kuwa kutakuwa na mchuano mkali wa kumpata mwenyekiti ajaye.

"Lakini ninaamini kwamba kila aliyependekezwa atakuwa amejipanga kivyake kwa ajili ya kuwania nafasi, ili mradi sisi sote tuheshimu na kuzingatia taratibu zote za uchaguzi ndani ya chama," anasema

**SABABU ZA WINGI**

Mmoja wa waliopendekezwa kuwania nafasi Bakari Nampenya, anasema hatua hiyo ni kuendelea kupanuka kwa demokrasia ndani ya chama hicho ambayo imewafanya kujitokeza kwa wingi kuomba kuwania nafasi hiyo.



Mwenyekiti wa sasa wa Jumuiya ya Wazazi, Dk. Edmund Mndolwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

"Ndani ya CCM kuna demokrasia pana ambayo kila mwanachama anaruhusiwa kuwania nafasi ya uongozi, ili mradi awe na sifa ikiwamo kuwa mwanachama hai na nyingine nyingi," anasema Nampenya.

Mbali na hilo anasema fomu zilikuwa zimetolewa bure tofauti na miaka ya nyuma ambapo kila aliyetaka kuwania nafasi hiyo, alitakiwa kuilipia Sh. 10,000, kwa ajili ya kuchangia chama na jumuiya zake.

Nampenya wanachama wote waliojitokeza kuomba nafasi hiyo inawezekana wote walikuwa na sifa, lakini bahti mbaya nafasi yenyewe ni moja na kwamba vikao vya chama vikaona ni busara kupendekeza hao nane.

"Katika hao nane nami nimebatika kuwamo, lakini si kwamba sisi ni bora sana kuliko wanachama wengine, bali wote tuko sawa ila tumependekezwa ili hatimaye apatikane mmoja atakayekuwa mwenyekiti wetu wa taifa," anasema.

Mgombea huyo ambaye ni mjumbe wa zamani wa Baraza Kuu la Jumuiya ya Wazazi Taifa na kuachia nafasi hiyo baada ya uchaguzi wa mwaka 2017, anasema atakayeshinda katika uchaguzi huo, utakuwa ni ushindi wa jumuiya.

Nampenya ambaye kwa sasa ni Mjumbe wa Bodi Mamlaka ya Hifadhi ya Ngongoro, anasema wanachama wa CCM wameiva kisiasa na kwamba ndio maana hakuna aliyelalamika baada ya kupendekezwa majina manne.

"Lakini pia wapo wenzetu ambao hawakuingia kwenye kinyang'a nyiro, waliamua kujiondoa na kujikuta tukibaki wagombe wasiozidi 70 ambao ndani yake tumependekezwa nane," anasema.

**WENYEVITI WATANGULIZI**

Katika ya mwishoni mwa miaka 90, jumuiya hiyo ya wazazi taifa, imeongezwa na makada mbalimbali, akiwamo Abiud Maregesi ambaye baadaye aliondolewa kwenye nafasi hiyo wakati wa serikali ya wamu ya nne.

Baada ya kuiondolewa, nafasi hiyo ilishikiliwa na mwenyekiti mwingine Athman Mhina, ambaye kwa sasa ni marehemu, ndipo ikachukuliwa na Bulembo aliyejitoa katika kinyang'nyiro katika uchaguzi wa mwaka 2017.

Katika uchaguzi wa mwaka huo ndio ambao ulimwezesha Dk. Mndolwa kuingia madarakani hadi sasa ambapo umeitishwa uchaguzi mwingine utakaofanyika Novemba 25 mwaka huu.

Hata hivyo, hajigambi kushinda, bali asisitiza kuwa uchaguzi huo ni sawa na vita na kwamba ni muhimu ajiandae vizuri, kwa ajili ya kuhakikisha anatetea nafasi hiyo anayoishikilia hadi sasa.

"Kama nilivyoeleza awali, ushindani utakuwa ni mkali kwani ninaamini kila mgombe atakuwa amejipanga kuhakikisha anaibuka na ushindi kwenye uchaguzi huo tunaousubiri kwa hamu," anasema.

Dokta Mndolwa ana uzoefu wa zaidi ya miaka 40 katika tasnia ya ukaguzi wa hesabu akiwa na ujuzi kwenye maeneo ya kodi, utawala bora, benki, fedha na uandaaji sera.

# Yaelekea inawezekana kusomesha wanafunzi vyuo vikuu bila mikopo

Na Michael Eneza

KUNA uwezekano wa kusomesha vijana vyuo vikuu iwe ni sehemu ya majukumu ya kitaifa yanayolipiwa na serikali, badala ya kutoa mikopo kwa maana kuwa mwanafunzi anajisomesha mwenyewe, na serikali inamkopesha arudishe baadaye.

Mfumo huu wa kupeleka vijana vyuo vikuu unakaribia miaka 30 tangu ulipobuniwa na mikakati kuanza kuutekeleza mwaka 1993, licha ya kuwa 'nyufa' za kusomesha vijana vyuo vikuu kama jukumu la kitaifa zilianza kujitokeza kabla ya mwaka 1990 bado kazi inaendelea.

Ni katika mwaka 1991 ambako walimu vyuo vikuu, wakichoshwa na migomo ya wanafunzi kulalamikia kucheleweshwa donge la kujikimu almaarufu 'boom' vyuoni, wakaona ni vyema kuondoa kupewa fedha ya kujikimu, na serikali ikahamia kuwakopesha.

Kimsingi serikali ilifuata mawazo yaliyokuwa yakitolewa kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitivo cha Fani na Sayansi za Jamii mwaka 1991 kuwa chuo kisijihusishe na maslahi ya wanafunzi chuoni.

Hivyo serikali ilitakiwa ilete 'tuition fee,' mishahara na stahili za wahadhiri na wafanyakazi wengine, halafu wanafunzi 'wapambane na hali zao.'

Kama ingeachwa wazazi na walezi wenye fedha wakawalipia vijana wao, na wengine wabaki nyumbani au watafute pa kujishikiza bila hitaji la masomo ya ziada pengine hakuna mwenye jibu kuwa ingekuwaje leo.

Kiitikadi, kulikuwa na mielekeo miwili ikishabihiana licha ya kuwa ina ncha tofauti huko ilikotoka. Mwelekeo wa kwanza ulikuwa ni wa Benki ya Dunia (WB), ambayo ilitaka gharama za huduma za jamii zionyeshwe kwa uhalisia wake na watumiaji warudishe hizo gharama, ili serikali iweze kupanua huduma za jamii kwa uwezo ilionao, na si kungoja misaada iongezeke ili huduma zipanuliwe.

Hivyo sera ya 'kuchangia gharama' ikaingia mahospitalini, wakulima wakanyimwa ruzuku ya pembejeo na wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu kutakiwa waombe mikopo wasome na warudishe fedha baadaye wakihitimu tena kwa utaratibu wa riba.

Mwelekeo mwingine ulikuwa ni wa kitaifa, ulioenea serikalini wakati huo kuwa 'kila mtu atauchukua mzigo wake mwenyewe,' na kwa mantiki hiyo taifa lilikuwa na wawekezaji binafsi wa vyuo vya elimu ya juu hivyo walikuwa tayari elimu ya vyuo na vyuo vikuu iwe ndani ya huduma za kibiashara ila umiliki usibadilishwe.

Vyuo vingetakiwa vipate fedha za kujiendesha kutoka kwa wanaotumia huduma zao, hivyo wazazi kulipia kama ambavyo wengi wanawapeleka vijana wao nchi za nje. Walikuwa wakisema waziwazi kuwa Watanzania wanapenda vitu vya dezo hisia ya kibwanyenye ya kuwadharau wasiokuwa na uwezo wa kusomesha vijana vyuoni.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda, akitoa ufafanuzi kujibu masuala mbalimbali bungeni. **PICHA: BUNGE**

> Kama ingeachwa wazazi na walezi wenye fedha wakawalipia vijana wao, na wengine wabaki nyumbani au watafute...

Kubuniwa mkakati wa mikopo hasa kuliondoa migomo ya mara kwa mara vyuoni kwani utawala chuo kikuu haukuwa ukihusika na kutokea fedha za kujikimu.

Migomo ikahamia wizarani wakati ikiwa ndiyo inasimamia kutolewa mikopo, halafu ikaundwa bodi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Yako maswali mengi kuhusu utendaji wake, lakini la ziada ni kuwa mwaka huu ilipata fedha za kutosha kuwakopesha vijana 42,000 wakati waliofaulu kuingia vyuo vikuu, wakapata nafasi, walikuwa 70,000 na hivyo serikali ikabidi kuamua endapo wabaki nyumbani.

Rais Samia Suluhu Hassan akaamua kuwalipia wengine walioomba lakini wakakosa.

Licha ya kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliwaeleza wabunge kuwa vijana hao 28,000 watangulie vyuoni walikopata nafasi huku serikali ikitafuta fedha hizo kuna maswali yanayoibuka.

> Uwepo wa mifumo ya utambulisho kama namba za NIDA kutumiwa kokote unaweka njia ya kufuatilia walipo, tofauti...

Endapo serikali inataka kuhakikisha kuwa kila kijana aliyekubaliwa na chuo kikuu kimojawapo anaendelea na masomo bila kutegemea kupata mkopo, kuna haja ya kuendelea na mfumo huo?

Kwa mfano serikali imetoa Shilingi bilioni 570 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi 42,000 pekee.

Kama fedha hizo zingepelekwa vyuoni na viwepo vyanzo vingine, zingetosha kusomesha vijana wote 70,000 au la? Wangesoma, wahitaji tu chakula na malazi?

Suala linaloibuka ni kama kuna haja ya kuwepo bodi ya kukopesha ili fedha hizo zirudishwe baadaye. Kwa vile mkakati huo unakidhi haja tu ya mahitaji ya kusomesha vijana, na serikali haitaki kupigilia msumari uwepo wa mikopo na uwezo wa kusoma, au kujitegemea na kusahaulika, kuna pengo.

Ina maana kuwa fedha za serikali ingefaa zitumike kuendesha vyuo, halafu njia zitafutwe za kupata mikopo kujikimu bila viwango hivi vya sasa, fedha za wizara zitoshe.

Si rahisi kusema kama ufadhili na uwajibikaji binafsi wa kijamii ungetafutwa ili kila anayepata nafasi akasome na mikopo itoke benki za biashara kwa riba, SACCOS au amana za uwekezaji na hifadhi ya jamii, mikopo ya miaka kadhaa

Uwepo wa mifumo ya utambulisho kama namba za NIDA kutumiwa kokote unaweka njia ya kufuatilia walipo, tofauti na kuajiri bodi ishughulikie ufuatiliaji wa mikopo. Halafu theluthi moja ya wanaostahili wasipate fedha zilizopangwa.

Bado kuna tatizo la jinsi ya kujumuisha uwezo wa kusoma na kupata chakula na malazi, na jinsi uwezo wa wazazi unavyoweza kuingizwa katika suala hilo, na fedha za serikali zilipie nini katika mpangilio huo. Ila tumepiga hatua ya kuachana na dhana kuwa kusoma ngazi ya chuo au chuo kikuu inategemea uwezo wa mzazi husika, na kulenga kupata fedha za kutosha za mikopo, wakati ambapo fedha hizo zingepelekwa katika vyuo zingewezesha kuhudumia wanafunzi kwa ufanisi, ubora zaidi.

Endapo serikali iko tayari kulipia wanafunzi 28,000 kuna udhaifu wa kutumia mikopo kwa 42,000 licha ya kuwepo mantiki kwa upande mmoja.

Waliopata mikopo walihakikishiwa watasoma bila taabu ila wana mzigo mbeleni kulipa fadhila hiyo, na waliokosa wasingekuwa na uhakika wa kuingia vyuoni, lakini bado hatujasikia kuwa ni fedha za ziada za mikopo wafanane ikimaanisha wanalipiwa moja kwa moja na serikali au wanakopeshwa.

Sasa inaelekea waliokosa watapewa mikopo baada ya serikali , Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa , wakati akiahirisha bunge kutangaza wanafunzi hao waende shuleni.

# DRC yatupa karata ya mwisho kwa mzozo wa Kivu Kaskazini



Baadhi ya vikosi vya DRC vinavyopambana na majeshi ya M23. **PICHA: RFI**

**Na Ani Jozeni**

VITA inayoendelea kwenye jimbo la Kivu Kaskazini huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) inaelezwa kuwa sasa 'inakomaa.' Vikosi vya kundi la waasi (la Watutsi wa mashariki ya DRC wanaoungwa mkono na nchi jirani ya Rwanda) vinaelezwa kuwa vinasonga mbele maeneo tofauti ya mkoa wa Kivu Kaskazini ambao unapakana na nchi za Uganda, Rwanda na Burundi.

Hali hiyo imesababisha watu kuyakimbia makazi yao wakitafuta usalama Uganda na nchi nyingine jirani.

Hali hiyo inaelekea inaendana na kinachotokea nchini Rwanda, ambako DRC ni moja ya maeneo yake ya kimkakati, kuchochea vita au kupunguza kulingana na mahitaji yake ya kuchimba madini bila kubughudhiwa na serikali ya DRC.

Katika mkakati huo ina washirika wasio rasmi kwa mfano Uganda ambayo haijawahi kuwa na sera ya wazi kuhusu DRC, kwa mfano nini inafanya kupambana na kundi la uasi (unaojibandika 'bashasha' ya Uislamu, au hata wa siasa kali) la ADF - Alliance of Democratic Forces.

Cha kushangaza ni kuwa licha ya kundi hilo kujitambulisha kama linalopambana na watawala nchini Uganda, limehamia DRC na linaendesha shughuli zake huko, ikiwemo kuchimba madini bila kuingiliwa, pia.

Miezi kadhaa iliyopita aliyekuwa mkuu wa majeshi ya ardhini ya Uganda na mwanae Rais Museveni, Jenerali Kainerugaba Muhoozi, alitangaza kupelekwa kwa vikosi vya Uganda kusaidiana na vile vya DRC katika eneo linalosumbuliwa na ADF, na hasa kupanuka shughuli za M23.

Haikuwa bayana ni malengo gani ya pamoja yalifikiwa lakini vikosi hivyo viliondolewa muda si mrefu, wakati ambapo Jenerali Muhoozi akikorofosha zaidi hisia za watu, akiwa kama anatoa siri.

Hakupeleka vikosi hivyo kusaidia nchi hiyo ila kuwa 'jeshi mwenza' la eneo hilo, ila akasita kuunganisha kazi ya vikosi vyake na M23, hivyo akawa hana pa kusimama, kwani ADF hawateki maeneo. Wanapiga na kupora au walinde kambi za kuchimba madini, tofauti na M23 wanaotaka watambuliwe kama serikali.

Mzozo wa kidiplomasia umekuwa unalenga kuungwa mkono M23 na Rwanda, hata nchi kadhaa zenye nguvu zikajaribu kuwakutanisha watawala wa DRC na Rwanda kwa suala hilo, akiwemo Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa miezi kadhaa iliyopita.

> Tayari kuna mvutano mkubwa wa kutafuta au kukubaliana nani aiongoze tume huru ya taifa ya uchaguzi, ambako tofauti na Kenya ambako rais anamteua mwenyekiti huyo, DRC ni wakuu wa vyama bungeni wanaokubaliana, kila chama...

Hata hivyo, hajachukua hatua yoyote dhidi ya Rwanda kwani serikali yake kwa miaka kadhaa inatafuta njia ya kurudisha mahusiano yaliyovurugwa na mauaji ya kimbari ya mwaka 1994 ambako Ufaransa iliwaachia watawala wa Kihutu kuangamiza Wahutu.

Pia walisaidia vikosi vya jeshi la wauaji kujikita huko DRC, kukwepa kampeni za 'safishasafisha' za Rwanda maeneo tofauti tangu mwaka 1997.

Kundi hilo la jeshi ambalo ni pamoja na wakimbizi wa Wahutu wa siasa kali wasiotaka muafaka wowote na Watutsi ni chanzo cha wasiwasi mkubwa kwa upande wa Rwanda unaoleta kihoro.

Wanahofia watu hao wazaane na kufikia tuseme milioni moja na dhamira yao iko pale pale kurudi Rwanda kuua Watutsi kama katika mlipuko wa mauaji mwaka 1994.

Kwa hiyo Rwanda ikaubuni mradi wa M23 wa kuvugurika majadiliano ya amani DRC kuunda kundi la kijeshi kuwa 'tuta' kati yake na DRC. Kutatua uwepo wa M23 budi uhusishe FDLR - kundi la 'kidemokrasia' la 'ukombozi' wa Rwanda linalotokana na mauaji ya halaiki.

Ndiyo maana inakuwa vigumu kusema nini hatma ya 'mchongo' wa kivita na pia kidiplomasia wakati huu, ambakoo kwa mara nyingine tena nchi kadhaa za Afrika zinaona umuhimu wa kupeleka vikosi kuisaidia DRC dhidi ya M23.

Tofauti kubwa kijeshi ni kuwa licha ya umuhimu wa kimkakati wa FDLR hawako vitani kuteka eneo lolote la DRC au kukaribia mipaka ya Rwanda ila linaonekana kama tishio la muda mrefu.

Ni hisia iliyojikita zaidi katika historia na siyo katika hali halisi, na kwa upande mwingine ni kielelezo cha tatizo la kuondoa migogoro na makundi au wapiganaji au waasi wanaofikia mamia waliotapakaa majimbo tofauti.

Kisiasa, kupanuka kwa shughuli za M23 kumelazimisha wanasiasa DRC kuanza kuweka kando tofauti zao za kina, na hasa kuhusiana na uchaguzi mkuu ambao unatakiwa kufanyika Desemba 2023.

Tayari kuna mvutano mkubwa wa kutafuta au kukubaliana nani aiongoze tume huru ya taifa ya uchaguzi, ambako tofauti na Kenya ambako rais anamteua mwenyekiti hiyo, DRC ni wakuu wa vyama bungeni wanaokubaliana, kila chama kikiwa na kura moja.

Halafu wafikie makubaliano na viongozi wa makundi ya dini, hasa madhehebu makuu ya Katoliki na Protestanti.

Hivi sasa wananchi wa Congo ni kama wamelazimishwa kuweka kando tofauti zao ili kupambana kwanza na M23 kumega nchi hatua kwa hatua, kuunda kijamhuri cha Kitutsi jimbo la Kivu Kaskazini.

Wakati nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki bado zinasuasua kuhusu kupeleka vikosi kupambana na M23 na kuhakikisha mipaka ya DRC kama mwanachama wa jumuia, ni Kenya tu ambayo imepeleka vikosi.

Burundi bado ina makundi ya waasi na mzozo wa M23 siyo saizi yake, tofauti na Kenya ambayo imekuwa bega kwa bega na Uganda, Rwanda, kufifisha uwepo wa kundi la Al Shabaab linaloshika maeneo makubwa nchini Somalia.

Baadhi pia wanaamini Kenya inataka kuwa mshirika wa karibu zaidi na Marekani kuliko awali, ambako utawala uliopita ulikuwa karibu zaidi na serikali ya Uingereza.

Kimsingi serikali ya Rais Joe Biden inasongwa na makundi kadhaa ya haki za binadamu nchini Marekani ambayo yamechoshwa na utawala wa Rais Paul Kagame wa Rwanda na kwa upande mwingine Rais Yoweri Museveni wa Uganda.

Kuhitajiwa kwa ndege za kuwahisha misaada kila siku DRC wakati kuna milipuko ya maafa kila kukicha kunaponza utayari wa kutumia njia za kidiplomasia kuikumbusha Rwanda kuhusu suala hilo.

Itabidi M23 warudi nyuma na hata silaha zao zipunguzwe, na labda Rais Kagame angoje matokeo ya uchaguzi mkuu ujao Marekani kwani hata sasa wafuasi wa rais wa awali Donald Trump, asiyetaka kujihusisha na Waafrika wakiuana wenyewe kwa wenyewe, wanachukua tena ukanda Baraza la Wawakilishi.

Msukumo wa kuchukua hatua utapungua kwa Rais Biden, ila atafuatilia hatua zinazochukuliwa sasa kama sehemu ya utetezi mpana wa haki za binadamu, amani.

JUKWAA LA VIONGOZI

EDIMUND SENGONDO MVUNGI 1952- 2013

# Jina kubwa linalodumu linaloendelea kuishi mioyoni mwa tasnia, sekta nyingi

• Anakumbukwa kinara aliyepigania katiba mpya



Dk. Edmund Sengondo Mvungi

**Na Gaudensia Mngumi**

LEO imetimia miaka tisa tangu kufariki dunia katika hospitali ya Milpark huko Afrika Kusini mwaka 2013, Dk. Edmund Sengondo Mvungi, ni karibu muongo mmoja wa tafakari.

Bado daktari Mvungi ni jina kubwa au wengine wangemwita jembe, akiwa na mchango mkubwa katika sekta na tasnia nyingi za Tanzania Bara na Visiwani kuanzia habari, sheria, siasa, taaluma vyuo vikuu na mikataba.

Hata sasa Mvungi anakumbukwa na anatajwa wakati taifa linapoendelea na mchakato wa kuandika katiba mpya.

Bado kwenye uwakili mahakamani, uhadhiri vyuoni, harakati za kidemokrasia na utetezi wa haki za binadamu na hata ndani ya asasi za kiraia, jina lake linatajwa, hasa kwa kuwa alipoteza maisha akiwa kwenye jukumu la kuandaa katiba.

Kifo cha Dk. Mvungi kiliwaudhi na kuwashangaza Watanzania hasa kwa sababu ya unyama aliofanyiwa na watu waliodaiwa kuwa ni majambazi.

Walimvamia nyumbani kwake Kibwegere eneo la Kibamba jijini Dar es Salaam na kumkata mapanga kichwani na kusababisha kifo chake, wakati huo akiwa mshiriki wa mchakato wa kuandika katiba mpya.

Ni kazi iliyokuwa ikifanywa na Tume ya Jaji Warioba kwa miezi 18, jukumu lililokuwa likitamaniwa na hata leo likiwagusa Watanzania wote.

Habari za kifo chake licha ya kuwaogopesha na kuwashangaza Watanzania zilitikisa mataifa mbali mbali, kwa namna ya ajabu ziliwastua wanakijiji chake cha Chanjale kilichoko Mwanga mkoani Kilimanjaro, wafanyakazi wenzake wanasheria na wahadhiri wa vyuo vikuu vya Dar es Salaam na Bagamoyo, wanafunzi wa vyuo, umma wa wanahabari, wanasiasa kwa namna ya kipekee chama cha NCCR-Mageuzi na kambi ya upinzani.

Kisiasa Dk.Mvungi aliwahi kugombea urais kupitia NCCR-Mageuzi na alikuwa msuli wa chama hicho, aidha, kiliwashangaza jumuiya ya asasi za kirai, wanaharakati na watetezi wa haki za binadamu ni kutokana na mchango wake mkubwa katika kutoa mielekeo, kuhamasisha mabadiliko na kubwa kuandaa katiba mpya.

**CHANZO CHA KIFO**

Kutoka hospitali ya Millpark ya Johannesburg huko Afrika Kusini, wataalamu walieleza kuwa madaktari waliokuwa wakimtibu Kamishna wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Dk. Mvungi, alifariki kutokana na maji yanayoutunza ubongo "cerebrospinal fluids"' CCF.

Alifariki kutokana na kucheleweshwa kupata tiba baada ya maji ambayo ubongo unaelea ndani yake kumwagika.

Dokta Mvungi aliyezaliwa mwaka 1952 alifariki akiwa na miaka (61), alipata majeraha baada ya kupigwa kichwani baada ya kuvamiwa Novemba 3 nyumbani kwake usiku wa manane.

**KILIO KILIPOTANGAZWA**

Ni Katibu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Assaa Rashid, anayetangaza kifo cha Dk Mvungi: "Kwa masikitiko makubwa, tume inawatangazia Watanzania kuwa Dk. Sengondo Mvungi, mjumbe wa tume amefariki dunia Jumanne, Novemba 12, 2013, saa 8:30 mchana kwa saa za Afrika Kusini."

Tangazo hilo huenda liliwaudhi Watanzania na uchungu wa kuuawa kikatili mjumbe wa tume hiyo katika kipindi ambacho mchango wake ulihitajika kwenye kufanikisha mabadiliko ya katiba, umeendelea kubaki mioyoni mwao hata leo, taifa linapoendelea kusaka katiba mpya.

Marehemu Dk.Mvungi alizikwa nyumbani kwao Kitongoji cha Chamakera Kisangara Juu na ujumbe wa kila aina ulimminika kuonyesha namna watu na waomboleza walivyoguswa na mmoja wa watoa salamu alikuwa ni Mwigulu Nchemba, akiwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, aliyesema.

"Nawasihi waombolezaji na Watanzania wote tukemee na kuombea taifa letu lisipatwe na huyu pepo wa mauaji anayeendelea kuitesa, nchi yetu.

Naomba ushirikiano wa wananchi na vyombo vya usalama kufichua mitandao hii ya unyama na mauaji. Nasisitiza kuwa taifa hili linapatwa na mikasa kwa sababu halina hofu na Mungu. Hivyo ni wakati wa kuomba kama taifa na kushikamana kuombea nchi yetu kwa ujumla hatimaye kufichua maovu yote."

Anaungwa mkono na James Mbatia, aliyekuwa Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi wakati huo akisema: "Naomba serikali iimarishe ulinzi kwa gharama yoyote ile, ichukue hatua madhubuti kupambana na watu wanaojihusisha na vitendo vya kinyama kama hiki alichofanyiwa Dk. Mvungi cha kuvamiwa na kukatwa mapanga kitendo kilichosababisha kifo chake."

Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Jaji Joseph Warioba, akiwa Kisangara Juu ilikofanyika ibada ya mazishi ya Dk. Mvungi, naye alitoa salamu za rambirambi kwa kusema, alikuwa msaada mkubwa na mtu muhimu katika mchakato wa kuandaa katiba mpya. "Alitanguliza utaifa mbele na kuachana na ushabiki wa chama."

Watoto wa Dk. Mvungi wakiongozwa na binti yake Natujwa Mvungi, kwa masikitiko walizungumza mambo yaliyogusa mioyo ya Watanzania, wakiishukuru serikali na NCCR-Mageuzi kwa juhudi za kuokoa maisha ya baba yao lakini haikuwezekana na kuahidi kusoma na kufanyakazi kama alivyofanya baba yao ili baadaye wawe msaada kwa taifa bila kujali itikadi za vyama kama baba yao alivyofanya wakati wa uhai.

Waziri Mkuu wa awamu ya nne, Mizengo Pinda 'Mtoto wa Mkulima' ni miongoni mwa walitoa salamu za rambirambi siku ya mazishi ya shujaa Mvungi, akiwaomba Watanzania kujiepusha na matendo ya kuua watu na kumwaga damu jambo ambalo ni chukizo kwa Mungu.

Kazi za Dk. Mvungi hazitasahaulika kutokana na ujasiri wake katika masuala ya kuleta maendeleo kwenye jamii yake, akiwa mstari wa mbele kwenye ujenzi wa miundombinu kama shule za sekondari za Kisangara Juu, kanisa , kujenga barabara na kuwaunganisha wananchi.

Si hivyo tu kwenye siasa, kutafuta haki kwa wanaoikosa, alikuwa mstari wa mbele hakuwa na tama ya utajiri na aliishi maisha ya kawaida akisaidia watu mbalimbali kuanzia ndani na nje ya familia yake.

Wakazi wa Kisangara Juu na Kata nzima ya Ngujini wanamkumbuka Dk. Mvungi, akiwa ni miongoni mwa waasisi wa Chama cha Umoja wa Wanangujini-NGUDEA, kilichowekeza juhudi na mikakati katika kujiletea maendeleo kwa kutumia nguvu na hamasa za wananchi wa kata ya Ngujini.

Mvungi ni mtu aliyependa nyumbani kwake na kila mwaka kuanzia Desemba hadi Januari alikuwa nyumbani kwake kuzungumza na wananchi, vijana kwa wazee na viongozi mbalimbali kuhamasisha maendeleo ili kubadilisha maisha ya wananchi.

Ni msomi na jasiri asiyetaka sifa kwa ajili yake bali aliyependa watu kwanza, akiwaeleza mawazo na kile anachodhani kinafaa kwa ajili ya maendeleo yao, ndiyo maana rafiki yake kipenzi Dk. Harrison Mwakyembe, akizugumza katika mazishi yake alisemam hakuwa mwoga. "Hakuwa mwoga kutoa mawazo yake kwa kile alichokiamini,"

Wakati akimuaga, kwenye mazishi yake, rafiki mwingine wa Dk. Mvungi na mwanazuoni wa sheria, anayezungumzia kifo hicho ni Profesa Palamagamba Kabudi, alimfananisha na chui, akisema aliitwa "nguto" kwa Kipare ni chui, mnyama hodari kutokana na ujasiri katika kuamua mambo mazito na magumu kuanzia ya kitaaluma na ya kisiasa kwa mustakabala wa jamii na taifa.

CHADEMA MGOMO RUZUKU

# Wadai bado hawatambui uchaguzi 2020,Msajili vyama asita kuwagusa

**INATOKA UK. 13**

ni kwamba hawaukubali.

WANASTAHILI

Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi , anapoulizwa na Nipashe kuhusu suala la ruzuku, anasema chama hicho kinastahili kupata ruzuku.

Hata hivyo hakufafanua kiasi ambacho kinatakiwa kupokea na kama kimeshaanza kupata fedha hizo au bado.

"Wewe elewa tu kwamba wanastahili kupata ruzuku, inatosha," anajibu kwa kifupi Jaji Mutungi , anapoulizwa na gazeti hili kuhusu CHADEMA kupokea ruzuku na kiasi ambacho chama hicho kinatakiwa kupata.

Msimamo huo wa Jaji Mutungi ni sawa na ule uliouonyesha miezi miwili baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 alipoulizwa na gazeti moja ili kutoa ufafanuzi wa idadi ya vyama vyenye sifa ya kupata ruzuku.

Baadhi ya vyama ambavyo vilitakiwa kupata ruzuku kulingana na idadi ya wabunge, madiwani na kura za urais vilikuwa ni CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo, CUF na NCCR-Mageuzi.

Hata hivyo, kwa upande wake Jaji Mutungi wakati huo, hakutolea ufafanuzi suala hilo badala yake akakaririwa akijibu kwa kifupi tu kwamba hafahamu kuhusu kutolewa kwa ruzuku kwa vyama hivyo.

**MSIMAMO KISHERIA**

Mwanasheria, Bob Wangwe ambaye pia ni Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), anasema chama hicho kina haki ya kupokea ruzuku na pia hakiwezi kulazimishwa kupokea kama kinaona kuna jambo haliko sawa.

"Kwa mfano hao CHADEMA wamekuwa wakidai kwamba uchaguzi mkuu haukuwa huru na haki, hawawezi kulazimishwa kupokea kama wanaamini hilo na kuamua kuisusia hiyo ruzuku," anasema Wangwe.

Wangwe anafafanua kuwa; "Sheria Namba 5 ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2019, haitoi nafasi ya kumlazimisha mtu au chama kupokea ruzuku."



Mbunge wa Nkasi Kaskazini-CHADEMA, Aida Khenan, ndiye pekee aliyechaguliwa kutoka jimboni kwenye uchaguzi mkuu wa 2020. **PICHA: BBC SWAHILI.**

Anafafanua kwamba, kwa kuwa huo ndio msimamo wa viongozi wa chama hicho, ambao hauendi kinyume na Sheria ya Vyama vya Siasa na hata ya Taifa ya Uchaguzi, wanaweza kuendelea nao.

"Sina vitabu vya sheria hizo, kwa hiyo sikumbuki vifungu vyake, lakini ukweli ndio huo kwamba hakuna sheria inayowalazimisha kupokea ruzuku, wanaweza kuendelea na msimamo huo au wakaachana nao," anasema. Baadhi ya wadau wakiuzungumzia msimamo huo, wanasema unakuja wakati kuna jitihada zinazofanywa na awamu ya sita ambao ni kufungua tena uwanja wa demokrasia na kuwaletea Watanzania maridhiano ya kisiasa na umoja bila kujali tofauti zao za kisiasa.

Wanasema hatua hiyo ni msimamo wa chama lakini pia ungeangalia mwelekeo wa serikali wa kutaka kuwa na maridhiano na kuponya majeraha yaliyotokana na michakato na harakati za kidemokrasi wakati wa awamu ya tano.

Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, inasisitiza maridhiano ya kisiasa na ustahimilivu hatua inayolenga kuwapo na usawa na kutobaguliwa, fursa sawa kwa wananchi wote na vyama vya siasa ili kila mtu afurahie haki zake za msingi na kutekeleza majukumu kwa uhuru na kwa mujibu wa sheria.

Hivi karibuni, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nape Nnauye alifafanua kuwa Rais Samia, anaongozwa na mambo manne kwenye kusimamia maendeleo, akitaja maridhiano, ustahimilivu, mageuzi na kujenga upya Tanzania ili kuwaleta pamoja bila kujali tofauti za kisiasa na kuhakikisha utawala wa sheria, usawa na kutobaguliwa.

Katika ajenda ya ustahimilivu, Rais Samia anaamini katika kuhakikisha raia wanapatanishwa na wanapaswa kupona kutokana na shida yoyote iliyokuwapo huko nyuma katika awamu zote za uongozi wa nchi.

Aidha anasema kuwa, wote wanapaswa kukabiliana na changamoto za maendeleo kama taifa katika umoja na mshikamano ili nchi isonge mbele kwa kujiamini.

Waziri Nnauye anafafanua kuwa mageuzi ya msingi na muhimu ya kiuchumi, kisiasa na uchaguzi yatahakikisha sheria na haki nchini zinapatikana ili uchumi ukua na kuzalisha ajira kwa watu wake.

"Mageuzi haya yanapaswa kuimarisha juhudi zetu kuelekea kuwa na jamii yenye haki, kustawi kwa demokrasia na uchumi unaokua kwa faida ya Watanzania wote,"anasema Waziri.


Hata hivyo, ni vyema kuzungumza na kuainisha dukuduku zinazowaumiza wanasiasa na kuzimaliza ili mipango ya kuwa na uwanja mpana wa demokrasia, uvumilivu wa kisiasa na kukubali kutokukubaliana unaotoa fursa kwa wote unufaishe wanasiasa na vyama vyote pia.

## CHEMSHABONGO NA -00 22 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. Msaidizi wa Mungu
6. kinga
7. eleza
8. magoli
10.bara la pili kwa ukubwa
13.filimbi
14.jina la kale Afrika mashariki
15.sujudia mtu kwa kuinamisha kichwa 17.kinywani
20.wingi wa mlei
21.epusha mtu na janga
22.huzaa ndizi


Chini:
1. Mtu asiyekuwa na dini
2. Monrovia ni mji wake mkuu
3. chukua bila ruhusa
4. usawa juu ya ardhi
5. Mji mkuu wa Tanzania
8. mimea
9. shina la kuti 11. tenda
12.mtu asiyesikia maagizo
16.tendo la kumega
18.jimbo
19.oana kwa mke na mume




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

UHALIFU
MAKINI
ABELI
LILIGA
IGIZA
MZAZI
ARAKA
IRANI
AZIMIO
CHAKI
MHAYA
AMINI
TAMAA
KANYA

HADI
IASI
HABA
AGA
GAMU
AKUA
AUA
AMU
ONJA
DAU
KOMAA



Majibu toleo lililopita







# Mpango kuzindua mkutano wa mabonde ya maji nchini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAKAMU wa Rais wa Tanzania, Dk. Isdory Mpango, anatarajiwa kuzindua mkutano wa nane wa mabonde yote nchini unaonza leo jijini hapa, unaokwenda na kampeni ya upandaji miti zaidi ya milioni mbili kwenye mabonde yote.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema Dk. Mpango atazindua kampeni hiyo kukabiliana mabadiliko ya tabianchi na miti rafiki itapandwa kwenye vyanzo mbalimbali vya maji.

Pia kutakuwa na utiaji saini wa mikataba ya kisekta kwa ajili ya uhifadhi wa miti kwenye vyanzo vya miti kuzindua mipango ya uhifadhi ya vyanzo vya maji nchini pamoja na wasilisho za utafiti uliofanyika kwa ajili rasimali za maji.

**Tusimamie misingi ya ufundishaji ili wilaya yetu ifanye vizuri, wasiwapo watoto wanaoishia njiani, kama kuna kikwazo ofisi yangu iko wazi njoo tuyajenge.**

Wizara ya Maji imeandaa mkutano mkuu wa nane wa bodi za maji za mabonde unaofanyika leo kaulimbiu ya mkutano huo ni "utunzaji endelevu wa vyanzo vya maji kwa ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi" ufunguzi ambao unaenda sambamba na kupanda miti rafiki wa maji kwenye vyanzo maeneo mbalimbali nchini," alisema Dk. Chuachua.

Akizungumzia kampeni hiyo ya upandaji miti kwenye vyanzo vya maji, Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji kutoka Wizara ya Maji, Dk. George Lugomela, alisema upandaji miti utasaidia kuepukana na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, aliwashauri wananchi kuachana na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji kama kilimo, uvuvi, kukata miti na kuchoma mkaa ili kutunza vyanzo vilivyoko.

"Mkutano huu unalenga kujadili kwa pamoja mabadiliko ya tabianchi, mambo mbalimbali yatafanyika ikiwamo kujadili vikwazo vinavyochangia vyanzo vya maji kukauka, tutazindua mipango ya uhifadhi wa vidaka maji nchini pamoja na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti na maandiko mbalimbali yanayohusiana na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali," alisema Dk. Lugomela.



Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji kutoka Wizara ya Maji, Dk. George Lugomela (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Mbeya jana, kuhusu maandalizi ya mkutano wa nane wa mabonde ya maji nchini unaofanyika leo jijini humo. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Familia ya mchungaji yanusurika kifo nyumba ikiteketea kwa moto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATU sita wa familia ya mchungaji wa Kanisa Baptist Itezi jijini hapo, Daniel Mwandenga, wamenusurika kufa baada ya nyumba yao kuteketea kwa moto.

Katika tukio hilo, mali zote na samani zilizokuwa ndani ya nyumba hiyo zimeteketea huku askari wa Jeshi la Zimamoto lililokwenda kuzima mto huo likitimuliwa na wananchi kwa kuchelewa kufika eneo la tukio.

Akizungumzia tukio hilo jana, mke wa mchungaji, Rebeka Mwandenga, alisema moto huo ulizuka ghafla Novemba 14, majira ya saa 12 jioni katika moja ya chumba ambacho hakikuwa na umeme na kusambaa kwenye nyumba yote na kuteketeza vitu vyote vilivyokuwa ndani.

Rebeka alisema chanzo cha moto hakijajulikana kwa kuwa ulizuka kimiujiza kutokana na chumba ambacho hakikuwa na umeme.

"Kilitokea kama kimbunga ndani ya chumba ambacho hakikuwa na umeme sisi tulikuwa nje, kuna mtoto alishtuka na kuniuliza mama mbona kuna moto unawaka ndani, nikakimbia kuingia ndani ndipo tukaona moto unazidi kuwaka, nikatoka nje kuomba msaada kwa majirani na kumtoa mtoto mdogo aliyekuwa amelala, lakini kwa bahati mbaya sikufanikiwa kuokoa kitu chochote zaidi ya familia yangu kunusurika," alisema Rebeka.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Itezi Mashariki, Michael Kwimba, alisema alipigiwa simu na majirani wa mchungaji kuhusu tukio hilo na alifika eneo la tukio moto ukiwa umezimwa na wananchi.

Aliwashukuru wakazi wa Itezi Mashariki kushirikiana kuuzima ingawa uliteketeza vitu vyote vilivyokuwa ndani ya nyumba hiyo.

Alisema jitihada hizo, zimesaidia kuokoa uhai wa familia hiyo licha ya kuwa hakukuwa na vifaa vya kisasa kusaidia kuokoa mali zilizokuwa ndani ya nyumba hiyo na kusababisha hasara.

Baadhi ya vijana waliofanya kazi ya kuzima moto walisema licha ya kuunganisha nguvu zao, walishindwa kuuzima kwa wakati kutokana na uhaba wa vifaa vya kukabiliana na moto huo.

Shadrack Zawadi, alisema licha ya kuwa na ari ya kuuzima moto huo, walikwamishwa na vitendea kazi ambavyo vingewasaidia kukabiliana nao na kuokoa mali na samani zilizokuwa ndani ya nyumba hiyo.

"Vijana wote wa mtaa huu tuliungana kuhakikisha moto huu unazimwa lakini tulitumia muda mrefu kwa sababu tulikuwa tunatumia njia za asili kuuzima kutokana na ukosefu wa vifaa vya kisasa, tunaiomba serikali kuwa mstari wa mbele kukabiliana na majanga kama haya," alisema Zawadi.

Alisema gari la zimamoto lilichelewa kufika eneo la tukio hali iliyosababisha wananchi kushikwa na hasira na kuwafukuza eneo hilo huku akiiomba serikali kuchukua hatua za mapema yanapotokea majanga kama hayo.

## LATRA yafanya ukaguzi wa kushtukiza tiketi mtandao

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) imefanya ukaguzi wa kushtukiza wa matumizi ya tiketi mtandao kwa mabasi yanayofanya safari zake kuanzia jijini hapo kuelekea mikoa mbalimbali nchini.

Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Mbeya, Omary Ayoub, alisema lengo la ukaguzi huo ni kutaka kuhakikisha abiria wote wanakata tiketi za kimtandao ambazo zina manufaa makubwa kwa wadau wote wa usafirishaji.

Alisema ukaguzi huo ni mwanzo wa maandalizi ya kudhibiti ukiukwaji wa sheria za usafirishaji nchini hasa katika kuelekea kwenye sikukuu za mwisho wa mwaka abiria wanapoongezeka maradufu.

"Ukaguzi wetu huu pia ni maandalizi ya udhibiti wa hali ya usafiri hasa katika kipindi hiki cha kuelekea mwisho wa mwaka ambapo uzoefu unatuonyesha kuwa idadi ya abiria huongezeka na kusababisha ukiukwaji mkubwa wa sheria na wananchi kudhulumiwa," alisema Ayoub.

Akizungumzia faida za wananchi kukata tiketi mtandao, Ayoub alisema kuwa zinasaidia serikali kukusanya mapato inayostahili, wamiliki wa vyombo vya usafiri kutoibiwa na watumishi wa magari yao na kuepusha wananchi kudhulumiwa kwa kutozwa nauli kubwa kupita viwango elekezi vilivyopangwa na serikali.

Baadhi ya abiria waliozungumzia matumizi ya tiketi mtandao, walisema kuwa mfumo huo ni mzuri na unawasaidia kwa kiwango kikubwa kuepuka usumbufu waliokuwa wakiupata hapo awali.

Jumanne Hamis, alisema kuwa utaratibu huo unawasaidia kukata tiketi za safari zao bila kulazimika kufika kwenye ofisi za mawakala wa mabasi na pia tabia ya kugonganishwa abiria zaidi ya mmoja kwenye kiti kimoja imekomeshwa.

"Mfumo huu sisi tunaona unafaa, kwa sababu tunapata tiketi bila kufika kwenye ofisi za mabasi, lakini tunaona tunalipa nauli ile ile iliyopangwa na serikali bila kuzidishiwa na wapigadebe," alisema Hamis.

Serikali kupitia LATRA imeanzisha utaratibu wa kuwataka wamiliki wa mabasi kutoa huduma za usafirishaji wa abiria nchini kwa kutumia tiketi mtandao na kuachana na tiketi za makaratasi.

**Mfumo huu sisi tunaona unafaa, kwa sababu tunapata tiketi bila kufika kwenye ofisi za mabasi, lakini tunaona tunalipa nauli ile ile iliyopangwa na serikali bila kuzidishiwa na wapigadebe.**



# Ikulu ya Chamwino yakamilika asilimia 100

Na Augusta Njoji, DODOMA

UJENZI wa Ikulu ya Chamwino umekamilika kwa asilimia 100 ambao majengo yake yanafanana na Ikulu ya Dar es Salaam.

Kutokana na unyeti wake, serikali ililipa jukumu la ujenzi wa Ikulu hiyo Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Akizungumza jana kwenye Kituo cha runinga cha TBC, Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajab Mabele, alisema wataalamu waliochora na waliojenga ni kutoka JKT ambao ni maofisa na askari.

"Kiusalama ni jambo la juu kumleta mtu wa nje kutengeneza chumba chako unacholala, sidhani kama ni sahihi lakini kwa uamuzi wa serikali kuwatumia wataalamu wa ndani tena wa jeshi, kiusalama ni jambo zuri sana," alisema.

Jenerali Mabele alisema ujenzi huo umefanyika usiku na mchana kwa takribani miaka miwili na miezi tisa.

**Mimi kwangu ni fahari maana zipo taasisi nyingi zinazofanya kazi ya ujenzi lakini kwa kipekee kwa kuchagua Jeshi la Kujenga Taifa kupitia SUMA JKT (Shirila la Uzalishaji Mali la JKT) wafanye kazi ya ujenzi wa Ikulu, mimi kwangu ni fahari.**

"Mimi kwangu ni fahari maana zipo taasisi nyingi zinazofanya kazi ya ujenzi lakini kwa kipekee kwa kuchagua Jeshi la Kujenga Taifa kupitia SUMA JKT (Shirila la Uzalishaji Mali la JKT) wafanye kazi ya ujenzi wa Ikulu, mimi kwangu ni fahari," alisema.

Naye Msimamizi Mkuu wa Mradi huo, Meja Samwel Jambo, alisema ujenzi huo umetekelezwa kwa kufuata ubora na kuzingatia taratibu zote za ujenzi. Naye Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Daudi Kondoro, alisema kumekuwa na uzingatiaji wa upimaji wa vifaa vilivyotumika kwenye ujenzi ili kuwa na ubora unaotakiwa.

"Kwa kutambua Dodoma ni maeneo ya matetemeko nchini, vipimo vya tetemeko vimezingatiwa ili kama kutatokea tetemeko jengo letu liwe imara," alisema.

Mei 31, 2020, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, alizindua ujenzi wa Ikulu ya Chamwino huku akisema majengo sita yaliyounganishwa ya ofisi za ikulu yanajengwa na JKT katika eneo la Vikonje, Dodoma kwa usanifu na mwonekano sawa na Ofisi za Ikulu Dar es Salaam.

Magufuli alisema kutokana na umuhimu wa jengo hilo, hakuona umuhimu wa kufanya jambo hilo peke yake, hivyo aliwaomba marais wastaafu washirikiane kuweka jiwe la msingi.

"Mnamo Oktoba 10, 1973 Hayati Baba wa Taifa (Mwalimu Julius Nyerere), alitangaza uamuzi wa kujenga Ikulu jijini Dodoma pamoja na kujengwa kwa makazi ya Rais, nilipoingia madarakani, niliahidi kuhakikisha serikali inahamia Dodoma," alisema.

"Pamoja na ujenzi unaoendelea, tayari majengo matatu ya awali na ujenzi wa ukuta unaozunguka Ikulu vimeshakamilika, hakuna hata jengo moja la zamani litakalobomolewa," alisisitiza.



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Prof. Maurice Mbago (wa pili kushoto), akipata maelezo kuhusu ujenzi wa Shule ya Msingi ya mchepuo wa Kiingereza ya Msangalale, jijini Dodoma juzi, inayojengwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Elimu wa Taifa na kusimamiwa na TEA, kwa thamani ya Sh. milioni 750. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa TEA, Bahati Geuzye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watendaji waenguliwa ukusanyaji wa mapato

Na Augusta Njoji, DODOMA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Chemba mkoani Dodoma limejipanga kubadili mfumo wa ukusanyaji mapato kwa kuwatumia watu wa kawaida badala ya watendaji wa vijiji na kata.

Hatua hiyo inatokana na baadhi ya watendaji wa kata na vijiji kushindwa kuingiza fedha benki kwa wakati na kusababisha hoja za ukaguzi.

Akizungumzia kwenye baraza la robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Sambala Saidi, alisema suala la mapato kwa halmashauri hiyo limekuwa ni kikwazo kutokana na watendaji wanaokusanya.

"Wanakaa na fedha muda mrefu baada ya kukusanya hawapeleki benki kwa wakati na hii inatusababishia hoja za ukaguzi, wakati mwingine fedha zimekuwa zikiliwa na imekuwa ikituingiza kwenye hoja za ukaguzi kwa CAG (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) hadi mara ya mwisho kulikuwa hasara ya zaidi ya Sh. milioni 700, kutokana na watendaji kukaa na fedha,"alisema.

Pia alisema kikwazo kingine ni watendaji kutokuwa na utayari wa kukusanya mapato kama miongoni mwa majukumu yao.

"Sasa hili limekuwa likitusumbua sana kama halmashauri tunafikiria kuja na utaratibu mpya wa kukusanya mapato na moja ya utaratibu tunaofikiria ni kutafuta watu ambao si watendaji. Alisema ili halmashauri ijisimamie vizuri inapaswa kujiimarisha kwenye ukusanyaji wa mapato.

"Inapaswa kukusanya mapato kwa mujibu wa makadirio tuliyojiwekea lakini kusimamia matumizi ya mapato kwenda kwenye asilimia 40 ya miradi ya maendeleo na asilimia 10 ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu,"alisema.

Kuhusu usimamizi wa fedha kwenye miradi ya kimkakati, mwenyekiti huyo alisema Sh. milioni 470 zilitolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa sekondari ya Churuku.

# EWURA yabaini madudu mamlaka za maji

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imebaini upungufu kwenye mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira nchini hali inayokwamisha tathmini ya hali halisi ya utendaji na upatikanaji huduma.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Modestus Lumato, aliyasema hayo jana jijini hapo kwenye kikao kazi cha watendaji wa mamlaka za maji za mikoa na miradi ya kitaifa kilichoлenga kuhakiki taarifa za utendaji wa mamlaka hizo kwa mwaka 2021/22.

Mhandisi Lumato alitaja upungufu uliobainika kwenye tathmini iliyofanywa na EWURA kuwa ni kuwapo mamlaka za maji ambazo zimeendelea kuwasilisha taarifa zenye upungufu katika kukidhi viwango vya huduma, uchakavu, ufanisi wa makusanyo wa maduhuli.

Upungufu mwingine ni muda wa upatikanaji wa huduma, ubora wa maji pamoja na idadi ya wananchi wanaopata huduma, hali inayokwamisha kufanya tathmini ya hali halisi ya utendaji na upatikanaji huduma.

"Nitoe wito kwa mamlaka zote za maji kuhakikisha zinafanya masahihisho kwenye taarifa zenye mapungufu ili kutoa hali halisi ambayo mwisho wa siku itasaidia katika kupima utendaji na ufanisi wa huduma wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira," alisema.

Lumato alizisisitiza mamlaka hizo kuhakikisha zinatoa taarifa sahihi za huduma ya maji na usafi wa mazingira kwa wananchi ili kuimarisha upatikanaji wa huduma endelevu kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Naye Adam Ishara mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Maji, alizisihi kila mamlaka ya maji kujitahidi kutekeleza wajibu wake ikiwamo kuwa na takwimu sahihi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Alisema wizara ipo tayari kutoa miongozo na ushirikiano unaohitajika muda wowote.

Awali, Kaimu Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira ambaye ni Meneja Ufundi wa Maji na Usafi wa Mazingira EWURA, Titus Safari, alibainisha kuwa mchakato wa maandalizi ya ripoti ya utendaji wa mamlaka za maji ni shirikishi hivyo kila mamlaka itumie kikao hicho kuthibitisha usahihi wa taarifa zake.

Kikao hicho kilihudhuriwa na watendaji kutoka mamlaka 25 za majisafi na usafi wa mazingira za miji mikuu ya mikoa na mamlaka saba za miradi ya kitaifa.



# Kongamano lakutanisha washiriki 150

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KONGAMANO la udhibiti wa majitaka na usafi wa mazingira limewakutanisha washiriki 150 visiwani hapo kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

Akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano huo ulioanza jana hadi Novemba 18, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar (Zura), Omar Yussufu, alisema fursa hiyo ni ya kipekee kwa Zanzibar kuwa mwenyeji wa mkutano mkuu wa mwaka wa jumuiya ya udhibiti wa maji na usafi wa mazingira kusini na mashariki mwa Afrika.

Alisema kongamano hilo ni fursa ya kipekee na linaenda sambamba na juhudi za Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi za kuitangaza Zanzibar kutokana na mkutano kujumuisha nchi zote za Afrika.

**Sote ni mashuhuda juu ya miradi mikubwa ya maji serikali inayotekeleza nchini, haya maji tunayoyatoa kuwapelekea wananchi, wakishatumia yanakwenda wapi.**

Alisema lengo kuu la mkutano huo ni kuhakikisha mpango mkakati wa udhibiti wa maji yaliyotumika kutokana na tatizo la kuyadhibiti.

"Sote ni mashuhuda juu ya miradi mikubwa ya maji serikali inayotekeleza nchini, haya maji tunayoyatoa kuwapelekea wananchi, wakishatumia yanakwenda wapi," alihoji.

Alisema ili kuhakikisha miji inakua salama na safi ni lazima kudhibiti maji yaliyotumika yasisambae ovyo na kusababisha uchafuzi wa mazingira ambao utaleta athari ya maradhi.

Alisema mkutano huo utatoa fursa za kubadilishana mawazo jinsi ya taratibu zinazotakiwa kutumika katika kudhibiti usafi wa mazingira unaotokana na maji yaliyotumika.

"Mji wetu mkuu wa Zanzibar ni mmoja tu ambao ni mkongwe na ndio wenye mitaro maalum ya uhifadhi wa maji yaliotumika, lakini sehemu kubwa ya miji maji mengi yanapotea ovyo na hayana udhibiti," alisema.

Aidha, alisema matarajio baada ya mkutano huo ni kuona maji yaliotumika yanaleta tija katika matumizi mingine ikiwamo kutumika katika kilimo baada ya kudhibitiwa na kufanyiwa mchakato wa ajili ya kutumika na mazingira kuwa salama kimazingira.

Alisema mabadiliko ya tabianchi yameathiri upatikanaji wa maji Zanzibar kwa sababu mvua zimetoweka na kusababisha upungufu.

"Uhaba wa mvua umesababisha kiwango kidogo cha upatikanaji wa maji na sasa yanafuatwa katika kina cha mbali chini ya ardhi," alisema.

Naye Katibu Mtendaji wa Mamlaka Udhibiti wa Maji wa nchi za Kusini na Magharibi mwa nchi za Afrika (ESAWAS), Yvonne Magawa, alisema lengo la mkutano huo ni kuziunganisha mamlaka zote zinazoshughulikia udhibiti wa maji kwa kuhakikisha zinaweka mikakati ya kuwapatia wananchi huduma bora ya majisafi na salama.

Alisema mkutano huo ni wa kwanza unaozikutanisha nchi zote za bara la Afrika, umeweka mipango ya kuhakikisha wananchi wanapata majisafi na salama kwa bei nafuu.

Alisema wadhibiti wa maji wamejipanga ifikapo mwaka 2030 wanayafikia malengo endelevu ya dunia (SDG's) na wananchi kwa asilimia 100 wanapata huduma ya majisafi na salama ikiwamo vijijini.




Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar, Omar Yussuf (kulia), akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano wa udhibiti wa maji ulioanza jijini Zanzibar jana. Kushoto ni Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji wa Nchi za Kusini na Magharibi mwa nchi za Afrika (ESAWAS), Yvonne Magawa. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri aeleza umuhimu masomo stadi za maisha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein, amesema kuwapo kwa mwongozo wa ufundishaji wa masomo ya stadi za maisha ni muhimu ili kuwawezesha wanafunzi kujiepusha na majanga mbalimbali ikiwamo vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na mimba za utotoni.

Aliyasema hayo jana Shule ya Bububu, katika makabidhiano ya mwongozo wa ufundishaji wa masomo ya stadi za maisha yenye lengo la kuwajenga wanafunzi kufahamu viashiria hatari vya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema wanafunzi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni kikwazo katika kupiga hatua kubwa ya maendeleo ikiwamo sekta ya elimu.

Alisema kuwapo kwa mwongozo wa ufundishaji wa masomo hayo kutasaidia wanafunzi kufahamu viashiria mbalimbali ikiwamo mimba za utotoni ambazo ni kikwazo katika kuyafikia malengo yao ikiwamo sekta ya elimu.

"Mwongozo huo kwa kiasi kikubwa utasaidia na kuwawezesha walimu kufundisha masomo ambayo yatakwenda sambamba na mila na utamaduni wetu," alisema.

Mkurugenzi wa Elimu, Abdalla Mohamed Mussa, alisema mwongozo huo sasa utawezesha walimu kufundisha masomo hayo kwa mafanikio makubwa kwa kufuata misingi ya elimu na sheria pamoja na maadili.

Alisema bado wanafunzi wengi wanakabiliwa na changamoto za mimba za utotoni ambazo huzima ndoto zao za elimu ambapo sababu kubwa wanafunzi hawajaelimishwa na kuhafamu athari za matukio hayo.

"Mwongozo huu sasa unakwenda moja kwa moja kuwapatia nyenzo walimu juu ya ufundishaji wa masomo ya elimu na stadi za maisha katika kujiepusha na athari za tishio la mimba," alisema.

# Serikali kukusanya taarifa matukio udhalilishaji kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya imesema imejipanga kuimarisha vituo vya mkono kwa mkono kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa sahihi za matukio ya watu wanaofanyiwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hayo wakati akipokea vifaa vya ukusanyaji wa taarifa katika vituo vya mkono kwa mkono ikiwamo kompyuta vilivyotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Save Children Fund.

Alisema ukusanyaji wa taarifa katika vituo hivyo ni muhimu kwa kuwa utasaidia wizara kufahamu idadi kamili ya watu wanaofanyiwa vitendo vya udhalilishaji na kujua ukatili wa aina gani.

"Moja ya changamoto kubwa iliyokuwa ikitukabili katika vituo vya mkono kwa mkono ni tatizo la kupata taarifa kamili za matukio ya ukatili wa kijinsia zinazokusanywa na kuja katika vituo hivi," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Mipango wa Shirika la Save Children Fund, Jane Mbagi Mutua, alisema wamelenga kuvifikia jumla ya vituo saba vya mkono kwa mkono vilivyoko Unguja na Pemba ili kuviwezesha kukusanya takwimu sahihi za matukio ya ukatili wa kijinsia.

Alisema takwimu za matukio ya ukatili wa kijinsia ni muhimu katika vituo hivyo ambavyo wananchi hufika katika hatua ya kwanza kutoa taarifa mbalimbali za awali.

Alisema katika mwaka 2011 wamesaidia ukarabati wa kituo cha mkono kwa mkono katika Hospitali ya Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja na kutoa huduma za ukusanyaji wa takwimu kwa mafanikio.

"Tutaendelea kusaidia huduma za ukusanyaji wa takwimu katika vituo vya mkono kwa mkono ili kuona vinafikia malengo yao ya ukusanyaji wa takwimu halisi za matukio ya ukatili wa kijinsia," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Fatuma Mrisho, alisema wamejipanga kuwajengea uwezo watendaji wa sekta ya afya wanaofanya kazi katika vituo vya mkono kwa mkono ili kuwawezesha kufikia malengo ya ukusanyaji wa taarifa za matukio ya udhalilishaji wa kijinsia.

"Suala la ukusanyaji wa taarifa pamoja na kuwa na takwimu sahihi katika vituo vya mkono kwa mkono ni muhimu ambavyo vitatuwezesha kujua aina gani za ukatili wa kijinsia unaofanyika nchini," alisema.

Jumla ya vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 29 vimekabidhiwa kwa Wizara ya Afya kwa ajili ya vituo saba vya mkono kwa mkono ikiwamo kompyuta za kuhifadhi na ukusanyaji wa takwimu za matukio ya udhalilishaji wa kijinsia.





# Kulala usingizi kinga ya ugonjwa wa kisukari

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANANCHI wametakiwa kupumzisha mwili hasa nyakati za usiku na kupata muda mrefu wa kusinzia ili kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza kikiwamo kisukari.

Mwenyekiti wa Chama cha Kisukari Tanzania (TDA), Prof. Andrew Swai, alibainisha hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kisukari Duniani ambayo kitaifa yaliyofanyika Misungwi, mkoani Mwanza.

Alisema nyakati za usiku mtu anatakiwa kulala saa saba hadi nane ikiwa wakati wa usiku ndipo mwili ujitengenezea kinga, hivyo kuufanya mwili kuwa madhubuti katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza kikiwamo kisukari.

"Huduma ya matengenezo ya miwili kwetu sisi binadamu ni usiku. Wakati tumepumzika ndiyo inafanyika kwa sababu muda wa kupumzika una uhusiano mkubwa sana na kisukari. Kadri unavyopumzika ndivyo ambavyo mwili unajiweka kwenye nafasi ya kutumia hata vile ulivyokula na kuifanya sukari yako kukaa vizuri." Alisema.

**Jamii inapaswa kutotumia mafuta ya kupikia kwa wingi huku akisisitiza mtu anatakiwa kutumia vijiko vitano vya sukari na kijiko kimoja cha chumvi kwa siku.**

Kwa mujibu wa Prof. Swai, jamii inapaswa kutotumia mafuta ya kupikia kwa wingi huku akisisitiza mtu anatakiwa kutumia vijiko vitano vya sukari na kijiko kimoja cha chumvi kwa siku.

Naye Kaimu Meneja Mpango wa Taifa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza, Valeria Millinga, akieleza hali ya utoaji huduma za wagonjwa wa kisukari, alisema magonjwa yasiyoambukiza kikiwamo kisukari, huchangia asilimia 33 ya vifo nchini.

Pia alisema asilimia 9.1 ya watu wana ugonjwa wa kisukari kutokana na utafiti wa magonjwa yasiyoambukiza na viashiria vyake kwa mwaka 2012, katika nchi 10 zinazoongoza kwa ugonjwa wa kisukari barani Afrika, Tanzania inashika nafasi ya nane.

Alisema katika kuongeza uhamasishaji na uelewa kwa wananchi juu ya ugonjwa huo, wamefanya maadhimisho jijini Mwanza na kufikia siku ya kilele wananchi takribani waliopimwa 3,000 walikutwa na viashiria vya ugonjwa wa huo ni 34 tu.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau wake, imetoa mafunzo ya utoaji wa huduma ya magonjwa yasiyoambukiza ukiwamo wa kisukari kwa wahudumu wa afya 1,112 kati ya watoa huduma 2,600 wanaotakiwa kupata mafunzo hayo huku wakitarajia ifikapo mwishoni mwa mwaka 2023, wawe wametoa mafunzo hayo kwa watoa huduma katika vituo 600 nchini.

Kutokana na hali hiyo, aliwaomba wananchi kuendeleza kutekeleza maagizo wanayopewa na watoa huduma za afya ikiwamo kuzingatia ulaji unaofaa, mazoezi ya mwili ya kutosha, kudhibiti tabia bwete, kuepuka matumizi ya pombe kupita kiasi na kwa wanaotumia dawa wazifuatishe ipasavyo.



Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (wa pili kushoto), akikabidhi cheti cha shukrani kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Guy Williams (wa pili kulia), kwa udhamini wao wa Tuzo za Consumer Choice Africa, zilizofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yatoa agizo kuhusu baa la njaa

**Na Mohab Dominick,** SHINYANGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga, kimeitaka serikali kuangalia hali ya upatikanaji wa chakula kwa wananchi kwa kuwa hivi sasa baadhi ya kaya zinakula mlo mmoja kutokana na bei ya chakula kuwa juu.

Sambamba na hilo, pia chama kimewataka madiwani kuwa wakali watekelezapo majukumu katika maeneo yao ikiwa waliahidi kusimamia ilani ya chama na wao ndio watakaoulizwa waliyoahidi kwenye uchaguzi ujao.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Shinyanga, Edward Ngerela, alisema hayo juzi kwenye baraza la madiwani la robo ya kwanza ya mwaka lililofanyika kwenye ukumbi wa halmashauri hiyo hivi karibuni. Alisema madiwani wasipokuwa wakali wajiandae kuhukumiwa na wananchi ifikapo mwaka 2025.

"Chama Cha Mapinduzi kimewaamini katika maeneo yenu kusimamia ilani ambayo inaondoa changamoto na kero kwa wananchi. Kikubali kukaa kimya kwa kuogopa kuitwa wabaya kwa kutoisimamia halmashauri mpaka baadhi ya mambo yakaenda ndivyo sivyo, mtakuwa hamjakitendea haki chama," alisema.

"Tatizo la ukumbi leo miaka miwili fedha zinarudi kwa visingizio ambavyo havina maana wakati nyie mpo, watendaji na wataalamu wapo mmekaa tu bila kuchukua hatua. Mimi sijaridhika na majibu yaliyotolewa, chama kitawachukulia hatua kwani fedha zinakuja kazi wala jengo haliisha. Hapa katikati kuna nini ambacho kinasababisha haya?" alihoji.

Ngerela alimuunga mkono Diwani wa Isela Magazi, Isack Sengerema, kwa halmashauri kutotoa ahadi ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha polisi wakati wananchi wamejitolea kujenga boma zaidi ya Sh. milioni 10 na madiwani pamoja na halmashauri kwa

# Wakulima tumbaku wapewa somo ubora

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA 5,090 wa zao la tumbaku katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wamekumbushwa kulima kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo hicho ili kukabiliana na janga la ukame lililokithiri na kuhakikisha wanapata mavuno mengi na kufikia lengo la kilo milioni 17,000 katika msimu huu.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Hamisi Majogolo, alisema hayo jana wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii juu ya namna ambavyo wamejipanga kukabiliana na ukame na kuhakikisha mbolea zinawafikia wakulima kwa wakati ili wapate mavuno mengi.

Alisema ili kukabiliana na ukame unaotishia kutokupata mavuno mengi, ni bora kila mkulima kuhakikisha analima kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo hicho ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha maofisa ugani walioko kwenye maeneo yao.

Majogolo alizitaja kanuni ambazo wakulima wanatakiwa kufuata kuwa ni pamoja na kuandaa vitalu vya miche mapema, kulima na kupanda mwanzoni mwa mvua za kwanza, kupalilia na kuweka dawa ya kuua wadudu, kuvuna kwa kufuata mivuno, kukausha kwa kufuata dira na kuchambua na kufunga kwa kufuata mivuno ya tumbaku.

"Kukosekana kwa mvua za uhakika msimu huu kutasababisha wakulima kukosa tumbaku ya kutosha ukilinganisha na vipindi vingine. Lakini tumejipanga kuhakikisha uzalishaji haushuki na kufikia lengo la kupata kilo milioni 17,000 za tumbaku kwa kuwa tuna wanunuzi wa uhakika," alisema Majogolo.

**Ili kukabiliana na ukame unaotishia kutokupata mavuno mengi, ni bora kila mkulima kuhakikisha analima kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo hicho ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha maofisa ugani walioko kwenye maeneo yao.**

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani yatangaza zawadi atakayetoa taarifa za Al-Shabaab

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imesema itatoa zawadi ya hadi dola milioni 10 kwa yeyote ambaye atakuwa na taarifa kuhusu viongozi wakuu wa Al-Shabaab.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani jana ilieleza kuwa, kwa mara ya kwanza itatoa donge nono kwa mtu yeyote atakayetoa taarifa itakayowezesha kusaidia kutatiza mifumo ya kifedha ya kundi la Al-Shabab lenye mafungamano na Al-Qaeda.

Inaelezwa kuwa hivi karibuni wapiganaji wa Al-Shabab waliongeza mashambulizi katika mji mkuu wa Somalia, Mogadishu na maeneo mengine ya nchi hiyo kutokana na mashambulizi dhidi ya kundi hilo yanayofanywa na serikali mpya ya Rais Hassan Sheikh Mohamud.

Marekani ilisema donge hilo ni kwa kila mmoja atakaetoa taarifa zozote juu ya maficho ya kiongozi wa Al-Shabab Ahmed Diriye, naibu wake Mahad Karate na Jehada Mostafa, raia wa Marekani anayesemakana kuwa na majukumu mbalimbali katika kundi hilo.

Wizara hiyo pia inamhusisha Diriye na shambulio la mwaka 2020 katika kambi ya jeshi nchini Kenya, lililomuua mwanajeshi mmoja wa Marekani pamoja na wakandarasi wawili. Awali, Marekani ilitoa zawadi ya hadi dola milioni sita kwa yeyote mwenye taarifa kuhusu Diriye, ambaye pia anajulikana kama Abu Ubaidah.

Kwa mujibu wa bango lililotolewa na Marekani likiwa na picha za watatu hao, Washington ilisema viongozi hao wa Al-Shabaab wamehusika na mashambulizi mengi ya kigaidi nchini Somalia, Kenya na mataifa jirani na kusababisha vifo vya maelfu ya watu wakiwemo raia wa Marekani.

Naye Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) anayehusika na masuala ya haki za binadamu Volker Turk, alisema kuwa zaidi ya raia 600 wameuawa mwaka huu katika mashambulizi ambayo kwa kiasi kikubwa yamefanywa na Al-Shabaab.

Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni za UN, takriban watu 613 wameuawa na wengine 948 wamejeruhiwa mwaka huu, idadi hiyo ikiwa ni ya juu zaidi tangu mwaka 2017 ikiashiria ongezeko la asilimia 30 kutoka mwaka uliopita.

UN iliongeza kuwa, katika shambulio baya kuwahi kutokea katika muda wa miaka mitano, mashambulizi mawili ya mabomu yaliyodaiwa kufanywa na Al-Shabaab mnamo Oktoba 29 yaligharimu maisha ya watu 121 na kuwajeruhi wengine 333 mjini Mogadishu.

Kundi hilo, ambalo liliwekwa kwenye orodha ya makundi ya kigaidi na Marekani mwezi Machi mwaka 2008, limekuwa likipambana kuipindua serikali dhaifu inayoungwa mkono na mataifa ya Magharibi kwa takriban miaka 15.

Rais Hassan Sheikh Mohamud, aliyeingia madarakani mwezi Mei, aliahidi kupambana na kundi hilo, huku wanajeshi wa serikali wakionekana kupata mafanikio katika uwanja wa mapambano dhidi ya Al-Shabaab katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita, kwa kuchukua udhibiti wa maeneo yaliyokuwa mikononi mwa kundi hilo kwa muda mrefu.

Mnamo mwezi Mei, Rais wa Marekani Joe Biden aliamua kutuma tena wanajeshi wa Marekani nchini Somalia, akiidhinisha ombi kutoka wizara ya ulinzi ya nchi hiyo, Pentagon, ambayo iliuona mfumo wa kupokezana uliopendelewa na mtangulizi wake Donald Trump kuwa hatari na usiokuwa na faida.

Rais Donald Trump aliwaondoa wanajeshi hao mnamo Desemba 2020, na kuwaacha wakiingia na kutoka kwa kazi maalumu kutokea nchi jirani ya Kenya, hatua ambayo wataalam walielezea kuwa ya gharama kubwa na hatari.

***DW***



Wafanyakazi wa idara ya uokoaji wakiwa wamebeba mwili kufuatia shambulio la bomu lililotegwa ndani ya gari mjini Mogadishu, Somalia. **PICHA: RFI.**

# Mapigano makali yaendelea DRC

**KINSHASA, DRC**

WAKATI diplomasia ikifanya kazi ya kukomesha uhasama mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), mapigano kati ya waasi wa FARC na waasi wa M23 yameanza tena mwanzoni mwa wiki hii.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na RFI, kumekuwa na mapigano ya siku tano mfululizo kati ya wanajeshi wa Congo na waasi wa M23, tangu kuanza kwa mashambulizi makubwa yaliyoanzishwa na jeshi la DRC (FARDC) katika kujaribu kurejesha baadhi ya ngome walizopoteza hapo awali na ambazo zinashikiliwa na waasi hao.

Kwa mujibu wa vyanzo vya kiraia na waandishi wa habari wa Goma, askari wa Congo walifanikiwa kusimamisha kasi ya waasi wa M23 kuelekea mji mkuu wa mkoa wa Kivu Kaskazini tangu mwishoni mwa wiki iliyopita, baada ya kurudi nyuma kwa kilomita zaidi ya 10.

Vile vile vyanzo hivyo vilieleza kuwa, mapigano makali yamefika katika eneo la Nyiragongo, huku ongezeko la wimbi kubwa la wakimbizi likishuhudiwa katika jiji la Goma, na kwamba miji ya Rutshuru-centre na Kiwanja bado iko chini ya udhibiti wa waasi wa M23.

Kwa sasa, jeshi la Congo halijatoa ripoti yoyote ya mapigano hayo, wakati upande wa M23, wakidai kuharibu vifaru vinne vya kivita vya T55.

***RFI***

## Afunguliwa mashtaka kwa kuiba taarifa

**OTTAWA, Canada**

POLISI wa Canada wamemfungulia mashtaka ya uhaini mfanyakazi wa kampuni moja ya Hydro-Quebec, ya Canada, baada ya kudaiwa kutuma siri za biashara kwenda China.

Kwa mujibu wa VOA, mfanyabiashara huyo aliyetambulioka kwa jina la Yuesheng Wang (35), amefikishwa mahakamani katika mji wa Quebec, na kukabiliana na mashitaka ya kuiba siri za kibiashara.

Inaelezwa kuwa alifanya kitendo hicho kwa kutumia kompyuta bila ya kupata ruhusa na kufanya udanganyifu na kutosimamia uaminifu wa utumishi wa umma.

Inspekta wa polisi wa eneo hilo David Beaudoin, alisema kikosi cha usalama wa taifa kilianza kuchunguza shauri hilo toka mwezi Agosti mwaka huu, baada ya kupokea malalamiko kutoka tawi la shirika la Hydro-Quebec.

Aliongeza kwamba alichukuwa taarifa ili kuinufaisha Jamhuri ya watu wa China ili kupata taarifa za maslahi ya uchumi wa Canada.

**VOA**

## Watumishi 3,000 wafutwa kazi Kenya

**NAIROBI, Kenya**

GAVANA wa kaunti ya Garissa Kaskazimi Mashariki mwa Kenya Nathif Jama, ameamuru kuondolewa kwa zaidi ya wafanyakazi hewa 3,000 kwenye orodha ya malipo, baada ya kubainika kuwa wanalipwa kinyume na taratibu.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya nchini humo, majina ya watu hao yaligunduliwa baada ya kufanyika kwa ukaguzi wa rasilimali watu siku chache zilizopita.

Uchunguzi huo pia uligundua kuwa wakurugenzi wengi na manaibu wao waliajiriwa kuwa wakuu wa idara bila kuwa na shahada za vyuo vikuu.

Pia ilibainishwa kuwa takriban madereva 100 waliajiriwa ilhali kaunti hiyo ina magari 12 pekee katika idara yake ya uchukuzi.

Gavana Nathif Jama, alisema kuna jopo lililoteuliwa kushughulika na kesi za wale wanaodai kufutwa kazi kwa njia isiyo halali.


**BBC**

BURUDANI



## HARMONIZE ATAKA HESHIMA YAKE

**Na Mwandishi Wetu**



MSANII wa Bongo Fleva anayekimbiza kwa sasa, Harmonize, ameibuka na kutaka apewe sasa heshima yake.

Amesema huu ndio wakati wa kupewa heshima na kutambulika kutokana na vitu vikubwa anavyovifanya kwenye muziki.

Harmonize amesema anataka azungumziwe sasa na si akifa ndio watu waanze kumzungumzia kama mkali wa Bongo Muvi, Steven Kanumba, aliyetangulia mbele za haki.

Kupitia ukurasa wa Instagram, bosi huyo wa Lebo ya Kondegang, ameandika: "Kwa hiyo siku nikifa mtanizungumzia kama mnavyomzungumzia marehemu Kanumba?

"Nipeni heshima yangu acheni kufichaficha, hakuna hata mmoja anaweza kufanya kwa level [kiwango] hii."

## BURNABOY AMBWAGA ZUCHU TUZO MTV EMA



**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa Nigeria, Burnaboy, ameshinda tuzo ya MTV EMA.

Msanii hyuo ameshinda katika kipengele cha Best African Act.

Katika kipengele hicho Burnaboy alikuwa akishindana na msanii kutoka Tanzania, Zuchu.

Ni hatua kubwa sana kwa msanii kama Zuchu kuingia kwenye kipengele cha Best African Act licha ya kuikosa tuzo hiyo.

Llicha ya kuikosa tuzo hiyo, Zuchu anajivunia hatua kubwa aliyopiga na ukizingatia msanii aliyeshindana naye ni anayetajwa kuwa namba moja Afrika.

# RAYVANNY AMSHUKURU DIAMOND

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Rayvanny, amemmwagia sifa bosi wake wa zamani, Diamond Platnumz kuwa ndiye aliyempa maisha kimuziki.

Ikumbukwe Rayvanny kwa sasa amejitoa kwenye Lebo ya Wasafi inayomilikiwa na Diamond akiwa kivyake.

Kupitia wimbo wake wa Nitongoze, Rayvann ameelezea namna alivyotoka kimaisha na muziki kupitia Tandale, akimaanisha kwa Diamond.

Rayvanny ametoa shukrani hizo Kwa Diamond baada ya kusema bila yeye asingekuwapo.

Akaongeza si Rayvanny pekee, wengi wamepita huku.

HABARI MICHEZO

# MABALOZI WALAANI UPOTOSHAJI KOMBE LA DUNIA QATAR 2022

**Na Sabato Kasika**

BARAZA la mabalozi wa nchi za Kiarabu nchini, limelaani kampeni za kile ambacho linakiita upotoshwaji dhidi ya nchi ya Qatar zinazolenga kuonyesha kuwa nchi hiyo haifai kuandaa Fainali za Kombe la Dunia 2022.

Fainali hizo zinatarajiwa kuanza Jumapili wiki hii, Qatar ikiwa mwenyeji wa mashindano hayo makubwa zaidi ya soka ambayo hufuatiliwa na mashabiki wa soka kote duniani.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Katibu Mkuu wa baraza hilo ambaye pia ni Balozi wa Palestina hapa nchini, Hamdi Mansour AbuAli, alisema baraza hilo linafuatilia juhudi ambazo nchi hiyo imefanya ili kuwa mwenyeji wa tukio hilo kubwa zaidi la kimichezo duniani.

"Wakati Qatar inajiandaa kuzindua toleo la 2022 la Kombe la Dunia, sisi tunafuatilia kampeni za upotoshaji na kashfa ambazo nchi hiyo imekuwa ikikabiliana nazo, zinazolenga kuidhoofisha," alisema AbuAli.

Alisema nchi ya Qatar kuwa mwenyeji wa Kombe la Dunia ni kielelezo cha kihistoria na mafanikio makubwa kwenye michezo na kwamba wanaichukulia kama jukwaa la kimataifa lenye ushawishi mkubwa, kwa kuwa nchi hiyo inaendelea kufanya juhudi kubwa ili ipendeze na kuwa mahali ambapo watu wanatazamia kufika kufurahia soka.

"Tunaamini michuano ya Kombe la Dunia itaacha kumbukumbu kwa vizazi vilivyopo na vijavyo nchini humo, hivyo vyombo vya habari vya kimataifa visivyoitakia mema Qatar viache kufanya hivyo," alisema.

Alisema kampeni za kuidhoofisha Qatar zinalenga kuichafua nchi hiyo ya Kiarabu na Mashariki ya Kati ili mwisho wa siku ionekane haikufaa kuandaa mashindano, katika dunia ya mpira wa miguu

"Sisi mabalozi wa nchi za Kiarabu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa pamoja, tunalaani kampeni hizi za upotoshaji, na zenye uchochezi na chuki zinazoelekezwa kwa nchi ya Qatar," alisema.

Alisema wanaunga mkono kikamilifu juhudi za nchi hiyo ambazo wanaamini zitapambana na kampeni za upotoshaji na kashfa kwa kuwasilisha toleo maalum la Kombe la Dunia.




Mkurugenzi wa Wateja Binafsi na Wateja Wadogo Benki ya NBC, Elibariki Masuke, akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 15 kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Gofu Iringa, kwa Mkuu wa Mkoa huo, Halima Dendego. Kushoto ni Edmund Mkwawa, ambaye ni Mwenyekiti wa Mkwawa University Golf Club. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# NBC yatoa mamilioni ujenzi Uwanja wa Gofu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imeidhamini Klabu ya Gofu ya Chuo Kikuu cha Mkwawa (Mkwawa University Golf Club), Sh. milioni 15 , kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa mchezo huo ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali na mkoa wa Iringa kwa ujumla katika kutangaza Utalii wa Kusini.

Utalii wa Kusini maarufu 'Utalii Karibu Kusini', maadhimisho yake yalifungwa jana katika viwanja vya Kihesa, Kilolo mkoani humo.

Akizungumza baada ya kupokea hundi ya Sh. milioni 15 kutoka kwa Mkurugenzi wa Wateja Binafsi na Wateja Wadogo Benki ya NBC, Elibariki Masuke, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, aliipongeza Benki ya NBC kwa jinsi inavyojitoa katika kuunga mkono masuala mbalimbali ya kijamii pamoja na michezo.

"Hakika Benki ya NBC tunajivunia sana uwapo wenu , asante sana kwa jitihada zenu katika kukuza sekta ya michezo nchini, lakini pia kwa umuhimu mkubwa niwashukuru sana kwa kuiunga mkono klabu yetu ya gofu ya Mkwawa University Golf Club. Asanteni sana, kianzio hicho kitasaidia sana katika kuendeleza mchezo wa gofu hapa Iringa na moja kwa moja kutengeneza fursa zaidi za utalii," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Wateja Binafsi na Wateja Wadogo wa NBC, Masuke, alisema benki hiyo inapenda kuunga mkono sekta ya michezo hapa nchini.

"Kama mnavyojua sisi ni wadhamini wakuu wa Ligi ya mpira wa miguu maarufu kama NBC Premier League, lakini tumekua tukiendesha mashindano ya Marathon maarufu NBC Dodoma Marathon, ambapo fedha zinazopatikana katika mashindano hayo ya mbio huenda moja kwa moja kuwasaidia akina mama wenye matatizo ya kansa ya kizazi, kwa hiyo tupo hapa kujumuika na wana Iringa hasa katika tamasha hili kubwa lililofungwa leo (jana) Tamasha la " Karibu Utalii Kusini, " alisema.

Alisema tamasha hilo limehusisha watu mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi na NBC imekuja kama wadhamini wa Uwanja wa Gofu, ambapo wanaamini ukiwapo mkoani humo utavutia watalii zaidi na zaidi kwa watapata sehemu nzuri ya kujiburudisha baada ya kumaliza shughuli zao mbalimbali hifadhini.

Mwenyekiti wa Mkwawa University Golf Club , Yohannes Chavala, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, aliipongeza NBC kwa mchango wao wa Sh. milioni 15 , na kuongeza kuwa ujenzi wa uwanja huo utavutia watalii wengi na kukuza Utalii wa Kusini na Tanzania kwa ujumla.

## Wapinzani Simba, Yanga makundi leo

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wawili kwenye michuano ya kimataifa, Simba na Yanga, leo wanatarajia kuwafahamu wapinzani watakaokwenda kucheza nao kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho hatua ya makundi.

Droo ya makundi inatarajiwa kupangwa leo saa saba mchana kwa saa za Afrika Mashariki kwenye Makao Makuu wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), jijini Cairo, Misri ambapo mashabiki wa soka Afrika, hususan Tanzania wamekuwa wakiisubiri kwa hamu baada ya timu kubwa na kongwe nchini zote kutinga hatua hiyo.

Simba ambayo itaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, itapangwa kwenye moja ya makundi manne, ikiwa pot namba tatu na timu za CR Belouzidad na JS Kabylie zote za Algeria pamoja na Al Hilal ya Sudan ambazo haitakutana nazo.

Timu ambazo Simba inaweza kukutana nazo ni Al Ahly ya Misri, Wydad Casablanca na Raja Casablanca zote za Morocco, na Esperance ya Tunisia ambazo zipo pot namba moja, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Zamalek ya Misri, Petro de Luanda ya Angola na Horoya ya Guinea ambazo zipo kwenye pot namba mbili, huku pot namba nne ikiwa na timu za AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Coton Sport ya Cameroon, Al Merrikh ya Sudan na Vipers ya Uganda.

Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga ambayo ipo kwenye Kombe la Shirikisho imewekwa kwenye pot namba mbili na timu za Motema Pembe ya DR Congo, Asfar ya Morocco ambazo hawezi kukutana nazo kwenye hatua hiyo, lakini ina uwezekano na kupangwa na timu za TP Mazembe ya DR Congo, Pyramids ya Misri, ASEC Mimosas ya Ivory Coast, USM Alger ya Algeria, zilizopo Pot namba moja, St Eloi Lupopo ya Congo DR, Al Akhdar ya Libya, Real Bamako ya Mali, na River United ya Nigeria pot namba tatu, pamoja na Diables Noirs ya Congo Brazavvile, Future ya Misri, Marumo Gallants ya Afrika Kusini na ASKO Kara ya Togo.

## ZISIKUPITE

### RONALDO KUTEMWA UNITED

MANCHESTER United inaweza kufikiria kuvunja mkataba wa fowadi wa Ureno, Cristiano Ronaldo, kutokana na mahojiano yake na Piers Morgan, lakini watasubiri hadi watakaposikia mahojiano kamili kabla ya kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37. ***(Telegraph)***

### CHELSEA YAMSIKILIZIA CR7

CRISTIANO Ronaldo anaweza kwenda Chelsea baada ya fowadi huyo kuhusishwa na kuhamia Stamford Bridge majira ya joto, lakini iliripotiwa kuzuiwa na kocha wa wakati huo, Thomas Tuchel. ***(CBS via Express)***

### MUDRYK KWA ARSENAL, UTD

KLABU ya Manchester United imeungana na Arsenal kumsaka winga wa Shakhtar Donetsk na Ukraine, Mykhaylo Mudryk, huku Kocha wa United, Erik ten Hag, akisemekana kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, tangu akiinoa Ajax. ***(Sun)***

### ARTETA, MUDRYK KUTETA

MCHEZAJI Mykhaylo Mudryk amesema anataka kuzungumza na Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, kabla ya kuamua kuhusu mustakabali wake. ***(Vlada Sedan via Metro)***

### MOLEIRO AWANIWA LIVER

LIVERPOOL wanavutiwa na Kiungo wa Las Palmas, Alberto Moleiro, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, pia akidaiwa kulengwa na Barcelona na Manchester City. ***(Express)***

### ROMA KUMUUZA ABRAHAM

AS Roma inaweza kusikiliza ofa kwa mshambuliaji wa England, Tammy Abraham, 25. ***(Calciomercato)***

### SPURS NA MASKAUTI

KLABU ya Tottenham Hotspur ilituma maskauti kumtazama mshambuliaji wa Ufaransa, Marcus Thuram, mwenye umri wa miaka 25, kutoka Borussia Monchengladbach na mshambuliaji wa Cameroon, Youssoufa Moukoko mwenye miaka 19 wa Borussia Dortmund, kwenye mechi ya Ijumaa ya Bundesliga kati ya pande hizo mbili. ***(90 min)***

### THURAM LULU LIVER, ARSENAL

LIVERPOOL na Arsenal pia zinamtaka Marcus Thuram wa Borussia Monchengladbach. Mfaransa huyo anamaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu na amekuwa akihusishwa na Bayern Munich. ***(90 Min )***

### NKUNKU SAFI CHELSEA

CHELSEA ina imani kuwa imefanikiwa kufikia makubaliano na mshambuliaji wa RB Leipzig, Christopher Nkunku na kwamba Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 25 atajiunga nao Januari. ***(90 Min)***

### SILVA KUFUNGWA CITY

KLABU ya Manchester City inapanga mazungumzo na wakala wa kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva, wakati wa Kombe la Dunia ili kuamua mpango wa maisha yake ya baadaye. Mabingwa hao wa Ligi Kuu England wanafahamu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, anataka kujiunga na Barcelona na hawatamzuia iwapo ofa sahihi itatolewa. ***(Mundo Deportivo)***

### DRAMEH ATENGWA LEEDS

MLINZI wa kulia wa Leeds United, Cody Drameh, mwenye umri wa miaka 20, anavutiwa na Newcastle United, pamoja na Lille, Borussia Dortmund na Bayer Leverkusen. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HAZARD, NACHO WOTE WAWINDWA ASTON VILLA

**Nyota hao wataruhusiwa kuondoka Real Madrid katika dirisha la majira ya baridi, huku...**

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Aston Villa, Unai Emery, anawafukuzia wachezaji wawili wa Real Madrid, Eden Hazard na Nacho Fernandez, ili aweze kuwanunua katika dirisha dogo la Januari, kwa mujibu wa 90min.

Kocha huyo ameanza vema tangu kuchukua nafasi ya Steven Gerrard hapo Villa Park baada ya kupata ushindi mara mbili mfululizo kwenye Ligi Kuu England dhidi ya Manchester United na Brighton.

Emery ana nia ya kuongeza ubora kwenye kikosi chake huku ripoti kutoka nchini Hispania zikipendekeza Hazard na Nacho wote wataruhusiwa kuondoka 'Los Blancos' katika dirisha la majira ya baridi.

Hazard mwenye miaka 31 na ambaye alifanya vizuri akiwa na Chelsea, hajawahi kuonekana kufurahia katika mji mkuu wa Hispania na kiwango chake cha kudhoofisha kimemfanya akose namba ndani ya kikosi cha Kocha Carlo Ancelotti.

Mbelgiji huyo alisajiliwa kwa ada ya awali ya pauni milioni 89 pamoja na nyongeza, anaweza kupatikana kwa pauni milioni 22.

Villa walifanikiwa kumaliza dili kama hilo kwa mchezaji wa Barcelona, Philippe Coutinho, lakini watalazimika kuzuia nia ya klabu kama Newcastle United ambayo nayo inamtaka Hazard.

Nacho mwenye miaka 32, mkataba wake unamalizika msimu wa majira ya joto na pia anaripotiwa kupatikana kwa ada iliyopunguzwa.

Beki huyo mahiri ametumia miaka 21 Santiago Bernabeu tangu ajiunge na akademi ya klabu hiyo akiwa na umri wa miaka 11.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,051,2

MECHI KALI

SIMBA
VERSUS
NAMUNGO

1 | 1.30
X | 4.56
2 | 8.93

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DADA AJITOSA SAKATA LA RONALDO NA UNITED



**LOSBON, Ureno**

DADA wa Cristiano Ronaldo, amechapisha mfululizo wa jumbe za kumuunga mkono kaka yake akidai "ukweli lazima umesemwa".

Ronaldo alifanya mahojiano ya kipekee na Piers Morgan ambapo alimkashifu Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag na uongozi wa klabu hiyo, akidai kuwa "anadharauliwa na kusalitiwa" na walijaribu kumtoa kwa nguvu.

Huenda ikaashiria mwisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 pale Old Trafford, wakati huu akielekea Kombe la Dunia akiwa na Ureno.

Morgan pia alifichua kwamba ni Ronaldo ndiye aliyeomba kufanya mahojiano hayo ili kuweka hisia zake hadharani kabla ya kuelekea Qatar.

Dada wa Ronaldo, Elma Aveiro, naye akajitosa kutoa maoni yake juu ya hali ya kaka yake na alitumia mtandao wa kijamii wa Instagram.

Chapisho la kwanza aliandika: "Siko kimya juu ya milango ambayo sitaifungua tena kwa kiburi, lakini zaidi kwa kujiheshimu."

Kisha aliweka picha ya Ronaldo na Morgan wakiwa pamoja na akaandika: "Siku zote nitajivunia wewe mtu wangu."

Halafu akaweka video fupi kutoka kwenye mahojiano na kumwita Ronaldo "kiburi kikubwa zaidi cha maisha yangu."

Aveiro kisha akatoa habari kuhusu jinsi kaka yake Ronaldo anahisi kuchukizwa na Ten Hag na akaandika: "Ukweli unasemwa."

# Van Dijk tabu na Nunez




**LIVERPOOL, England**

MLINZI wa kati wa Liverpool, Virgil van Dijk amesema Liverpool "haijawahi kutilia shaka" ubora wa Darwin Nunez kufuatia kuimarika kwa mshambuliaji huyo hivi karibuni baada ya kuwa na mashaka mengi juu yake.

Nunez alikuwa na mwanzo mbaya wa maisha pale Anfield kufuatia uhamisho wake wa fedha nyingi kutoka Benfica, akipokea kadi nyekundu dhidi ya Crystal Palace katika mechi yake ya tatu pekee chini ya Jurgen Klopp.

Hata hivyo, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uruguay, ameanza kupiga hatua katika soka la Uingereza ambapo alitupia mabao mawili katika ushindi wa mabao 3-1 Jumamosi dhidi ya Southampton.

Na Van Dijk sasa anaamini ubora wake uko wazi na atakuwa na wakati mzuri zaidi baada ya Kombe la Dunia.

Ikumbukwe ligi tano kubwa Ulaya zimesimama kupisha michuano ya Kombe la Dunia inayoanza Jumapili wiki hii.

Van Dijk alisema kuwa Nunez ana sifa zote kwa mshambuliaji wa kisasa na kuna sababu ya yeye kununuliwa na anakomaa huku akiwa mvumilivu.

"Inachukua muda. Ni timu mpya, mazingira mapya, nchi mpya, lugha mpya, hivyo ni kawaida kabisa kwake kuchukua muda kidogo zaidi kutulia, lakini hakuna shaka sifa zipo, na malengo yatafuata," alisema Van Dijk.

Van Dijk pia alimwagia sifa kwa mlinda mlango Alisson, ambaye aliokoa michomo iliyokuwa inalenga lango lao walipokuwa wakicheza dhidi ya Southampton wakati wa ushindi wa Anfield.

Nahodha huyo wa Uholanzi pia aliangazia tabia ya Roberto Firmino, huku mshambuliaji huyo akifungua ukurasa wa mabao dhidi ya Saints hao baada ya kuachwa nje ya kikosi cha Brazil kitakachoshiriki Kombe la Dunia nchini Qatar.

07,683/-

# NBC YAPANIA KUBORESHA LIGI KUU, KUGAWA MABASI

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), ambao ni wadhamini Wakuu wa Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara, 'NBC Premiere League', imesisitiza dhamira yake ya kuboresha zaidi ligi hiyo kwa kuendelea kuziwezesha timu zinazoshiriki ili ziweze kujijengea uwezo wa kujitegemea.

Dhamira hiyo imesisitizwa na Mkurugenzi wa Fedha wa benki hiyo, Waziri Barnabas, mapema jana wakati akizungumza na washiriki wa Mkutano Mkuu wa kawaida wa 17 wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), uliofanyika jijini Mwanza.

"Kimsingi ni kwamba sisi kama wadhamini, tunajivunia sana kuona ligi yenye ushindani na viwango bora vya kiuchezaji vinavyoendelea kuonekana kwenye ligi hii. Hii inatokana na timu zinazoshiriki kuweza kusajili wachezaji wazuri kutoka ndani na nje ya nchi sambamba na kuweza kuwahudumia vema ikiwamo kuwapatia maslahi yao," alisema.

Kwa mujibu wa Barnabas, mbali na udhamini wa ligi hiyo benki hiyo imebuni mikakati mbalimbali inayolenga kufanikisha dhamira hiyo muhimu ikiwamo mikopo ya mabasi kwa klabu mbalimbali zinazoshiriki ligi hiyo ili kuzirahisishia usafiri.

"Ligi hii inahusisha suala zima la usafiri kwa klabu husika na wakati mwingine timu zinasafiri kwa umbali mrefu sana, hivyo kusababisha uchovu kwa wachezaji. Upatikanaji wa mabasi mazuri ya kisasa utasaidia kupunguza uchovu kwa wachezaji ili waweze kuleta ushindani unaohitajika wakiwa viwanjani. Tupo kwenye hatua nzuri na hivi karibuni baadhi ya timu zitapatiwa mabasi yao," alisema.

Barnabas alitaja huduma nyingine kuwa ni pamoja na utoaji wa bima kwa wachezaji, benchi la ufundi na familia za wachezaji wote wa ligi hiyo.

Aidha, aliwaomba wadau hao wa michezo zikiwamo klabu, viongozi wa mchezo huo na wachezaji mmoja mmoja, kuhakikisha wanachangamkia fursa ya kuwekeza kwenye Hati Fungani ya NBC Twiga Bond ili waweze kunufaika na faida mbalimbali zitokazo na hati fungani hiyo.



Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya NBC, Waziri Barnabas (wa tatu kulia), akiwa pamoja na viongozi waandamizi wa mchezo wa soka nchini, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), Wallace Karia (wa tatu kushoto), wakati wa mkutano mkuu wa kawaida wa 17 wa shirikisho hilo uliofanyika jijini Mwanza jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Singida Big Stars yapania kuvunja

INATOKA UK. 32

Licha ya kucheza mechi pungufu tofauti na timu nyingine za ligi hiyo, Yanga ipo kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi 23 baada ya kushuka dimbani mara tisa na haijapoteza mechi yoyote tangu msimu uliopita hadi sasa.

# SIMBA, NAMUNGO

INATOKA UK. 32

wakitokea kuuguza majeraha.

Naye mwakilishi wa wachezaji kipa namba tatu wa Simba, Ally Salim, alisema: "Walimu wametoa maelekezo yao na sasa kazi kubwa imebaki kwetu wachezaji kwa ajili ya kusaka pointi tatu, msimu huu tunapambana kila liwezekano kupata matokeo chanya ili kufikia malengo yetu ya kutwaa ubingwa."

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Shadrack Nsajigwa, alisema wako tayari kushindana na Simba katika mchezo wa leo.

"Tumepata muda wa kujiandaa vizuri na tuko tayari katika mchezo wa kesho (leo), tunatambua Simba ni timu ya aina gani, lakini maandalizi yako vizuri kwa ajili ya kufuta matokeo mabaya tunayoyapata tunapokutana na Simba.

"Mechi ya kesho (leo) ni tofauti sana na michezo tuliyocheza kwa sababu ya ukubwa na ubora wa wachezaji wa Simba," alisema Nsajigwa. Nahodha wa Namungo FC, Hamisi Mgunya, alisema, "Tumefanya maandalizi mazuri na benchi la ufundi limefanya kazi na kikubwa kilichobaki kwetu ni kufanya vizuri na kupambana kupata pointi tatu dhidi ya Simba".


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/11/22 | 18:00 | Fleetwood Town vs Bolton Wanderers | 3.05 | 3.35 | 2.24 |
| 02. 19/11/22 | 18:00 | Burton Albion vs Plymouth Argyle | 2.65 | 3.40 | 2.50 |
| 03. 19/11/22 | 18:00 | Port Vale vs Charlton Athletic | 2.33 | 3.35 | 2.90 |
| 04. 19/11/22 | 18:00 | Cambridge United vs Accrington Stanley | 2.40 | 3.35 | 2.80 |
| 05. 19/11/22 | 18:00 | Colchester United vs Doncaster Rovers | 2.27 | 3.25 | 3.10 |
| 06. 19/11/22 | 18:00 | Grimsby Town vs Stevenage FC | 3.00 | 3.25 | 2.32 |
| 07. 19/11/22 | 18:00 | Cove Rangers FC vs Greenock Morton FC | 2.55 | 3.35 | 2.60 |
| 08. 19/11/22 | 18:00 | Inverness Caledonian Thistle FC vs Ayr United FC | 2.90 | 3.45 | 2.31 |
| 09. 19/11/22 | 18:00 | Queen of The South FC vs Montrose FC | 2.48 | 3.40 | 2.70 |
| 10. 19/11/22 | 18:00 | Albion Rovers FC vs Stranraer FC | 2.38 | 3.40 | 2.80 |
| 11. 19/11/22 | 18:00 | Annan Athletic FC vs Elgin City FC | 2.31 | 3.40 | 2.90 |
| 12. 19/11/22 | 18:15 | SD Ponferradina vs Real Oviedo | 2.55 | 3.05 | 2.85 |
| 13. 19/11/22 | 20:30 | Sporting Gijon vs CD Leganes | 2.28 | 3.05 | 3.30 |
| 14. 19/11/22 | 22:00 | MVV Maastricht vs Almere City FC | 2.60 | 3.60 | 2.45 |
| 15. 20/11/22 | 19:00 | Sakaryaspor vs Bandirmaspor | 2.80 | 3.30 | 2.45 |
| 16. 20/11/22 | 19:00 | Qatar vs Ecuador | 3.30 | 3.10 | 2.26 |
| 17. 20/11/22 | 21:00 | Racing Santander vs Burgos CF | 2.30 | 2.95 | 3.40 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 16/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2252 | Mtibwa Sugar vs Coastal Union | 2.20 | 2.72 | 3.59 |
| 14:30 | 4612 | Preah Khan Reach Svay Rieng FC vs Phnom Penh | 2.09 | 3.59 | 2.91 |
| 15:00 | 3436 | Saudi Arabia vs Croatia | 6.88 | 4.05 | 1.50 |
| 16:00 | 1761 | Kabwe Warriors vs Buildcon | 1.86 | 2.86 | 4.66 |
| 16:00 | 2215 | Uzbekistan vs Kazakhstan | 1.90 | 3.38 | 4.23 |
| 16:00 | 3190 | Zesco United vs Green Buffaloes | 1.93 | 2.91 | 4.18 |
| 16:00 | 3695 | Napsa Stars vs Chambishi FC | 1.70 | 2.92 | 5.84 |
| 16:00 | 3721 | Tanzania Prisons vs Geita Gold FC | 2.90 | 2.70 | 2.80 |
| 16:00 | 5236 | Nkwazi vs Prison Leopards | 2.25 | 2.63 | 3.61 |
| 16:00 | 5741 | Green Eagles vs Nkana FC | 2.28 | 2.53 | 3.75 |
| 16:00 | 5823 | FC Muza vs Red Arrows | 3.89 | 2.72 | 2.10 |
| 16:00 | 5940 | Power Dynamos vs Nchanga Rangers | 1.62 | 3.12 | 6.23 |
| 16:30 | 4789 | Alessandria vs Renate | 3.26 | 3.11 | 2.12 |
| 16:30 | 5979 | Padova vs Gubbio | 2.28 | 2.93 | 3.12 |
| 17:00 | 2493 | Shabab AL Amari vs Jabal EL Mokaber | 7.41 | 4.87 | 1.32 |
| 17:00 | 3671 | Shabab Al Dhahiriya vs Thagafi Tulkarem | 2.15 | 3.20 | 3.11 |
| 17:00 | 5744 | Islami Qalqilya vs Shabab AL Khaleel | 9.75 | 5.46 | 1.23 |
| 17:00 | 5956 | Viterbo Calcio vs Pontedera | 2.23 | 2.97 | 3.17 |
| 18:30 | 5467 | United Arab Emirates vs Argentina | 20.19 | 7.47 | 1.14 |
| 19:00 | 1400 | Catanzaro vs Avellino | 1.35 | 4.47 | 7.38 |
| 19:00 | 1843 | Simba vs Namungo | 1.30 | 4.56 | 8.93 |
| 20:00 | 1274 | Rimini vs Vicenza | 2.30 | 3.21 | 2.82 |
| 20:00 | 1293 | Oman vs Germany | 23.10 | 8.26 | 1.12 |
| 20:00 | 1542 | Latvia vs Estonia | 2.24 | 3.11 | 3.02 |
| 20:00 | 1757 | Turkey vs Scotland | 2.07 | 3.28 | 3.68 |
| 20:00 | 1892 | Andorra vs Austria | 40.31 | 11.09 | 1.06 |
| 20:00 | 1921 | Kosovo vs Armenia | 1.83 | 3.54 | 4.34 |
| 20:00 | 3555 | Sandefjord vs Kongsvinger IL | 1.90 | 3.60 | 3.80 |
| 20:00 | 3719 | Moldova vs Azerbaijan | 2.86 | 3.22 | 2.50 |
| 20:00 | 3837 | Poland vs Chile | 2.17 | 3.13 | 3.58 |
| 20:00 | 5280 | Czech Republic vs Faroe Islands | 1.12 | 8.04 | 25.14 |
| 21:00 | 3084 | Charlottenburger FC Hertha 06 vs SpVgg Blau-Weiss 1890 Berlin | 2.39 | 3.85 | 2.55 |
| 21:00 | 3833 | Cyprus vs Bulgaria | 2.97 | 3.12 | 2.48 |
| 21:00 | 4404 | TSV Schott Mainz vs FV Engers 07 | 1.66 | 4.40 | 4.10 |
| 21:00 | 5616 | Gibraltar vs Liechtenstein | 1.96 | 3.24 | 4.15 |
| 22:00 | 3068 | Antwerp U21 vs OH Leuven U21 | 2.77 | 3.54 | 2.19 |
| 22:00 | 4857 | ADO Den Haag vs Roda Kerkrade | 2.52 | 3.51 | 2.47 |
| 22:15 | 1334 | Deportivo Malacateco vs Antigua GFC | 2.29 | 3.10 | 3.20 |
| 22:15 | 1359 | CDA Aguilas FC vs CAP Ciudad De Murcia | 1.30 | 4.69 | 8.59 |
| 22:30 | 1685 | Lorca Deportiva CF vs Real Murcia B | 2.00 | 3.30 | 3.70 |
| 22:30 | 4065 | Foggia vs Crotone | 2.52 | 3.25 | 2.52 |
| 22:30 | 5450 | Algeria vs Mali | 1.65 | 3.78 | 5.24 |
| 22:30 | 5541 | Attard FC vs Birzebbuga St. Peters F.c. | 1.34 | 4.87 | 6.63 |
| 22:30 | 5821 | Mexico vs Sweden | 2.18 | 3.23 | 3.43 |
| 22:45 | 1914 | Woking vs Oxford Utd | 4.03 | 3.64 | 1.78 |
| 22:45 | 3028 | Albania vs Italy | 6.84 | 3.90 | 1.52 |
| 22:45 | 3360 | Salford City vs Peterborough | 3.65 | 3.50 | 1.90 |
| 23:00 | 1054 | St Andrews vs Zabbar Saint Patrick FC | 1.76 | 3.98 | 3.59 |
| 23:15 | 3467 | Kalkara FC vs Tarxien Rainbows | 4.19 | 4.19 | 1.61 |
| 23:15 | 4781 | Sporting Farense vs CD Trofense | 1.46 | 4.05 | 6.52 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Novemba 16, 2022

Nipashe




UKURASA 29

## Hazard, Nacho wote wawindwa Aston Villa

**HATUWAACHI...**




Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuelekea mchezo wao dhidi ya Namungo FC utakaopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa leo. Kushoto ni kipa wa timu hiyo, Ally Salum na Kaimu Ofisa Habari wa Bodi ya Ligi, Salma Seif. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba, Namungo FC soka kutembea leo

## Kocha wa makipa atua, Mgunda asema mabao sasa yanarudi kikosini huku Nsajigwa akieleza watavunja mwiko...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikiikaribisha Namungo FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara katika Uwanja wa Benjamin Mkapa leo, huku makocha wa timu hizo kila mmoja akijinasibu kupata matokeo chanya, licha ya wote kukiri utakuwa mchezo mgumu kwa kila upande, Wekundu wa Msimbazi hao wamemtangaza kocha mpya wa makipa.

Uongozi wa Klabu ya Simba jana ulitangaza kufikia makubaliano ya kumwajiri Kocha wa Makipa, Chlouha Zakaria, raia wa Morocco kwa mkataba wa mwaka mmoja. Kocha huyo amejiunga na Simba akitokea Klabu ya Dibba Al Fujairah ya Falme za Kiarabu (UAE), ambaye sasa anachukua nafasi ya Mohamed Rachid ambaye mkataba wake ulisitishwa na klabu hiyo Septemba 9, mwaka huu.

Simba inashuka uwanjani ikitaka kuendeleza kasi yake ya ushindi baada ya mchezo uliopita kushinda 1-0 dhidi ya Ihefu FC katika uwanja huo, shukrani kwa Pape Sakho, aliyeifungia, wakati Namungo yenyewe ikitaka kutibu jeraha lake la mchezo uliopita lililotokana na kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Mbeya City ugenini kwenye Dimba la Sokoine jijini Mbeya.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, makocha wa timu hizo kila mmoja alieleza kufanya maandalizi mazuri ya kuibuka na pointi tatu leo.

Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema wako tayari kwa mchezo huo dhidi ya Namungo FC, licha ya kutambua kwamba ligi ni ngumu na itaendelea kuwa hivyo hadi mwisho wa msimu.

Kuhusu timu yake kushindwa kutumia nafasi nyingi wanazotengeneza, alisema tayari amelifanyia kazi tatizo hilo na anatumai leo mashabiki wataona tofauti.

"Ligi ni ngumu, tunashindana na watu wanaotafuta matokeo kama ilivyo kwetu, tumeona madhaifu yetu na kufanyia kazi katika kushindwa kumalizia nafasi tunazotengeneza na tayari tumefanyia kazi ili kurejea katika uwiano mkubwa wa mabao na ushindi.

"Niwahakikishie mashabiki tutaendelea kushindania ubingwa hadi dakika ya mwisho kwa sababu haiwi mwisho hadi iwe mwisho, bado hatujakata tamaa licha ya kupoteza pointi na waliopo juu yetu," alisema Mgunda.

Alisema amewasoma Namungo FC na anaamini itakuwa mechi ya ushindani mkubwa kwa sababu wote wanahitaji pointi ili kila mmoja kujiweka katika mazingira mazuri ya kufikia malengo.

Mgunda alisema mfululizo wa mechi na kuwapo kwa majeruhi wengi ndani ya kikosi chake ni moja ya sababu kubwa ya timu kucheza mechi moja kwa kiwango kikubwa na inayofuata kushuka kiwango.

Simba inashuka dimbani ikiendelea kukosa baadhi ya wachezaji wake ambao ni Nelson Okwa, Peter Banda na Jimmyson Mwanuke ambao bado wako chini ya uangalizi wa madaktari huku John Bocco, Israel Patrick na Jonas Mkude nao wakiwa katika hatihati ya kucheza kutokana na ndio kwanza wameanza mazoezi mepesi

INAENDELEA UK. 31

# Singida Big Stars yapania kuvunja rekodi Yanga kesho

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, amesema wamezisoma mbinu za Yanga na wako tayari kuvunja rekodi yao ya kutofungwa 'Unbeaten', kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara watakapokutana kesho katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pluijm alisema maandalizi yanaendelea vizuri na wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mchezo huo kwa kucheza kwa tahadhari kubwa ili kuvunja rekodi ya Yanga.

Alisema amewasoma na kufahamu ubora wa wapinzani wao hao, hivyo anaamini mchezo utakuwa mgumu kwa sababu wanahitaji kupata matokeo chanya na Yanga wakitaka kuendelea kulinda rekodi yao ya kutopoteza.

**"Nimewasoma Yanga vizuri , ina wachezaji wazuri na mabingwa watetezi, lakini wanarekodi yao ya kuto fungwa, kwa maandalizi ya timu yangu na ubora tulionao ninaimani kitaleta ushindani mkubwa.**

"Kuhusu kuvunja rekodi ninaamini inawekezana kwa sababu ya maandalizi tunayofanya kuelekea mchezo wetu dhidi ya Yanga," alisema Pluijm.

Alisema malengo yao makubwa ni kufanya vizuri kwenye mchezo huo ili kupata pointi tatu kwa ajili ya kufikia malengo yao ya kuendelea kupanda katika nafasi za juu kwenye msimamo.

Singida Big Stars watashuka dimbani kesho majira ya saa 1:00 usiku kusaka pointi tatu ili kuendelea kujiweka katika nne bora, wakati huu ikiwa katika nafasi ya nne na alama 18 baada ya kushuka dimbani mara 10 hadi sasa kwenye ligi hiyo.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >